

UFUNUO, MLANGO WA NNE

SEHEMU YA III



Asante Ndugu Neville. Bwana akubariki pia. Na habari za asubuhi, darasa la Biblia. Basi kila mtu anajisikiaje asubuhi ya leo? Sawa, natumaini. Amina. Kwa namna fulani sisi... hii kidogo ilikuwa ni taarifa fupi tuliyokuwa nayo ya kusema kwamba tungekuwa hapa asubuhi ya leo, kwa sababu sikuwa na...ratiba yangu haijapangwa bado kwamba nitaondoka lini. Na hii kwa kuwa sasa imefanywa kwa muda wa miezi sita ijayo, vema, basi, nilifikiri ni afadhali tufanye ibada asubuhi ya leo maana itachukua muda kabla sijarudi tena, nijuavyo mimi; labda msimu huu wa kupukutika majani.

² Nami nitaninii...tutaondoka sasa juma hili lijalo kwenda Beaumont, Texas, ambako tutaanzia kule chini juma lijalo na kupitia kwenye mikutano ya siku nane ama kumi kule pamoja na shirika la—la wanaojitegemea na makanisa mbalimbali. Kusema kweli umedhaminiwa na makanisa ya *Jesus Name* kule chini Beaumont, Texas, ambako tulikuwa na mkutano mkubwa muda fulani uliopita, mara tu baada ya picha *hii* kupigwa. Nao... Najua wana behewa kule, lenye, ninaamini, mabehewa ishirini na saba...ama garimoshi lenye mabehewa ishirini na saba, wakija kwenye mkutano huko Beaumont. Hapo ndipo meya wa mji alifanya gwaride na kupitia mitaani, na hao wote. Tulikuwa na wakati wa ajabu huko Beaumont, nasi tunarudi huko juma lijalo. Kisha tulikuwa tukitarajia San Antonio, bali hatutakuwa na wakati wa kutosha kwa ajili yake, isipokuwa iwe ni wakati tukirudi.

³ Ndipo tutaenda kutoka huko mpaka Phoenix, Los Angeles, tushuke hadi Long Beach. Kisha turudi, Bwana akipenda, turudi kwenye Pwani ya Mashariki, tupande tuingie Virginia na Carolina ya Kusini. Turudi basi mpaka Bloomington, Illinois. Na kutoka huko twende kwenye Shule ya Sekondari ya Juu ya Lane Tech, juma la mwisho Aprili, Wafanyabiashara Wakristo. Kisha niondoke huko niende kaskazini mwa British Columbia, kupanda kuelekea Alaska, na tuwe huko hadi Juni. Halafu, basi, tunatarajia kuwa na wakati mzuri.

⁴ Tunaomba basi kama ule uchunguzi wa...ambao nimekuwa chini yake kwa muda kwa kodi ya mapato, kuhusu kanisa hapa, utakuwa umekwisha kufikia wakati huo. Kisha tutaninii... Nitaweza kwenda katika nchi za ng'ambo basi ukiwa umekwisha, katika Juni hasa, ambalo litalifanya sawa tu kwa

Afrika; kwenye Juni, Julai, na Agosti, huko—huko Afrika. Kwa hiyo bila shaka ninahitaji maombi yenu.

⁵ Nasi tunakutazamia kuja kwa Bwana. Mambo haya yote ni “ikiwa ni mapenzi ya Bwana,” mnaona. Hatujui, Yeye angeweza... Haya si miongozo hasa, tuliikusanya tu mialiko yote pamoja na kuiombea, tukamwomba Bwana, “Tuelekee wapi?” Ndipo—ndipo ilionekana kana kwamba, basi, siliachii lote kwa nafsi yangu mwenyewe, mimi huwaacha wengine waliwazie, waliombee. Ndipo basi ilionekana kana kwamba sisi sote tuliongozwa kwenda magharibi, kusini na magharibi kwenye wakati huu. Kwa hiyo basi tulikuwa na mialiko ya kila mahali, ndipo basi tukaanza tu moja kwa moja. Basi mahali pa kwanza palipoingia moyoni mwangu palikuwa ni ama Beaumont au San Antonio. Kwa hiyo tukaangalia, nasi tulikuwa na mialiko mahali pote pawili. Pia ninii. . .

⁶ Tulipiga simu mahali pamoja Beaumont. Na kwa kuwa walikuwa na ushirikiano wa makanisa arobaini na mawili, ya United Pentecostals na kadhalika, tulidhani wakiwa na jumba kubwa la mikutano ni afadhali tuwape yapata siku kumi badala ya kutoa kila mahali tano na tano. Nafikiri kama ukiifanyia mahali pamoja namna hiyo ni bora zaidi. Halafu, kuna watu wengi wa—walio wahitaji katika maeneo ya Beaumont na kote katika sehemu hiyo ya mafuta ya Texas, na kwa hiyo tunatarajia wakati mzuri sana huko Beaumont.

⁷ Basi, sasa, hatujaribu kwenda mahali penye vituo vikubwa na mahali pakubwa. Ila sisi hujaribu kwenda jinsi Bwana atakavyotungoza twende, haijalishi ni wachache ama wengi jinsi gani, mradi tu Bwana anatuongoza. Sasa, wakati wowote, Yeye angeweza kutupatia wito wa *Makedonia* nasi tungeondoka uwanjani wakati wowote kwa ajili ya chochote Yeye angetuitia kufanya, mahali popote.

⁸ Basi hakika tumefurahia wakati huu wa ushirika kwenye Neno la Mungu pamoja nanyi watu wazuri. Ninatumaini ya kwamba mtakuwa waaminifu sasa na kuja kanisani na kuyatii mafundisho ya Biblia kupitia ndugu yetu shujaa hapa, Ndugu Neville, ambaye ninampendekeza sana kama mtumishi wa Bwana Mungu, na kuzama zaidi na zaidi pamoja na Mungu, nami nina furaha sana kwa jambo hilo.

⁹ Nanyi kanisa dogo, ninawaonya katika Jina la Bwana Yesu kukua katika neema ya Mungu, mjishikilie imara na kuangalia Kalvari wakati wote, mkiondoa mashina yote ya uchungu moyoni na nafsini mwenu, Mungu apate kuwatumia wakati wowote. Kama kamwe mkijisikia kufanya jambo lolote, ama ufunuo ama kitu fulani kije kwenu kiajabu, kitu cha kuwaonya ama kitu fulani, iweni waangalifu! Shetani ni mjanja na mwenye hila awezavyo kuwa. Mnaona? Liwekeni pamoja na Neno la Mungu na kumtaka shauri mchungaji wenu. Mnaona?

¹⁰ Nanyi mkiona karama na kadhalika zikinyemelea kanisani, na kutenda kazi kwa karama hizi. Kabla hamjaruhusu zianze kutumika na kadhalika, kwanza... Ukizisikia zikikusukuma moyoni mwako... Sasa, adui ni mjanja sana. Mnaona? Na hilo ndilo tu linaloyarua makanisa vipande-vipande kila wakati, ni karama ya kweli ikitumiwa vibaya. Mnaona? Jambo fulani ambalo Mungu anajaribu kufanya, nalo linatumiwa vibaya, lita—kwa urahisi tu litaninii... Sio tu kuwadhuru, bali litalirua kanisa lote. Mnaona? Shaurianeni, lipitishieni katika Biblia tena na tena, kisha mlijaribu muone kama ni Mungu ama siye. Endeleeni tu kulijaribu na kulichunguza, muone kama ni kamilifu kote kote na linalingana na Neno kikamilifu. Ndipo mko sawa, mnaona.

¹¹ Maadamu Neno limesema zitakuwa hapa, na zingetenda kazi kwa njia fulani hii, dumuni moja kwa moja nalo. Kamwe msiende kombo, haidhuru mtu yeyote anafanya nini, jinsi linavyoonekana ni halisi. Endapo haliakisi katika Maandiko kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, achaneni nalo. Msibahatishe hata kidogo, tuko katika siku za mwisho wakati Shetani ni mdanganyifu kabisa awezavyo kuwa.

¹² Samahani kama nikijaribu kupachukua mahali pa bosi; mimi si bosi. Lakini najisikia kwenu kama Paulo alivyosema huko nyuma kuhusu kusanyiko lake wakati mmoja, “Ninyi ndio nyota katika taji yangu.” Nitakapovuka kwenye ile nchi upande ule mwingine, na kukutana nanyi katika hali hiyo iliyotukuka, ninawatakeni msimame pale na kunawiri kama nyota kwenye taji yangu. Mnaona? Na mimi—mimi nawatakeni mwe kule, ninataka kuwa kule.

¹³ Nami ninakumbuka katika ono langu wakati nilipouona Uwepo wa Bwana, ama watu Wake katika Nchi ile tukufu huko ng’ambo, niliangalia kote, nikawaambia... Nao wakaniambia Yeye atanihukumu mimi kwanza kwa Injili ninayohubiri. Nikasema, “Kama vile tu Paulo alivyoihubiri!”

¹⁴ Ndipo hao mamilionni ya watu wakapaza sauti, “Tunategemea hilo!” Mnaona? Mnaona. Sasa, nataka iwe hivyo. Nasi tutakutana kule siku moja.

¹⁵ Wala Mungu hakunituma mimi na Ndugu Neville tuwe mabosi, hata kidogo. Sisi ni ndugu zenu tu, mnaona, walimu katika Injili. Kwa hiyo hebu sote tufanye kazi pamoja.

¹⁶ Na wakati mwingine kama—kama jambo fulani linaloendelea halina budi kutajwa ama—ama kusemwa kitu kulihusu, kurekebisha ama kitu kama hicho, naye mtu aliye na karama hiyo aikatae, kumbukeni tu... aikatae, kumbukeni, hiyo karama haikuwa ya kweli. Haikuwa ni Mungu kwa kuanzia. Roho wa Mungu daima yuko tayari kwa masahihisho, ni mtamu na mnyenyekevu, yuko radhi. Mnaona. Kama akisimama na kusema, “Nitalifanya kwa vyovyote vile,” mnajua jinsi wakati

mwingine... Kumbukeni tu, roho za majivuno si za Mungu. Mnaona? Kwa hiyo mbona kuchukua kabadala wakati kila kitu, dunia nzima, imejaa Utukufu wa Mungu, mnaona, nguvu halisi za Mungu. Kwa nini tuchukue kabadala? Muda umeenda sana katika siku sasa; ila, kumbukeni, Biblia ilisema angekuja kama... mjanja tu awezavyo kuwa, na kuwadanganya walio Wateule kama yamkini. Mnaona?

¹⁷ Na, sasa, wakati mwingine tunafikiri sisi ni Wateule, nami natumaini ndivyo tulivyo, bali hebu tukae tu moja kwa moja na Biblia. Halafu basi kama kila kitu ni sawa na Maandiko, na ni taratibu katika Maandiko, kikileta Utukufu kwa Mungu na heshima ya kanisa, na kadhalika, basi tunajua ya kwamba ni cha Mungu kwa sababu Biblia inakiunga mkono. Bali nadharia yetu tu haitaliunga mkono, haitafaa kitu, hushindwa kabisa.

¹⁸ Kwa hiyo basi kama kitu fulani kimetugusa, haidhuru kinaonekana ni cha halisi jinsi gani, kama si cha kweli, si cha Kimaandiko, kiondolee mbali sasa hivi; maana kuna—kuna Cha halisi kinachongojea, mnaona.

¹⁹ Kwa hiyo, ombeni sasa. Na sikuzote, na lolote mfanyalo, niombeeni. Niombeeni maana sasa tunaingia hudumani kwa mara za mwisho, nionavyo mimi. Sasa tunaenda...

²⁰ Pia, kumbukeni, mambo makuu yanatukia, hayajulikani miongoni mwa walimwengu. Yesu alikuja, akaishi, akafa, na kutolewa sadaka, akarudi Utukufuni, na mamilioni hata hawakujua neno juu yake. Mnaona? Si madoido, mambo makubwa, makuu; ni “Alikuwa kwa walio Wake,” mnaona. Na ninii... “Aliye na sikio, na asikie yale Roho ayaambiayo makanisa.” Sio kwa walio nje, “kwa Kanisa.” Kanisa ndilo linalopata kutikiswa Kwake.

²¹ Nilikuwa nikifikiri tofauti na hilo mpaka siku moja Yeye akasema nami; akafanya nirejee kwenye Neno na kuwazia jinsi ambavyo manabii wote walinena habari za wakati Yohana alipokuja, kasema, “Mahali palipoinuka patashushwa, na kila bonde litajazwa.” Na jinsi nguvu za Mungu zingetenda kazi! Na ninii—ninii... “Milima yote itaruka kama kondoo wadogo waume, nayo majani yatapiga makofi.” Vema, hilo lilionekana kana kwamba jambo fulani kweli litatukia. Mnaona? Basi lilipotukia, ilikuwaje? Maskini jamaa mmoja alitoka nyikani, labda ndevu zimerefuka sana huku amejizungushia maskini kipande cha ngozi ya kondoo. Hapakuwapo na urahisi huko nyikani. Alikuwa huko tangu alipokuwa na umri wa miaka tisa, naye alikuwa na thelathini wakati huo. Akaja akitembea kutoka nyikani, akikanyaga, akihubiri toba, amesimama kwenye matope hadi magotini, labda, ufukoni mwa Yordani. Basi hapo ndipo mahali palipoinuka paliposhushwa na mabonde kujazwa. Mnaona? Ni...

²² Huna budi kuwa na ufahamu wa kiroho. Kumbukeni, Mungu kamwe hakuishi wala hataishi, humu duniani, katika madoido. Yeye anayapinga. Yeye kamwe... Zile jumbe kuu kamwe hazitakuwa “fanyeni *hiki-na-hiki* kikubwa mno na *hiki-na-*...” Halifanyiki jinsi hiyo. Watumishi Wake hawafanyi kazi namna hiyo. Madoido na utukufu Wake ni wa huko juu.

²³ Jana, ama siku mbili zilizopita, nikitoka kwenda Kentucky, huko Kentucky pamoja na rafiki yangu mwema, Ndugu Banks Wood, palikuwapo na polisi mwanamke aliyesimama pale nje, naye akasema, “Jamani, afadhali tupunguze mwendo,” kasema, “yeye ni mkali.”

²⁴ Nami nikasema, “Naam, hiyo ni kweli.” Nikasema, “Wakati taifa linapofikia mahali ambapo mamilioni wameajiriwa kazi nao inawabidi kuwachukua wanawake, kuwafanya polisi na kuwatuma huko nje, na waendesha tekisi na vitu kama hivyo, ni moja ya madoa makubwa mno juu ya taifa letu.” Yeye ana shughuli huko nje kadiri su—kadiri sungura alivyo nazo katika birika la grisi. Mnaona? Kamwe si—si—si mahali pake. Kisha nikasema, “Hilo lilikuwa likinisumbua sana, bali sasa ninaanza kukumbuka, ‘Mbona, si ajabu, huu si—huu si ufalme wetu, sisi si wa ulimwengu huu.’” Hao ni... wewe...

²⁵ Kwa nini wanawake (wanawake wetu) ha—hawana nywele fupi, na vipodozi, na roki, na upuuzi huu wote? Mbona, watu wanaenda kwenye makanisa ya kawaida na kadhalika, wanawazia, “Hilo ni sawa.” Kwa nini? Ni... wao—wao ni Wamarekani; wao ni Wamarekani, wana roho ya Kimarekani. Sisi si Wamarekani, sisi ni Wakristo. Tunaishi... roho yetu ni ya Ufalme mwingine. Kama roho yetu ilikuwa ya ufalme huu basi tungeabudu pamoja na mambo hayo, kisha tungeabudu nyimbo hizi zote za kishenzi na kuabudu roki hii yote. “Palipo moyo wako, ndipo ilipo hazina yako.” Na hazina zetu ziko juu. Kwa hiyo basi tunaenda kwenye Ufalme.

²⁶ Haya siyo makazi yetu, sisi ni wageni tu hapa tukijaribu kuwatoa wenyeji wengine gizani. Nami naingia katika mji fulani na labda ninafanya uamsho wa mji mzima, ninalima tu juma zima ama siku kumi, kwa ajili ya nafsi moja ya thamani huko nje; moja, moja tu anayeketi kule nje.

²⁷ Huenda ukasema, “Mkutano huo ulifanikiwa sana, elfu tano walikuja madhabahuni”; huenda pasiwe na mmoja wao aliyeokoka, si hata mmoja. Mnaona? Na huenda kukawa... Unaweza kuwazia pale, “Ni watu wawili tu waliokuja madhabahuni”; lakini mmoja wao huenda akawa ni kito. Tunavua tu kwa juya kijitoni. Mungu anawachagua samaki, Yeye anajua yupi ni samaki na yupi siye.

²⁸ Kwa hiyo, mnaona, tunahubiri tu. Basi kumbuka mnafanya jambo lile lile katika maskani hii. Lakini sikuzote kumbukeni

jambo hili, “Kondoo wangu waijua Sauti Yangu.” Nayo Sauti ya Mungu ni Neno Lake.

²⁹ Nilikuwa nikiwazia hivi majuzi jinsi watu hawa wanaosema ya kwamba kamwe hakukuwapo na...Dhehebu fulani la makanisa likisema, “Uponyaji wa Kiungu haukuwa ni wa kweli. Kamwe hakuna mtu aliyewahi kupewa karama ya uponyaji wa Kiungu ila Mtakatifu Paulo au mitume, wale kumi na wawili kwenye chumba cha juu. Walipewa karama ya uponyaji wa Kiungu, na hivyo tu. Hilo lilitosha.”

³⁰ Lakini, mnaona, kupitia kwenye chati hii ya ajabu ambayo Ndugu Willie, aliye hapa, alituchorea kiajabu, maskini uzi huo umepitia kwenye makanisa kote kote. Nashangaa yale dhehebu lilo hilo linayosema juu ya historia ya kanisa, kuhusu Ireneo, kuhusu Mtakatifu Martin? Na wafia imani hao wote kote katika wakati, kwa mamia ya miaka baada ya kifo cha wale mitume, walionena kwa lugha na kuwaponya wagonjwa na kuwafufua wafu na kufanya miujiza, kanisa zima. Nashangaa ni nini juu yao, kama ilikuwa tu ni kwa ajili ya mitume?

³¹ Unaona jinsi ilivyo finyu? Hawana ufahamu wa kiroho, hivyo tu. Mnaona, “Vipofu! Wamekufa katika dhambi na makosa!” *Dhambi* inamaanisha “kutokuamini.” Chochote katika kutokuamini ni dhambi. Kama jamaa fulani alikuwa na si—sifa ndefu namna *hiyo* (za D.D., L. maradufu, Ph.D., L.L.D.) kisha anasema “hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu ama ubatizo wa Roho Mtakatifu,” huyo mtu amekufa katika dhambi. Huenda akaweza kuelezea namna zote za siri katika Biblia, bali maisha yake yenyewe (ushuhuda wake) yanathibitisha kwamba yeye amekufa. Amekufa katika dhambi na makosa kwa kuwa yeye ni mwenye dhambi.

³² Dhambi ni kutokuamini. Mtu yeyote anapaswa...Dhambi, sio kufanya uzinzi na kuvuta sigara na kucheza dansi na—na kufanya yasiyofaa na kuendelea namna *hiyo*. Hayo siyo dhambi, hayo ni sifa za kutokuamini. Lakini mwa—mwaminio... Haidhuru kama mtu huyo hanywi pombe, havuti sigara, hafanyi mambo haya, kamwe hajasema neno baya, anatii Amri zote Kumi, angali anaweza kuwa mwenye dhambi mweusi, mnaona, mbaya tu awezavyo kuwa. Kama akikana chochote cha nguvu za Mungu, yeye ni mwenye dhambi! Neno *dhambi* ni “kutokuamini.” Sasa, wewe tafuta kujua, uone kama hilo ni kweli ama si kweli. Asiyeamini Neno la Mungu, yeye ni mwenye dhambi wala hawezi kuingia katika Ufalme wa Mbinguni.

³³ Sasa, loo, niliwazia basi asubuhi ya leo, nikijichukulia jukumu kwa mapenzi ya Bwana, kwa amri ya Roho Mtakatifu, kushuka kuja humu maskanini tena na labda niwaweke ninyi nyote saa mbili au tatu. Lakini ninataka kukimaliza kitabu cha mlango wa 4 wa Ufunuo kabla sijaondoka. Na sasa natumaini haiwachoshi, natumaini ni—ni adhimu kwenu. Ninataumaini

ni jambo litakalowafaidi na kuwasaidia katika siku zijazo zilizo mbele.

³⁴ Na sasa labda... Nilimwambia Billy ashuke aje huku asubuhi ya leo na kusambaza kadi za maombi endapo kulikuwako na wageni wowote miongoni mwetu, kwa sababu tutakuwa tunaondoka, na... sasa, wala sijui tutakaporudi. Mungu ndiye tu ajuaye hilo. Nami nilitaka... niliwazia labda mkutano wa mwisho ikiwa... na wakati aliponiita basi yapata—yapata saa tatu na kusema, “Baba, kuna watu pale wa kuombewa. Nimewauliza, lakini,” kasema, “ni watu ambao—ni watu wanaokuja kanisani wakati wote.”

³⁵ Nikasema, “Basi usisambaze kadi zozote za maombi, mnaona.” Nikasema, “Kwa kuwa hao ni watu... Ikiwa tutawaombea wagonjwa asubuhi ya leo, tutawaita hao watu huku na kuwaombea.” Lakini nikasema, “Kama ni—ni watu wanaokuja maskanini ambao tunawajua... La, ninataka mgeni.”

³⁶ Ndipo akasema basi, alikuja kule nje dakika chache zilizopita wakati aliponikuta nimesimama huko nje, kasema, “Vema, niligawa kadi kadhaa za maombi.” Kasema, “Chache tu mle ndani, nilisambaza kadi za maombi.” Kasema, “Unaweza kufanya lolote utakalo.”

³⁷ Nikasema, “Vema, tutaona jinsi ujumbe unavyoendelea, tuone mahali tulipo, kisha tutaenda. Mimi...”

³⁸ Akasema, “Vema, wengi wa watu walitaka kadi za maombi, hakika, bali” kasema “walikuwa ni watu waliomo mle kanisani.” Mnaona?

³⁹ Vema, tunajua ya kwamba Mungu ni Mungu. Na, jamani, mambo tu Yeye afanyayo! Mbona, si—simu inalia wakati wote, ya watu wa mambo mbalimbali, za mambo madogo madogo wakati mwingine, na jinsi Mungu anavyoyajibu maombi!

⁴⁰ Nashangaa kama maskini mama huyo ama mume wake yuko hapa kutoka huko chini New Albany, waliomleta maskini yule mtoto mdogo aliyesongwa roho hivi majuzi usiku, kwa nimonia, nyumbani kwangu yapata saa sita, saba? Kule, mzima. Huyo mtoto mchanga yukoje? [Mtu katika kusanyiko anasema, “Sawa!”—Mh.] Mzima, vema, sawa.

⁴¹ Hebu niwaonyeshe tu, mnaona, kwamba ni jambo fulani ambalo msingelijua, lisiloendelea wakati Roho Mtakatifu anapozungumza. Fred Sothmann, ndugu yetu wa thamani, Fred; nilimsikia akisema “Amina” muda mfupi uliopita, lakini nisingeweza kuona alipo. Yuko wapi? Yuko hapa? Hapa, papa hapa, Ndugu Fred Sothmann. Na kuonyesha jinsi ilivyo rahisi... Alikuwa na marafiki waliokuwa wakija, ambao walikuwa ni Ndugu Welch Evans, nadhani, sijui. Walikuwa na trela kule; walikuwa wamefunga milango naye Fred akazipoteza

funguo, naye alikuwa amezitafuta kila mahali wala asingezipata mahali popote. Naye Ndugu Welch alikuwa akija moja kwa moja. Kwa hiyo siku ikaja wakati ambapo alikuwa afike na kadhalika, wasingeweza kupata ule ufunguo mahali popote, kwa hiyo akapiga simu tu nyumbani, kasema, “Ndugu Branham, funguo ziko wapi? Tuzipate wapi?”

⁴² Sasa, hilo linaweza likawakwaza baadhi yenu, kwa mtu kuuliza swali kama hilo. Lakini ngoja kidogo, mnawakumbuka wale wana wa Yese waliokuwa wakiwatafuta wale nyumbu? “Kwa hiyo kama nilikuwa na zawadi mkononi mwangu, ningeipeleka kule chini na kuonyesha . . . kumwuliza, ningempa nabii, na labda angetwambia mahali hao nyumbu walipokuwa.” Mnakumbuka hilo?

⁴³ Ndipo alipokuwa akitembea barabarani wakakutana na nabii. Akasema, “Unawatafuta hao nyumbu.” Kasema, “Hapo, wewe rudi nyumbani,” kasema, “wamerudi tayari.” Hiyo ni kweli?

⁴⁴ Nikaomba. Fred akaenda kule na kuziokota hizo funguo. Jambo ndilo hilo. Mnaona?

⁴⁵ Ndugu Ed Daulton, uko wapi? Yuko wapi Ed Daulton? Najua yuko hapa mahali fulani, nilimwona muda mfupi uliopita. Loo, nyuma katika . . . yule pale. Alinisikia kwa mawasiliano ya ndani ama mfumo wa mawasiliano ya hadhara. Hivi majuzi usiku simu iliingia naye Ndugu Ed alikuwa katika matatizo mabaya. Nilitaka kumsaidia. “La,” kasema, “ninataka tu wewe unwombe Mungu.” Nikamwomba Bwana amsaidie. Ndipo kesho yake mke wake akapiga simu, mtu fulani alikuja akawasaidia. Vema. Hiyo ni kweli, Ndugu Ed?

⁴⁶ Mnaona, Yeye ni Mungu tu. Hivyo tu, Yeye ni Mungu tu. Mnaona, Yeye ananinii tu . . . Ni wakati wote sikuzote kutoka mahali pamoja hadi pengine. Haijalishi ni shida gani, Yeye ni Mungu. Hatuzunguki, tukijivunia mambo hayo, hatupaswi kufanya hivyo. Kamwe usiache mkono wa kulia ama mkono wa kushoto ujue yale mkono wa kulia unayofanya. Tunazungumza miongoni mwetu ila hatuyatangazi hayo huko nje mahali fulani. Kwa sababu hayo ni majivuno ya kibinafsi, kama vile, “Mungu angeweza tu kulifanya kwa ajili ya mtu mmoja.” Angeyafanya kwa mtu yeyote ambaye ata—ambaye atamwamini. Ni kusadiki, imani! Chochote—chochote unachotaka kufanya, chochote kilicho mawazo yako, kipeleke kwa Mungu. Yeye—Yeye—Yeye—Yeye hukidhi kila kitu. Hiyo si ni kweli? Kwa hiyo Yeye hujibu maombi. Yeye ni . . . Mungu ni Baba anayejibu maombi.

⁴⁷ Sasa, kwa hiyo basi katika . . . Nikawazia, nikifunga katika mikutano hii ya mwisho na kadhalika, kama tulivyokuwa . . . tunavyofanya, tunge—tungekuwa na labda utambuzi kwenye mkutano wa mwisho, Bwana akipenda, na labda kwenye

wakati wa mkutano huo. Hatujui kabisa yale atakayofanya. Ninalipenda jinsi hiyo. Usipangilie jambo lolote, mwache tu Yeye afanye atakavyo.

48 Sasa, fungueni mlango wa 4 wa Kitabu cha Ufunuo, kisha mwisimamishe ile saa ya ukutani.

49 [Mtu fulani anaomba anene—Mh.] Naam. Naam, ndugu. [Ndugu huyo anaanza kushuhudia. Sehemu tupu kwenye kanda.] Hakika, ninaamini hilo. Kabisa, ninaamini hilo.

50 Hapa, Ndugu Welch Evans, nafikiri huyo ni yeye aliyeketi pale pale nyuma. Hebu mimi . . . Tunapofungua Ufunuo 4.

51 Hapa si muda mrefu uliopita, ninyi nyote mlisikia na kusoma katika magazeti kuhusu kundi hili la majambazi Louisville ambalo huiba magari, wanayapeleka huko chini Kentucky mahali fulani, upesi sana. Na huko Kentucky hata haikubidi kuwa na hati, watakutengenezea moja huko Kentucky. Kwa hiyo unaninii tu . . . jambo pekee likupasalo kufanya ni kulipeleka kule na kuliuza. Kwa hiyo watayachukua magari haya na kuyapeleka kule na kayapaka rangi tena, na kuyaleta magari hayo na kuyauza. Yote unayopaswa kuwa nayo ni namba ya bloku yako na wao—wao watakutengenezea hati. Kwa hiyo wanachukua tu gari mtaani na kuliondoa upesi sana na kukimbia kulipeleka dukani mahali fulani, wanabadilisha tu kitu hicho chote kwa jumla, mnaona, na—na kulipaka rangi tena na kadhalika, wanalichukua na kuliuza. Kuna utapeli wake, na hasa sana kote Marekani, na sehemu yake kubwa—kubwa iko Kentucky. Nilisoma makala kwenye gazeti hapa sio muda mrefu uliopita kulihusu.

52 Vema, Ndugu Evans wa thamani, mkubwa, mwenye moyo mwema na familia yake, wakiendesha gari kote kutoka Macon, Georgia, huku juu kila Jumapili kuisikia Injili. Loo, ni waaminifu jinsi gani, na ni marafiki halisi jinsi gani! Halafu yeye huenda kwenye Kafeteria ya Miller ambako . . .

53 Siitangazii Miller, bali hakika nafikiri ya kwamba wana chakula kizuri kuliko vyote Kentucky; Louisville, Kentucky, kwa vyovyote vile. Kadiri . . . Simaanishi ninyi nyumba za binafsi ambamo nimekula huko, sasa, ninamaanisha (mwajua) huko nje. Nami hula huko, pia. Ninaweza kuilisha familia yangu huko rahisi kuliko ninavyoweza kuwalisha nyumbani. Hiyo ni kweli.

54 Kwa hiyo ninaenda kule, na kwa hiyo Ndugu Evans anaingia ndipo anajipatia chakula na kugesha gari lake huko nje. Anapotoka (pamoja na nguo zake zote) na familia na wote hao, hakuwa na gari lolote wala chochote. Lote lilikuwa limeenda. Vema, maskini jamaa huyo, Ndugu Evans ni mtu kama sisi sote, ana biashara ndogo huko chini, yeye huyashughulikia magari, ananunua magari yaliyoharibika na kuyatengeneza. Yeye ni

maskini, naye hutumia pesa zake kuja huku maana anaamini Injili ya namna hii. Ninaomba ya kwamba Mungu atawatumia mjumbe kule chini mahali fulani, apate kuwasaidia huko chini katika nchi hiyo.

⁵⁵ Sasa, Ndugu Evans alikuja huku, kwa hiyo hakujua la kufanya. Alikuwa amewaarifu polisi nao wasingeweza kulipata. Kwa hiyo akaja nyumbani, yeye na Ndugu Fred na hao wengine, tukaketi chumbani na kulizungumzia. Nikasema, “Sasa...” Hivyo ndivyo tunavyofanya, tunaketi chumbani, tuone linalotukia, halafu basi tunamwendea Mungu. Kwa hiyo tulipomwomba Bwana, “Kumgeuza mtu huyo aliyekuwa na hilo gari, kumgeuza na kumrudisha nyuma, popote alipokuwa.”

⁵⁶ Kwa kawaida wanayapeleka karibu na Bowling Green ama mahali fulani, wanayatoa moja kwa moja kutoka sehemu moto moto hapa, mnaona, kusudi wapate... mpaka wapate kuyapaka rangi upya na kuyatengeneza. Hili lilikuwa ni gari zuri, nafikiri ni gari dogo la abiria na mizigo. Hiyo ilikiwa ni kweli, Ndugu Evans? Lilikuwa ni ga—gari dogo la abiria na mizigo.

⁵⁷ Kwa hiyo, na kwa hiyo lililotukia, tuliinama tukaomba. Naye Bwa—Bwana akatupa ushuhuda, yote ilikuwa ni shwari, kila kitu sawa. Kwa hiyo basi nguvu za Bwana zikatushukia. Ndugu Evans anatoka na kuanza kutoka, akaongozwa kwenda kupitia njia fulani.

⁵⁸ Akarudi moja kwa moja hapa Jeffersonville. Hilo gari liliibiwa huko Louisville; hili hapa gari lake limeegeshwa pale likiwa na petroli ya kutosha tu kulipeleka...loo, iliyotumika, kuweza kulipeka huko chini karibu sana na Bowling Green na kurudi. Wakatoka kwenye gari, wakalisimamisha gari, wakauacha ufunguo ndani yake, wakaondoka tu na kuliacha limeegeshwa hapo, papa hapa Jeffersonville ambako angeweza kulipata; sio Louisville, hapa Jeff., wakalirudisha mpaka huku.

⁵⁹ Mwajua, Bwana anaweza kuwafanya ndege wantii, anaweza kuwafanya wanadamu wantii, anaweza kumfanya adui Wake amtii. Yeye... Naam, bwana, Yeye ni Mungu. Hili hapa gari lake limekaa bila kitu kimoja kupotea, likiwa na karibu tu nusu tangi ya petroli ambapo alikuwa amefika karibu Bowling Green, ndipo Roho Mtakatifu hapana shaka alisema, “Geuka! Rudi nyuma ulirudishe gari hilo Jeffersonville. Liweke papa hapa mtaani, na kuliegesha papa *hapa*, (maana nitamtuma moja kwa moja upande *huu* na huku juu *hivi* kulitafuta).” Hiyo ni kweli, Ndugu Welch? Hiyo ni kweli. Mnaona.

⁶⁰ Yeye ni Mungu! Yeye huyajibu maombi, Ndugu Roy. Ananinii tu... Hiyo ni, Ndugu Slaughter, hilo ni jambo lile lile tu, Yeye alimponya maskini mbwa wako. Nami ninajua ya kwamba Yeye huponya, Yeye huyajibu maombi, angali anafanya miujiza, Yeye angali ni Mungu, daima alikuwa ni Mungu, daima atakuwa ni Mungu!

Yeye—Yeye ni Mungu kwenye paa la nyumba,
(Ni kitu gani, ndugu huyo huimba hapa
kanisani?)

Mungu jikoni, Mungu huko nje shambani,
Mungu katika gari, Yeye ni Mungu kila mahali,
Yeye ni Mungu kote—kote na kote, Mungu.

⁶¹ Loo, ni ajabu jinsi gani! Tungeanza kuhubiri baada ya kitambo kidogo wala hatulifikii somo hili.

Vema, na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo wa maombi.

⁶² Baba yetu wa Mbinguni mwenye neema, tunalipenda sana Neno Lako Takatifu mpaka mioyo yetu inawaka tu ndani yetu, wakati tukijua ya kwamba Roho Wako anashuka miongoni mwetu na hapo anazungumza nasi, nayo mioyo yetu inanyoshwa na kumshika. Nasi inaonekana tunajisikia vizuri sana juu Yake, Bwana.

⁶³ Na kujua ya kwamba katika saa hii yenye giza ambamo kuna kuchanganyikiwa kwingi... Kama vile nabii alivyosema, “Katika siku za mwisho kungetokea njaa,” kitu kama hiki, “sio kwa ajili ya chakula wala maji, bali kwa ajili ya kulisikia Neno la kweli la Mungu; nao watu wangesafiri kutoka mashariki kwenda magharibi, kaskazini na kusini, wakitafuta kupata Neno la kweli la Mungu.” Neno! Neno ni nini? Yesu ni Neno, “Neno lilifanyika mwili likakaa miongoni mwetu.” Kuona kule kudhihirishwa kwa Neno halisi la Mungu likidhihirishwa kulingana na Maandiko na kutimizwa, kwamba, jinsi watu wangesafiri na kutafuta na wangeshindwa kulipata Hilo. Ee Mungu, tuna furaha sana, tuna furaha sana ya kwamba tulimpata Yeye miaka mingi iliyopita, akiwa ni wa thamani kwa moyo wetu, na kuona ya kwamba hatujachanganyikiwa hata kidogo.

⁶⁴ Ee Mungu, Wewe ulisema, “Hao wamjuao Mungu wao watafanya mambo makuu katika siku hiyo.” Nasi hapa katika siku za mwisho, tukiyaona mambo yote ambayo Yesu alisema yangetimia, yakidhihirishwa moja kwa moja miongoni mwetu. Ishara zenyewe, maajabu, miujiza ikifanyika, ikifanyika kama vile tu Yeye alivyoifanya. Kama Yeye alivyosema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

⁶⁵ Basi, Bwana, Wewe unaturuhusu, kwa Roho Mtakatifu, kuliendea Neno hilo na kupata mambo hayo halisi na kuyafunganisha katika Kalvari, kwa Neno, na kuona ya kwamba ndani Yake tunao utimilifu. Na utajiri na baraka na utukufu na yote yanaenda Kwake Yeye astahiliye, ambaye alikuja na kukitwaa kile Kitabu kutoka kwenye mkono wa kuume wa Yeye akitiye juu ya Kiti cha Enzi, na kukikalilia Mwenyewe, kwa kuwa alichinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

⁶⁶ Tunanena juu Yake asubuhi ya leo, Baba. Tunaomba ya kwamba Wewe utabariki mioyo yetu. Jalia Roho Yake itende kazi miongoni mwetu na kutubariki, na kuimarisha ujuzi wetu, na kuponya ugonjwa miongoni mwetu, na kutupa neema ya kushinda.

⁶⁷ Pia, Mungu, ninapoenda huko nje hudumani kukabiliana na adui, jalia nitambue ya kwamba nimezingirwa kila saa kwa maombi. Loo, jinsi ninavyoitategemea ngome hiyo, adui akikaribia, bali najua ya kwamba ngome hiyo inashikilia kwa maana akina mama na baba, na wavulana kwa wasichana, Wakristo, waliozaliwa mara ya pili na wenye ujuzi, watu wanaoelekea Mbinguni wako magotini mwao wakiomba, “Ee Mungu, tupe ukombozi!” Pia, Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia kutoka kwenda katika kambi za adui huko nje na kushinda kila nafsi ya thamani inayongojea. Litekeleze, Bwana, na uwatoe gizani waingie kwenye Nuru. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁶⁸ Sasa, katika mlango wa 4 wa Kitabu cha Ufunuo. Tulimalizia kwenye mlango wa 3, na hebu kwa namna fulani tuwe na kicho nami nitajaribu kutowaweka kwa muda mrefu kupita kiasi. Lakini katika mlango huu wa 3, Kanisa lilipaa juu kama mfano, wakati Yohana alipotwaliwa juu. Kanisa lilipaa juu, na tangu wakati huo na kuendelea ni kuwashughulikia Israeli, mpaka kule Kuja tena. Hivi hamwoni jinsi ilivyo? Watu siku hizi, jinsi walivyo, “Kitu fulani kikuu kitautikisa ulimwengu mzima na kila kitu.” Hilo si la kimaandiko! La, bwana. Linalofuata katika mpangilio wa mambo ni kule kuondoka kwa Kanisa. Someni katika nyakati za kanisa, muone kile. . .

⁶⁹ Sasa, mambo haya mengine yanayopaswa kutukia, ni katika ule wakati wa Sherehe za Arusi wakati Kanisa likiwa Utukufuni. Mungu anarudi kufanya maajabu makuu, maajabu ya kimataifa na kadhalika, kwa Wayahudi, hayaendi kwa Kanisa hata kidogo.

⁷⁰ Kwenye mlango wa 3 unamalizika wakati wa Kanisa. Hiyo ni kweli. Nao huo wakati wa Kanisa unaishia na uchache mdogo sana hata tunaona. . . Sikilizeni tu hapa. Ni—nilisoma hili tena asubuhi ya leo, karibu linirarue tu vipande-vipande, mahali na mwelekeo wa Kristo mwishoni mwa wakati wa Kanisa, panapopatikana katika kifungu cha 20 hadi kifungu cha 22 cha Ufunuo 3. Wazieni juu ya Kristo, wakati wa mwisho, mahali alipo! Yuko wapi mwishoni mwa wakati wa Kanisa? Nje ya kanisa Lake, amesukumwa nje na madhehebu na kanuni za imani. Mwelekeo Wake ni upi? Akijaribu kurudi ndani. Hiyo ni hali ya kusikitisha!

⁷¹ Ndipo tunaona hapa, “baada ya mambo haya,” alisikia Sauti iliyokuwa ikisema naye ambayo. . . Loo, ilikuwa ni nini? Roho

aliondoka duniani. “Baada ya mambo haya,” unanza mlango wa kwanza ama—ama kifungu cha kwanza:

Baada ya mambo haya nikaangalia, na, tazama, mlango ulifunguliwa mbinguni: . . .

⁷² Ufunuo 4:1, baada ya Kanisa kuondoka, ndipo M—Mlango ukafunguliwa. Nasi tumepitia hayo yote na kuona kwamba huyo alikuwa ni Kristo, alikuwa ni Mlango. Ndipo Sauti ile ile iliyokuwa ikitembea katikati ya vinara saba vya taa vya dhahabu pia ilikuwa ni Sauti ile ile aliyoisikia Mbinguni, ikisema, “Njoo huku.” Yohana akapaa juu. Iliwakilisha Kanisa likiondoka katika Unyakuo.

⁷³ Yohana alipaa juu katika Roho, akachukuliwa Mbinguni na kuona mambo yote kimbele ambayo Mungu aliahidi na kuwaambia wanafunzi, “Imewapasaje nyinyi ikiwa atakaa hata nijapo?” Aliona kule kuja kwa Bwana na yale yangetukia. Yeye aliona duniani yale yangetukia duniani hata kwenye Unyakuo wa Kanisa, naye alitwaliwa juu na kuonyeshwa kote kote hata kupita ule Utawala wa Miaka Elfu. Loo, si ajabu hiyo?

⁷⁴ Sasa, tulimwacha Jumapili iliyopita kwenye mlango wa 4 na kifungu cha 4.

Na viti ishirini na vinne vilikizunguka kile kiti cha enzi: na juu ya vile viti nalion wazee ishirini na wanne, wameketi, wamevikwa mavazi meupe; na juu ya vichwa vyao walikuwa na taji za dhahabu.

⁷⁵ Sasa, tuliona ya kwamba hawa walikuwa ni wazee. Mzee kamwe halitumiwi kwa Malaika wala Kiumbe chochote. Ni mwanadamu aliyekombolewa, wazee! Maana hao. . . Viti vya enzi, taji, na milki kamwe hazitajwi kwa, kwa Malaika. Lakini taji na viti vya enzi, na kadhalika, vinahusu wanadamu. Nao hawa wazee walitiwa taji na kuvikwa mavazi na wameketi kwenye viti vya enzi. Nasi tuliwaona kwenye sehemu zingine za Maandiko kwamba walikuwa ni wale mitume kumi na wawili na walikuwa ni wale wazee wetu kumi na wawili. Wakiwa *Ishirini na wanne*, ambayo inamaanisha “ishirini na wanne”: mitume kumi na wawili, wazee wetu kumi na wawili.

⁷⁶ Pia, tuliona, hata ule mji ulioshuka kutoka kwa Mungu Mbinguni. . . Baada ya dunia kulipuliwa na yote kuvunjika vipandevipande na hakuna kilichosalia duniani ila majivu ya volkano (hayo tu ndiyo yatakayosalia), hakutakuwako na bahari tena. Bahari itakauka.

⁷⁷ Kama nilivyokuwa nikizungumza na mtu fulani jana usiku, ama jana, mahali fulani, dunia wakati mmoja ilisimama juu namna *hii*, kweli, kulizunguka jua, joto sawa kote juu na chini. Huko juu kwenye maeneo ya barafu ya Uingereza, unaweza kulipua huko chini futi mia tano na kupata mitende. Ilitukia mara moja, ikaigandisha kama kugandishwa kwa baridi sasa.

Kama *kujikausha* kwako, na kadhalika, na *kugandisha* kwako na jokofu yako ambayo huzihifadhi stroberi na kadhalika kwa miaka na miaka ijayo. Mnaona? Hivyo ndivyo vile ilivyokuwa wakati huo. Upesi kulikuja yale maangamizi yaliyotangulia gharika na kuifunika dunia yote kwa maji. Basi yalipofanya hivyo, nguvu za atomiki ziliutikisa ukatoka kwenye mizingo yake, nayo yakaganda kabisa na hapo ikakaa. Mnaona? Chimba chini na unaweza kuipata, huko juu karibu na ukanda wa aktiki na kadhalika, mitende na kadhalika. Ilionyesha ya kwamba wakati mmoja ilikuwa imekaliwa vizuri, kimpangilio. Lakini sasa imetikiswa ikarudi.

⁷⁸ Sasa, mahali ninapofikiri Mungu aliyapata maji hayo, wakati Mwanzo kinapoanza, Mwanzo 1, “Nchi ilikuwa ukiwa, tena tupu, nayo maji yalikuwa juu ya vilindi. Roho ya Mungu ilitulia juu ya maji na kusema, ‘Iwe nuru.’” Mungu akatenga basi nchi na maji, ambayo yaliifanya dunia. Lakini dunia nzima ilifunikwa. Sasa, yale Yeye aliyofanya, alininii tu... kupitia kwenye angahewa, Yeye alininiii tu... angahewa ni... Angahewa imejaa haidrojeni na oksijeni, na kadhalika. Ndipo aliinua tu juu kutoka duniani na kuitenganisha. Hapakuwapo na bahari juu ya nchi wakati huo. Mungu aliinyunyizia dunia maji, hata hakukunyesha. Yeye aliinyunyizia maji kwa chemchemi na kadhalika, unyunyizaji. Ndipo wakati Yeye... Jambo pekee Yeye alilofanya wakati huo...

⁷⁹ Wakati mwanadamu alipoilipua ikatoka kwenye mzingo wake, nje upande mmoja, ni kitu gani kilichotukia? Iliirusha nyuma katika... joto *hapa* chini, na baridi *huko* juu. Na joto na baridi, limbikizo gani? Lihisi hapa kwenye hayo madirisha sasa hivi, joto humu ndani na baridi upande wa nje. Mnaona hilo jasho? Nayo mvua si kitu ila jasho, kutokwa na jasho. Nayo maji ni majivu. Na kwa hiyo basi wakati hiyo...

⁸⁰ Ninaupenda wimbo huo:

Uliweka mkono Wako, Bwana wa thamani, juu
ya uwanda mpana wa majani,
Ukaweke mkono Wako wa ajabu kwenye safu
ya milima;
Bwana, ulimwaga chemchemi,
Ukainua mlima,
Loo! Bwana, weka mkono Wako wa thamani
juu yangu.

Uliyafanya mawingu, ukayafanya mawingu
yaliyofanya mvua,
Kutoka kwa mvua ukafanya bahari,
Kutoka kwa bahari ukayaleta mawingu
Kutupa uzima tele;

Unaishikilia dunia na mbingu kwa amri Yako,
Bwana,
Loo! Naomba uuweke mkono Wako wa
thamani juu yangu. (Loo, ni mkuu jinsi gani!
Naam, Mungu wa Mbinguni.)

⁸¹ Halafu katika wakati huu mkuu, ni kuegemea nyuma namna *hii* sasa, Naye alitutolea ahadi, “Hakuna maji tena, bali moto wakati huu!” Badala ya kuitupa... Waliitupa dunia mbali na jua, hakika, ikawa baridi. Ukiitupa kwenye jua, itateketea. Na kama tu vile alivyoiangamiza kwa maji na kuweka upinde angani, Yeye “asingefanya hivyo tena,” sasa, Yeye alitupatia ahadi Yeye “ataiteketeza kwa moto!” Kwa hiyo unakuja ambapo dhambi na madoido yote na uchafu wote. . .

⁸² Na sio muda mrefu uliopita nilikuwa nikiendesha kwenye mbuga pana. Kama mvulana mdogo nilikuwa nikiwazia, ninachukua vitabu vyangu vya historia na vya jiografia na kuwazia juu ya nyanda kuu za magharibi. “Siku moja,” nilisema, “nitaishi kule, kwa amani na utulivu ambapo hapana dhambi, nami nitatembeatembea makondeni na kuwinda kama Mhindi. Nami ni—nitaishi kule, maisha ya amani, siku zote za maisha yangu.” Lakini sasa ni . . . mzungu amekuwa kule. Popote mzungu aendapo, dhambi inamwandama. Yeye ndiye mwuaji wa kinyama mkubwa kuliko wote na mwuaji wa watu wote duniani, ni mzungu. Yeye ndiye haini wa rangi zote!

⁸³ Hapa si muda mrefu uliopita kwenye gazeti (Ndugu Thom hapa, kutoka Afrika), niliona makala kwenye gazeti majuma mawili yaliyopita, ninaamini ilikuwa, naye alisema . . . walisema, “Ikiwa Wamarekani wangali wanakubaliwa kwenda Afrika, katika miaka kumi kuanzia sasa yule simba mkubwa wa Afrika atakuwa amemalizwa kabisa, wale ndovu.” Hawa haini wakisika risasi kila mahali wawezapo. Picha ya dume wawili wakubwa wakijaribu kumshikilia dume mwingine aliyejeruhiwa. Inaonekana kana kwamba machozi yanatiririka kutoka machoni mwao. Hawakutaka ninii . . . dume hawakutaka huyo wa kike afe. Na kila mmoja akimshikilia huyo jike ubavuni mwake, namna *hii*, asije akaangukia . . . ardhini. Alipigwa risasi ikamrarua vipande-vipande. Jamaa anayepiga risasi kitu kama hicho hastahili kuwa na bunduki mkononi mwake. Hiyo ni kweli. Huna akili za kutosha kuitumia.

⁸⁴ Sasa, miaka kadhaa iliyopita, nikijaribu kulifukuza kundi, la kulungu, lielekee kwa rafiki yangu mwema, Ndugu Roy Roberson na hao wengine kule nyuma, wakati nilipokuwa kiongozi huko Colorado; nilijua tulikuwa na kundi zuri. Mimi na Jeff tulikuwa nao huko juu kwa miaka na miaka, karibu kulungu themanini kwenye hilo kundi. Wakawaruhusu baadhi ya hawa jamaa wa ofisini kutoka Denver waje huko wamevaa suruali hizi za makunjo, na mguu wenye kamba. Hao ni wawindaji. Hmm!

Hawa hapa wanakuja huko juu, kundi, katika magari ya jipu na vitu kama hivyo, wakaingia kwenye eneo letu huko.

⁸⁵ Nami nilikuwa nikiwasukuma hawa kulungu mlimani nyuma yao, karibu maili moja ama mbili, nao walikuwa wakiendelea kukusanyika. Inakubidi kuwatenganisha, wale mafahali wakongwe wakubwa na kadhalika; usipofanya hivyo, unavunja kundi lako. Hao ni kama tu kuwafuga ng'ombe ama chochote kile. Wanyama mwitu wanapaswa kuwa vivyo hivyo kwetu. Si kuwalenga shabaha. Ukitaka kulenga shabaha wana uwanja wa shabaha huku nje wa kulengea. Hiyo ni kweli. Ni fedheha kuua vitu kikatili namna hiyo. Ni dhambi, ni uovu!

⁸⁶ Nami nilihesabu risasi mia moja na ishirini na tatu kutoka kwenye bombom, kitu kama hicho, wakiwarushia risasi kutoka mabegani mwao. Na kesho yake asubuhi, Ndugu Banks Wood hapa pamoja nami, tulipanda mlimani, nikahesabu sehemu kumi na tisa zilizojaa damu. Hawakujua chochote juu ya kuwinda; unaweza kumpiga risasi mnyama mkubwa kama huyo, unaweza kumpiga kwa kilindi vya kutosha kumwua. Nao waliachilia tu, "bum, bum, bum," wanampiga risasi mmoja kisha huyo mwingine. Mbona, watakufa. Na ninii. . . Baada ya wao kupatwa na homa, kama ungewapata hawafai kitu, wanaharibika mara moja; nao wala mizoga, mbwa mwitu na kadhalika, wanawala. Sehemu kumi na tisa zenye damu, mafahali wakubwa, kwato kubwa *hivi* kote, na damu ikibubujika futi mbili ambapo ilikuwa imetobolewa hivyo kwa bunduki hizo. Hawapaswi kumruhusu haini kama huyo kuwa na bunduki mkononi mwake. Hiyo ni kweli. Hana akili ya kutosha kutumia bunduki. Loo, ni dhambi kubwa mno, kufanya kitu kama hicho.

⁸⁷ Hilo ni baya sana, bali huyo ni Mmarekani. Canada, ninyi watu wa thamani kutoka Canada! Kama Marekani ikizidi kuendelea, Canada itakuwa duni kama Marekani, baada ya kitambo kidogo. Hebu nenda karibu na mipaka ya Canada popote pale, nawe una hayo mazingira ya Marekani. Marekani hii ndiyo kahaba wa mataifa. Hivyo ndivyo ilivyo hasa, na itakuwa mbaya zaidi kuliko hapo zamani sasa. Inafikia mwisho wake! Biblia inazungumza juu ya maangamizi yake, inasema jinsi itakavyokuwa. Marekani: duni sana, imeoza, ni chafu, haifai kitu. Hiyo ni kweli kabisa. Imekuwa taifa kuu. Imeubeba ujumbe wa Injili. Ni kitu gani kinachoifanya kuwa jinsi ilivyo? Kwa sababu imeukataa Ujumbe wa Injili, na kuzikataa zile Kweli. Ni ya kuchukiza sana. Litajuta, msijali. Niliona jambo hilo katika ono kama BWANA ASEMA HIVI! Inakuja. Italipia dhambi yake.

⁸⁸ Huko nyuma wakati Marekani ilipokuwa Marekani, ilikuwa ni taifa kuu. Lililo kuu sana ulimwengu ulilopata kujua tangu Israeli, lilikuwa ni Marekani, bali hakika limejichafua sasa. Limeukataa Ujumbe. Halijachukua kitu ila tu. . . Sasa

limejifanya... Mnaweza kuona mahali lilipo sasa. Kila mtu anajua hilo, katika uchaguzi uliopita inaonyesha mahali msimamo wake wa kiroho ulipo. A-ha. Haijui.

⁸⁹ Sasa, hawa wazee wameketi kwenye kiti cha enzi pamoja na taji yake. Sasa, kifungu cha 5, tutaanza:

*Na katika kile kiti cha enzi kunatoka umeme...
ngurumo... sauti: na taa saba za moto zilikuwa mbele
ya kile kiti cha enzi, ndizo Roho saba za Mungu.*

⁹⁰ Loo, napenda hili! Nanyi je? Loo, ninajisikia tu kana kwamba koti langu linanikaa, mwajua. Ninaninii tu... wakati... Loo, ninamaanisha katika koti la kiroho, hakika, mwajua. Vema.

⁹¹ “Kutoka katika kile Kiti cha Enzi.” Hebu tuzungumze juu ya Kiti hiki cha Enzi sasa kwa dakika chache. Hiki hakikuwa ni Kiti cha rehema. Kiti cha rehema kimekwisha; hakuna rehema tena, ni bila rehema. Tutaendaje... Kiti cha hukumu kitakuwaje kiti cha hukumu cha Kristo, kiti cha hukumu, Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi? Kutakuwako na rehema basi? Hakuna hata chembe moja ya rehema itakayotolewa. Kwenye Kiti cha Enzi cha hukumu ungepiga makelele “rehema” mpaka usiweze kupiga makelele tena, na ni kwamba, ni afadhali hata ungepigia makelele huko nje hewani mahali fulani, maana hakuna rehema tena.

⁹² Sasa ndiyo siku ya rehema! Sasa, hebu turudi kwenye Agano la Kale hapa kwa muda mfupi tu tuone rehema ni nini. Turudi nyuma tuone nini kilichokipata Kiti hiki cha Enzi. Kiti hiki cha Enzi, hakika, ni kiti cha—cha hukumu. Na ninii... sababu ya kuweko na rehema leo, ni kwa sababu kiti cha rehema kimenyunyiziwa upatanisho. Damu! Na maadamu Damu iko kwenye kiti cha hukumu basi si hukumu tena, ni rehema, kwa sababu kitu Fulani kilikufa kipate kuizua hukumu. Kama mkiliona, semeni “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Mradi Damu iko kwenye kiti cha rehema, ilionyesha ya kwamba kitu Fulani kilikufa kipate kuizua hukumu. Bali Kanisa likinyakuliwa, kiti cha rehema kinakuwa kiti cha hukumu!

⁹³ Huku, mwajua, kwenye Agano Jipya hapa, pia, “Na madhabahu.” Hapo ndipo ba—baraza la wazee... madhabahuni, hakimumu akiketi madhabahuni. Sasa, kiti hicho cha hukumu madhabahuni kilijaa moshi. Ilikuwa ni kitu gani? Kama vile Mlima Sinai, hukumu! Rehema ilikuwa imeondoka kwenye Ki—Kiti cha Enzi cha Mungu. Mungu atauhukumu ulimwengu bila rehema. Ni wangapi wanaojua hilo?

⁹⁴ Kitu cha pekee atakachotambua siku hiyo, ni kitu gani? Damu. Hicho ndicho kitu pekee kilichomridhisha Mungu mwenye hasira.

⁹⁵ Adamu na Hawa walishona nguo nzuri tu kama Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, ama Mpentekoste yeyote angeweza kushona, iliufunika uchi wao. Lakini Mungu angeweza kuona kupitia hiyo, kwa hiyo akaua kitu fulani na kuzichukua hizo ngozi zilizokufa za—ngozi za mnyama aliyekufa na kuufunika. Ilibidi damu ichukue mahali pake. Hiyo iliizuia hasira Yake, Yeye aliona hiyo damu ndipo akarudi nyuma, kwa sababu kitu fulani kilikuwa kimeumwaga uhai wake. Ee Mungu!

⁹⁶ Wazia hilo! Kitu pekee kitakachomzuia Mungu ni Damu. Na kuna Damu moja tu ambayo itamfanya arudi nyuma, na hiyo ni Mwana Wake Mwenyewe. Akiona hiyo ni Damu ya Mwana Wake Mwenyewe, atarudi nyuma. Maana hiyo ndiyo karama ambayo... Mungu amempa Mwanawe, kuwakomboa wale aliowajua tangu zamani, nayo inamrudisha Mungu kutoka kwenye hukumu Yake. Lakini hiyo Damu ikiondolewa, na wote waliojulikana tangu zamani wameletwa wakaingia kwenye huo Mwili wa thamani, Kanisa Lake limefanywa tayari na kunyakuliwa, basi hasira ya Mungu iko juu ya watu.

⁹⁷ Loo, ndugu, kamwe usipende kusimama hapo! Acha nisimame mbele ya bombom, acha nikatwe vipande-vipande, acha nikatwe kwa msumeno inchi kwa inchi, acha chochote kitukie (kama vile kiapo cha Mashujaa wa Columbus), acha walipasue tumbo langu na waiwashe salfa na kila kitu kingine ndani yangu, na mikono na miguu yangu ikatiliwe mbali, chochote kile, bali *kamwe* nisisimame kwenye ile Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi mbele za Mungu.

⁹⁸ Loo, hebu nichukue kiti hiki kidogo cha enzi *hapa* mbele ya kiti cha Kristo na kuikubali Damu Yake. Sina cha mkononi, Bwana.

Si—sijui chemchemi nyingine
Si chochote ila Damu ya Yesu; (Hiyo tu ndiyo
ninayojua habari zake.)

Hii ndiyo tumaini langu lote na ngome,
Si chochote ila Damu ya Yesu.

⁹⁹ Si ajabu Eddie Perronet... walizikataa nyimbo zake. Wakati alipokuwa Mkristo, Mkristo hodari, hawakutaka kununua nyimbo zake. Siku moja akasema, “Nitaandika mmoja, na siku moja... ambao wataupokea.” (Nao watu walikuwa wakitaka kitu cha kisasa zaidi katika nyimbo za kidini.) Siku moja pale Roho Mtakatifu akachukua mamlaka, ndipo akanyakua kalamu na kuandika:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!
Malaika na wamsujudie;
Leteni taji ya kifalme,
Mkamvike taji Bwana wa mabwana.

Kwa kuwa kwake Kristo, Mwamba wenye
imara, nasimama;
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao,
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

¹⁰⁰ Kama ni kanisa, kama ni rafiki, kama ni adui, kama ni taifa, kama ni utajiri, kama ni umaskini, kama ni mema, ama chochote kilicho, sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao! Hilo ndilo jambo pekee, hatimaye litaondoka. Bali:

...Kristo, ule Mwamba wenye imara,
nasimama;
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.
(Kumbukeni hilo.)

¹⁰¹ Angalieni! Hebu twende kwenye Mambo ya Walawi 16, na tusome nyuma, huko nyuma kabisa nyuma ya Biblia sasa, katika sheria za Walawi, na tuone hapa kwenye Mambo ya Walawi—Mambo ya Walawi mlango wa 16. Na tuanzie kwenye kifungu cha 14 cha mlango wa 16. Loo, na—napenda kuuchukua wakati wangu kwenye mambo haya, kuyaleta. Mambo ya Walawi kumi na n-...ama Mambo ya Walawi 16:14.

Kisha atatwaa baadhi ya damu ya yule ng'ombe, na kuinyunyiza kwa kidole chake juu ya kiti cha rehema (Juu ya kiti cha rehema! Angalieni, tutaingilia jambo hili baada ya kitambo kidogo)...upande wa mashariki;...

¹⁰² Msilisahau neno hilo “Mashariki”? Yesu anatokea wapi? Mashariki, katika wingu la Utukufu. J-u-a huchomozea wapi? Mashariki. M-w-a-n-a atatokea wapi? Mashariki. Kiti cha rehema kilikuwa kimewekwa wapi? Upande wa mashariki. Ni kwa nini nimewafanya ninyi nyote mketi *hivi* mmeelekea mashariki? Kwa nini? Madhabahu yako upande wa mashariki. Tataliona baada ya kitambo kidogo, jinsi lilivyo zuri, nitalichora. Niliwaomba wengi kadiri nilivyoweza walete makaratasi na kadhalika, kupata ramani hizi katika dakika chache. Vema:

...atainyunyizia...upande wa mashariki; na mbele ya kiti cha rehema atainyunyiza...damu kwa kidole chake mara saba.

¹⁰³ Loo, hilo si linapendeza? “Mara saba upande wa mashariki.” Ni kitu gani? Zile Nyakati Saba za Kanisa zitafunikwa kwa Damu. Haleluya! Damu ya Yesu Kristo imetosha kabisa ndani yake, jana, leo, na hata milele, na kwa kila wakati, kumwoko kila mwenye dhambi, kumponya kila mgonjwa, kufanya kila mwujiza, kila ishara kutimia. “Mara saba,” huko nyuma kabisa katika Agano la Kale, miaka elfu moja mia nne na tisini kabla ya kuja kwa Kristo. Wazieni hilo! Ishara, “mara saba ataninii...”

Kisha atamchinja yule mbuzi. . . sadaka ya dhambi, aliye kwa ajili ya watu, na kuileta damu yake pamoja na. . . ndani ya pazia, na kwa damu hiyo atafanya vile vile kama alivyofanya kwa damu ya ng'ombe, . . . kuinyunyiza juu ya kiti cha rehema, na mbele ya kiti cha rehema:

Naye atafanya upatanisho kwa ajili ya mahali patakatifu, kwa sababu ya. . . ninii. . . mambo machafu ya wana wa Israeli, kwa ajili ya makosa yao katika dhambi zao zote: naye atafanya vile vile kwa ajili ya hema ya kukutania, ikaayo pamoja nao iliyo katikati ya—ya machafu yao.

104 Ilikuwa ni kitu gani? “Kiti cha rehema.” Wako wapi sasa? Na mle ndani ya lile sanduku kulikuwa na nini? Torati. Nayo torati, kukiuka amri moja ilikuwa ni kifo pasipo na rehema. Lakini kwa kuwa ungeweza kupata rehema, ile damu ilipaswa kuwa juu ya madhabahu. Wanakinyunyizia kiti cha rehema. Nacho kiti cha rehema ni madhabahu ambapo unapiga magoti na kuomba rehema. Mungu na azuie kamwe tusiyaondoe makanisani mwetu, yale madhabahu ya mtindo wa kale ambapo watu wanaweza kupiga magoti na kumwomba Mungu rehema. Nayo rehema ni tajiri, na inatiririka kwa njia huru kutoka kwa Damu ya Bwana Yesu. Sasa, pia, hiyo ni rehema. Hicho ni kiti cha rehema.

105 Bali mnaona hapa ndani, hakikuwa ni kiti cha rehema, kwa kuwa kulikuwako na “radi na ngurumo na sauti.” Hakuna radi na ngurumo kwenye neema. Hiyo ni hukumu.

106 Hebu tufungue Kutoka, mlango wa 19 wa Kutoka na kifungu cha 16. Kutoka, mlango wa 19 wa Kutoka, na hebu tuanze kwenye kifungu cha 16:

Ikawa. . .

Sikilizeni vile. . . hapo Mungu alipopanda juu ya Mlima Sinai:

Ikawa siku ya tatu, wakati wa asubuhi, palikuwa na ngurumo. . . radi, na wingu zito juu ya mlima, na sauti ya baragumu iliyolia sana. (Sauti ya baragumu ni nini? Ni malaika mkuu.) Watu wote. . . (Sikilizeni!). . . watu wote. . . waliokuwa kituoni wakatetemeka.

107 “Hukumu!” Whiu! Walikuwa wameenda pale naye Mungu alikuwa amewapa neema ya kusafirira, bali walikuwa wamedai wapewe torati. Wao. . . Mungu alitaka wawe wasio na umadhehebu; wao walitaka kuunda dhehebu kutoka kwake, kitu fulani wangeweza kubishania, badala ya kumfuata tu Mungu na kuishi chini ya utawala Wake, chini ya nguvu Zake. Neema ilikuwa imemtoa nabii, neema ilikuwa imetoa upatanisho (mwana-kondoo), neema ilikuwa imetoa mambo haya yote,

na hata hivyo wao walitaka hukumu. Walitaka jambo fulani wangaliweza kufanya.

¹⁰⁸ Mungu alisema, “Wakusanyeni pamoja, nitawafanya wajue ni kitu gani. Nitawaonyesha ni kitu gani.” Someni! Sikilizeni! Nayo sauti ya baragumu ikazidi kuwa kubwa zaidi na zaidi mpaka ikaitikisa dunia. Mnaona jinsi hukumu ilivyo. Siitaki hiyo. Nipe rehema!

¹⁰⁹ [Ndugu Fred anasema, “Ndugu Branham?—Mh.] Na... [Ndugu Branham?”] Naam? [“Andiko hilo—hilo la mwisho ulilosoma lilikuwa ni lipi?”] Hilo lilikuwa ni Kutoka, m—m—mlango wa 19 na kifungu cha 16, Ndugu Fred. Kutoka 19:16.

¹¹⁰ Sasa, angalieni kifungu cha 17:

Musa akawatoa hao watu katika kituo, akawaleta ili waonane... Mungu; (Loo, jamani! Ninataka kukutana Naye katika amani, si jinsi hiyo.) wakasimama pande zote za chini za ule mlima. (Huko mbali kabisa.)

¹¹¹ Kumbukeni, mlima huo ulikuwa na mistari iliyochorwa kuuzunguka. Hata kama ng’ombe aliugusa mlima huo, ilibidi afe papo hapo, hawezi kuja Mbele za Mungu. Naye Mungu... “Naye Musa akawaleta hao watu.”

¹¹² Sasa, kifungu cha 18, kifungu kifuatacho:

Mlima wa Sinai wote pia ukatoa...moshi, kwa sababu BWANA alishuka juu yake katika moto:... (Ukitoa moshi tu na kuwaka moto kama tanuru.)

¹¹³ Yeye alishuka vipi? Sio katika Utukufu Wake wa Shekina, bali katika hasira ya hukumu Zake.

...na ule moshi wake ukapanda juu kama moshi wa tanuru, mlima wote ukatetemeka sana. (Ndugu, sitaki kuwa kule!)

Na hapo sauti ya baragumu ilipozidi kulia sana, na kulia zaidi na zaidi, Musa akanena, naye Mungu akamwitikia kwa sauti. (Musa alinena; sio hao watu, wao walikuwa wakitetemeka vibaya sana.)

BWANA aka—akashukia juu ya mlima Sinai, juu ya kilele cha mlima: BWANA akamwita Musa aende hata kilele cha mlima; Musa akapanda juu.

Ndipo BWANA akamwambia Musa, Shuka chini, uwaonye watu, wasije wakapasua njia waje kwa BWANA kutazama, kisha wengi miongoni mwao wakaangamia.

¹¹⁴ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Watu huketi nyuma ya kanisa na kumcheka mtu anayenena kwa lugha, ama kucheza katika Roho; wamekwisha, wamemkufuru Roho Mtakatifu, wametiwa muhuri milele! “Yeyote atakayenena neno dhidi ya Roho Mtakatifu hatasamehewa kamwe katika ulimwengu huu,

wala ulimwengu ujao.” Usimkodolee macho! Kaa mbali Naye ama umkubali!

¹¹⁵ Afadhali tuliache Andiko hilo. Endeleeni kusoma, hayo mengine, mwone yale Mungu aliyosema. Nao watu wakasema, “Loo, Musa, wewe nena. Usiache Mungu anene tena! Laiti sasa tusingalikuwa tumeomba hili.” Mnaona? “Wewe nena nasi, Musa. Mungu akinena, sisi sote tutakufa.” Mnaona, Mungu alikuwa amefanya upatanisho.

¹¹⁶ Sasa, “Sauti ya Kiti cha Enzi.” Angalieni katika Kiti hiki cha Enzi, “mbele ya Kiti cha Enzi kulikuwako na nyota saba,” Sauti ya zile nyota. “Sauti nyingi,” mnaona. Kulikuwko na zingine katika Ufunuo 4 hapa, ama 5, tunaona, “Na kutoka kwenye kile Kiti cha Enzi kulitoka radi, ngurumo, na sauti nyingi.” Sio sauti moja; “sauti nyingi,” wingi. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akinena na kanisa, akijiakisi Mwenyewe kupitia zile Roho saba. Wakati wale wenye upako wa kweli wa Mungu wanaponena, ni Sauti ya Mungu! Kuikataa Hiyo ni kuondoa kinara cha taa. Mnaona? “Sauti nyingi,” Sauti ya Nyakati Saba za Kanisa (hapa pembeni,) sauti nyingi zikizungumza pamoja na ngurumo na radi.

¹¹⁷ Siku hizi wao ni ninii sana, “Vema, hatuamini katika kusema ‘kuzimu’ mimbarani.” Loo, rehema! Salala! Hmm! Tunahitaji watu wa Mungu, watu ambao hawatasitasita!

¹¹⁸ Sasa, kila mtu hawezi kuwa mhubiri, bali unayo sauti. Na endapo huwezi kuwahubiria watu somo... Kama wewe ni mhubiri, umeitwa mimbarani kuhubiri. Kama hujaitwa, ungali ni mhubiri, bali *waishie* watu mahubiri. Acha mahubiri yako *yaishiwe*, nayo ni Sauti ya Mungu ambayo itasababisha lawama kwa hao wanaokataa. Wanasema, “Hakuna mtu anayeweza kuyaelekezea kidole maisha ya huyo mwanamume ama mwanamke. Wao ni watamu, wanaishi... Wao... Kama kuliwahi kuwa na mtu wa Mungu, ni mwanamume huyo ama mwanamke huyo.” Unaona, ishi mahubiri yako. Usijaribu kuyahubiri ikiwa hujaitwa kuwa mhubiri; utachanganyikiwa kabisa, kwa vyovyote vile, na kutatanika, na utawavuruga watu, wala hutajua... Vema, uta—utajiangamiza na kuwaangamiza, pia. Yaishi tu mahubiri yako!

¹¹⁹ Mhubiri ameitwa kuhubiri yake, na kuyaishi pia. Endapo huwezi kuyaishi, basi acha kuyahubiri. Lakini unapaswa kuyaishi mahubiri yako.

¹²⁰ Vema, hapa zilikuwapo “sauti.” Loo, jinsi tunavyohitaji katika Jeffersonville maelfu ya sauti zinazoishiwa, ngurumo ya Mungu ikinguruma katika utamu na utakatifu, usafi, maisha yasiyoghoshiwa, zikitembea huku na huku duniani leo hii, pasipo na lawama. Naam, bwana, Wakristo halisi, hao ni ngurumo dhidi ya adui. Ibilisi hajali jinsi unavyoweza kupiga makelele kwa sauti kubwa; ibilisi hajali jinsi unavyoweza kuruka ama jinsi unavyoweza kufanya *hivi* ama kupaza sauti.

Bali linalomuudhi ibilisi ni kuona hayo maisha yaliyotakaswa, matakatifu yaliyowekwa wakfu kwa Mungu; mwambie chochote, mwrite chochote, ni mtamu tu awezavyo kuwa na anasonga mbele tu. Loo, jamani! Hilo humtupilia mbali, hiyo ndiyo ngurumo inayomtikisa ibilisi.

¹²¹ Kama tu vile, “Vema,” unasema, “laiti angeweza kuhubiri kama Billy Graham ama Oral Roberts, ama mtu fulani, msemaji mashuhuri mwenye ushawishi mwingi, angekuwa. . .” Loo, la! Wakati mwingine ibilisi hulicheka tu hilo. Yeye hashughuliki na hilo kwa vyovyote vile. Unapata theolojia—theolojia yote uliyotaka na mafunzo yote ya seminari, naye ibilisi anaketi tu kitako na kulicheka. Lakini anapoona hayo Maisha!

¹²² Waangalie wale wanafunzi kule chini, mtoto yule mwendawazimu siku ile aliyekuwa na kifafa, wakisema, “Toka ndani yake, ewe ibilisi! Toka ndani yake, ewe ibilisi! Toka ndani yake, ewe ibilisi!”

¹²³ Ibilisi akiketi pale, kasema, “Sasa, hivi si mnajiaibisha sana? Sasa, mnaona kile mnachofanya? Yesu aliwaambia, Yeye aliwaagiza, mwende mkanitoe. Hakuna hata mmoja wenu anayeweza kufanya hivyo.”

¹²⁴ Lakini, ndugu, walipomwona Yeye akija, Mtu akija kwa utulivu. Aa-ha. Loo, jamani! Haikumbidi kusema lolote. Huyo ibilisi tayari alikuwa ameogopa papo hapo. Alijua ilimbidi kuondoka, kweli, maana hayo hapo Maisha yanakuja; sio tu mahubiri, bali Maisha. Kasema, “Toka ndani yake.” Loo, jamani! Hilo lilitosha! Kwa utulivu; Yeye alijua alichokuwa akizungumzia, alijua alichokuwa akifanya.

¹²⁵ Sasa, “Sauti nyingi,” sauti za zile baragumu saba, zilikuwa ni sauti za zile nyota saba, wajumbe saba. Lakini sasa angalieni hapa:

. . . na . . . taa saba . . . mbele ya kile kiti cha enzi, ndizo
Roho saba za Mungu.

¹²⁶ “Taa saba.” Hebu tuchore kidogo hapa, Kiti cha Enzi, mahali patakatifu, kusanyiko. Na papa *hapa* palikuwapo (moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba) nyota saba, taa saba, wajumbe saba, Roho saba; sio kwa jumla kumaanisha ya kwamba Mungu yuko katika Roho saba, bali “madhihirisho saba ya Roho Mtakatifu yeye yule.”

¹²⁷ Roho Mtakatifu yuko wapi? Hapa kwenye Kiti cha Enzi, akiangaza katika kila wakati wa kanisa. Wakati *huu* wa kanisa unaakisi *hivi*, zile sauti za Mungu, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaona, saba, kulikuwako na “sauti nyingi.” “Na taa saba zikiwaka,” Roho saba, “ndizo Roho saba za Mungu.”

¹²⁸ Mnakumbuka Jumapili chache zilizopita tuliifikia, ile almasi kubwa? Lakini imekatwa katika njia nyingi mbalimbali

ipate kuakisi moto na nuru kutoka kwake. Hivyo ndivyo, “Yesu Kristo ni mwanzo wa kuumba kwa Mungu,” Ufunuo 1. Hiyo ni kweli? Basi Mungu aliumbwa lini? Yeye ni mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Naye Mungu ni wa Milele. Hiyo ni kweli? Lakini wakati Mungu alipoumbwa... hapo mtoto mchanga aliyechukuliwa mimba katika tumbo la uzazi la mama mmoja, bikira. Naye akaanza kuzikuza seli hizi ndani yake apate kumzaa mtoto huyu mchanga, huo ulikuwa ndio mwanzo wa kuumba kwa Mungu, “Kwa kuwa Mungu alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu, kisha akawa *Imanueli*, ‘Mungu pamoja nasi,’ ule mwanzo wa kuumba kwa Mungu.”

129 Ndipo katika Kito hicho kikuu kilichotoka mavumbini... kwa sababu Yeye alifanyizwa kwa mavumbi. Hiyo ni kweli? Yeye alikula chakula kama nifanyavyo mimi, alikula chakula kama ufanyavyo wewe. Ambapo, mavumbi ya mwili, Yeye alifanyika kalisi, chumvi, petroli, nurulimwengu, bali ndani Yake mlikaa Nuru ya Milele. Si ajabu wale mamajusi waliambia ile Nyota, “Tuongoze kwenye Nuru yako kamilifu.”

130 Walikuwa tu wakiakisi Mwangaza wa Nuru Moja kamilifu. Na Yeye huyo hapo, ile Nuru kamilifu ya Mungu, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Sasa, mle ndani alikuwamo Yeye...

131 Yeye aliwezaje kujiakisi Mwenyewe kwenye nyota Zake za duniani, baada ya wale mamajusi kumwona Mbinguni, nao wakawa roho zihudumu hapa duniani? “Alijeruhiwa (yule Almasi kuu, akakatiliwa mbali) kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa uovu wetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa mapigo Yake sisi tuliponywa.” Ilikuwa ikifanya nini? Kuakisi!

132 Mtu yeyote anayedai kuwa ni mtumishi wa Mungu, ambaye hukana uponyaji wa Kiungu na nguvu Zake, hapati nuru yake kutoka kwenye Almasi hiyo, hapati nuru yake kutoka kwenye Kiti hicho cha Enzi. Kwa sababu inamwakisi Yeye yule yule jana, leo, na hata milele kupitia kwenye zile nyota saba na zile Nyakati Saba za Kanisa.

133 Loo, Mungu asifiwe! Nadhani inafaa kwa mhudumu kumwabudu Mungu kutoka mimbarani, pamoja na kutoa shukrani na sifa na heshima na nguvu. Loo, ni halisi jinsi gani, jinsi inavyoisisimua tu nafsi yangu mpaka ninajisikia kama ningeweza kupiga makelele, na kukimbia na kuruka juu niwezavyo, kwa sababu kuna kitu Fulani ndani yangu ambacho kimenibadilisha kutoka nilichokuwa. Mimi siko vile ninavyopaswa kuwa, wala si vile ninavyotaka kuwa, bali ninajua nimebadilishwa kutoka vile nilivyokuwa. Jambo fulani limetendeka, jambo fulani limetukia!

134 Na kusimama hapa na kuona Neno hili la Milele ambalo limestahimili kila dhoruba! Walipojaribu kuzichoma Biblia na kila kitu, ilistahimili moja kwa moja vivyo hivyo, kwa kuwa

ilisema, “Mbingu na nchi zitapia, bali Neno Langu halitapita kamwe.”

¹³⁵ Huku juu karibu na Chicago sasa, basi Bi—Biblia imewekwa juu ya mimbara ya kanisa. Huko nyuma kabisa kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia, mmishenari mmoja alikuwa nayo ndipo jamaa fulani akaongoka, naye alitaka kumpa huyo mmishenari Biblia yake, kasema, “Siwezi kukupa hii, mama yangu alikuwa amenipa hii.” Kasema, “Mimi, nitakapofika nyumbani, nitakutumia moja.”

¹³⁶ Akaanza kuvuka bahari nayo nyambizi ya Ujerumani ikailipua hi—hiyo meli. Kamwe hawakupata hata kipande chake. Ndipo miaka miwili baadaye, huko chini kabisa pwani, waliona kijisanduku kikielea. Baadhi yao walidhani huenda kikawa ni kitu kilichozama, na kwa hiyo wakakitoea hicho kijisanduku wakakifungua, jamaa wawili waliokuwa wakitembea pale. Basi mle ndani, kitu cha pekee kilichonusurika, hiyo hapo ile Biblia aliyokuwa akimtumia yule mmishenari. Imewekwa mimbarani hapa karibu na Chicago leo hii, katika kanisa la Methodisti. “Mbingu na nchi zitapia, bali Neno Langu halitapita kamwe.”

¹³⁷ Mnamo wakati wa yale mafuriko hapa, katika mwaka wa 1937, maskini kanisa hili, wakati sakafu za matope na kadhalika zilizokuwa ndani yake, tungeweza kuabiri juu yake hapa ka—katika mtumbwi wa makasia. Mafuriko yalipanda juu. Ndipo, vema, usiku huo wakati nilipokuwa nimehubiri Injili na nilikuwa nimeiacha Biblia yangu imefunguliwa mimbarani nilipokuwa nimeenda nyumbani; nikibashiri ya kwamba mafuriko yangekuja, nilisema, “Nilimwona akipima futi ishirini na mbili juu ya Barabara ya Spring hapa chini.”

¹³⁸ Mzee Ndugu Jim Wiseheart na hao wengine walinicheka. Unakumbuka hilo, Ndugu George? Nilisema... Yeye—yeye alisema, “Loo, Billy, katika mwaka wa ’84 yalikuwa takriban inchi sita tu juu ya Barabara ya Spring.”

¹³⁹ Nikasema, “Nilimwona mtu akishuka kutoka angani, akachukua kijiti cha kupima na kukibandika pale kwenye Barabara ya Spring, kasema futi ishirini na mbili.”

Akasema, “Wewe umesisimkwa tu.”

Nikasema, “Sijasisimkwa! Ni BWANA ASEMA HIVI!”

¹⁴⁰ Waulizeni ilikuwa ni futi ngapi juu ya Barabara ya Spring. Futi ishirini na mbili ka—kamili! Kabisa.

¹⁴¹ Nayo maskini Biblia hiyo mahali ilipokuwa imehubiriwa usiku huo... Ikaanza kunyesha, mafuriko yakivunja na kuingia na kadhalika, ndipo maskini kanisa hili... Viti vilienda juu moja kwa moja hata darini, Biblia ikaenda moja kwa moja hata darini, yakienea kote huku pamoja na hayo maji yote yakiipeleka juu. Mimbara ikaenda moja kwa moja juu. Vikashuka chini moja kwa

moja; na kila kiti kikarudi moja kwa moja mahali pale pale, nayo Biblia ilikuwa imerejea mahali pale pale, na maji hayo yote, na ingali imefunguliwa, sura ile ile mahali pale pale.

142 “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.”

143 Jinsi Biblia hiyo ilivyoelea kwenye hayo maji ya chumvi kwa muda wa miaka miwili pasipo hata kuyachafua maneno ndani Yake! Maneno ya Mungu ni ya kweli. Amina.

144 Ninakumbuka baada ya hapo, mzee Ndugu Jim Wiseheart aliridhika sana na hilo, kila mara angesikia maumivu mkononi mwake. . . Alipata shida fulani alipofikia umri wa yapata miaka sabini na mitano, akapatwa na baridi yabisi. Uchungu ungeanza kuuma *hapa*, yeye angekimbia na kuchukua Biblia, na kuifungua, na kuiwekelea pale, uchungu mwingine *hapa* chini. Nilikuja kule siku moja naye alikuwa amejikelelea Biblia nyingi sana nisingeweza kumwona Ndugu Jim, alikuwa amefunikwa kabisa na Biblia! Akasema, “Ni ahadi ya Mungu!” Jambo ndilo hilo.

145 “Mbingu na nchi zitapia, bali Neno Langu halitapita kamwe.”

146 Nakumbuka yule jamaa mzee aliyekuwa akija huku kuniona. Na hakuna yeyote wa watu wake hapa sidhani. Nami nilikuwa nikimsaidia kidogo, mwajua, kimaisha, maana alikuwa ni mzee na alihitaji pesa naye angeshuka na kuja. Akasema. . . Siku moja nilikuwa nikiondoka kwenda Canada, nikageuka, nikatoka tu nje ya lango, naye akasema, “Billy, mwanangu, moja ya siku hizi utarudi naye maskini Uncle Jim hatakuwa akijikokota huku na huku kwenye barabara hii tena.” Hiyo ilikuwa ndiyo mara ya mwisho. Nilipokuwa Canada, nikapata barua ya simu; alikuwa amekufia kuko huko nje mikononi mwa Dada Morgan. Alishikwa na mshtuko wa moyo, nao wakamkimbiza hospitalini, akamtazama kisha akafa.

147 Dada Margie, yupo hapa asubuhi ya leo? Kwa kawaida huwa anaingia. Nyote mnajua. Mojawapo ya hali mbaya sana za ugonjwa wa kansa ambapo huko kwenye Hospitali ya Baptisti amekuwa amekufa kwa muda wa miaka kumi na saba, kwenye kumbukumbu za Kliniki ya Matibabu huko, juu ya “kufa kwa kansa,” miaka kumi na saba iliyopita. Yeye anaishi katika Barabara kuu ya Knobloch 412, akiwa muuguzi wa hospitali huku nje. Loo, neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu!

148 Jim Tom Robertson, mwanasheria katika Louisville, nasi sote tunamfahamu Jim Tom. Hilo ndilo lililomfanya kuuamini Ujumbe huu, alipanda kule. Naye baba yake ni mmoja wa viongozi wa hao wafanyakazi huko hospitalini. Alienda na kuichunguza, aone iwapo ilikuwa ni kweli kwamba alikuwa akifa kwa kansa, na alikuwa amekatiwa tamaa na kurudishwa

nyumbani, nao wakawaza kadiri wajuavyo alikuwa tayari amekufa. Basi baba yake akaichunguza, na ni kweli. Ndipo Jim Tom akasema, “Ni uongo; yeye ameketi papa hapa sasa, ninaweza kuwapeleka kwake.”

¹⁴⁹ Loo, loo, Yeye—Yeye ni Mungu halisi, sivyo? Nina furaha sana Yeye anaweza kusamehe makosa yetu, nanyi je? Inatufanya tumpende kwa moyo wetu wote.

¹⁵⁰ Viti vya enzi, radi...Nini? “Taa saba,” ama taa, ama nyota saba, zinazoitwa “Roho saba,” ikimaanisha madhi... madhihirisho saba ya Roho Mtakatifu ya Nyakati Saba za Kanisa kwenye viti saba vya rehema kwa ajili ya watu. Hivi hapa: viti saba vya rehema, viti saba, makanisa saba, nyota saba, madhihirisho saba, Roho saba, taa saba. Loo, jamani, jinsi ambavyo Mungu ni mkamilifu sana! Kila...

¹⁵¹ Zimewekwa pale katika tarakimu za Biblia; tarakimu za Biblia ndizo kitu kikamilifu sana kilichopo duniani. Huwezi kupata dosari moja kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, katika tarakimu za Biblia. Hakuna kipande kingine cha maandishi kilichoandikwa ambacho huwezi kupata dosari moja kabla hujasoma vifungu vitatu; bali sio katika Bi-...

¹⁵² Wamekuwa wakijaribu kwa zaidi ya miaka mia mbili kuongeza fungu moja la maneno kwenye Sala ya Bwana, ama kuondoa moja kutoka Kwake. Ni kamilifu! Huwezi kuongeza zaidi wala kutoa tena Kwake. Wamekuwa wakifikiri wangeiboresha kidogo hiyo sala. Watajaribu kuchambua *hili* ndani Yake, na kuliweka *lile* ndani Yake, ama kutoa *hili* ndani Yake; kamwe si sahihi. Mnaona, Hilo ni kamilifu! Njia zote za Mungu ni kamilifu.

¹⁵³ Kwa hiyo sisi si wakamilifu, bali Yeye alisema “Iweni wakamilifu kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu.” Tunawezaje kuwa? Kupitia kwa Damu ya thamani ya Yesu Kristo, kujisahau wenyewe na kuishi tu ndani Yake. Haya basi. Jinsi lilivyo la thamani!

¹⁵⁴ Vema, kifungu cha 6 sasa kama tunaweza kukifikia. “Taa saba.”

Na mbele ya kile kiti cha enzi...kulikuwa na bahari ya kioo, kama bilauri; na katikati ya kile kiti cha enzi, na pande zote za kile kiti, walikuwako wenye uhai wanne, wamejaa macho mbele na nyuma. (Loo, jamani! Angalieni hili!)...wenye uhai wamejaa macho—wamejaa macho mbele na nyu-... (Sasa, ngojeni.)...mbele ya kile kiti cha enzi...kulikuwa na bahari ya kioo kama bilauri; na katikati ya kile kiti cha enzi, walikuwako wanne...na pande zote...kile kiti, walikuwako wenye uhai wanne, wamejaa macho mbele na nyuma.

¹⁵⁵ Sasa, “bahari ya kioo.” Ninyi ambao mtaninii... Mimi... Hii si ishara sana hapa, bali ninataka kuifuta hii kwa dakika moja. Sasa, sasa tunataka kusoma hapa kidogo tu. Bahari ya kioo imeonyeshwa kwa mfano katika hekalu la kale, kwa kuwa Musa aliamriwa na Mungu kujenga hekalu duniani kama alivyoiona mbinguni. Kila mtu anajua hilo. Vema.

¹⁵⁶ Na hebu tu nichore kidogo hapa sasa, nikisema, *hapa* lilikuwapo lile sanduku katika Agano la Kale, vema, hapo pengine, hapo paliitwa “Patakatifu pa patakatifu.” Na mahali panapofuata hapa palikuwa ni madhabahu, ambapo paliitwa “mahali patakatifu.” Na moja kwa moja mbele ya *hapa* palikuwapo na “bahari ya shaba,” ndivyo inavyoitwa. Kwa maneno mengine, palikuwa ni mahali ambapo dhabihu... dhabihu zilioshewa—zilioshewa hapa kabla hazijapokelewa... madhabahuni; kwenye madhabahu ya shaba, ama madhabahu ya shaba ambapo dhabihu iliteketezwa.

¹⁵⁷ Sasa, tunataka kuangalia hili sasa ambapo ninii... mahali yalipokuwa. Na, sasa—sasa, katika bahari hii ya kioo... iliyokuwa mbele ya Kiti cha Enzi na mbele ya mahali patakatifu. Ninii tu... Sasa kumbukeni, vinara saba vya taa vya dhahabu viliwekwa *hapa* namna hii, ndipo vikaingia kwenye birika. Mnaona? Sasa, hivyo ndivyo vinavyoakisi nuru kutoka mahali patakatifu mpaka *hapa* nje. Sasa, kama ninyi... la, sio lazima muandike hili isipokuwa mnataka kuandika, lakini hiyo ni... Nina kitu kingine hapa nilichokichora mwenyewe, nilichotaka kuwaletea. Lakini sasa, mnaona, *hii* iliitwa bahari ya shaba; haikuwa kubwa hivyo, iliwekwa takriban mahali pake hekaluni. Iliwekwa namna *hii* hapa, ilikuwa ni bahari ya shaba, lilikuwa ni birika lililotengenezwa kwa shaba ambapo walizioshea dhabihu. Kabla dhabihu hazijateketezwa ama kukubalika, ilibidi zioshwe.

¹⁵⁸ Loo, hilo si lingeweza kufanya mahubiri sasa hivi, Daktari. Loo, jamani! Hilo si—hilo si lingeninii tu... Ndio kwanza linijie, “kuziosha.” Kabla dhabihu yoyote kupokewa kwa Mungu, haina budi kuoshwa kwanza. Vipi? Sio kimhemuko, bali kuoshwa kwa Neno. Sasa, tungeweza kurudi na kupata ambapo rabi huyu wa Kiyahudi... nilipokuwa nikihubiri juu ya somo hilo la maji ya farakano, yule ndama mwekundu, maji yaliyowekwa, kwamba yalifanya maji ya farakano. Na kabla hatujapata kumjia Mungu kwa imani ya kweli, inatupasa kwanza kuja kwa maji ya farakano. Naam, bwana. Inakupasa kuja kwa nini? Neno!

¹⁵⁹ Loo, hebu nione tu kama ninaweza kuzungumza tu ili kwamba mtaninii... kila mmoja atalipata. Sasa, vaeni mawazo yenu ya kiroho. Vueni kofia yenu ya vita na mvae mawazo yenu ya kiroho sasa, maana hiki hapa kitu fulani kinakuja. “Inaoshwa kabla haijapokelewa madhabahuni,” haina budi kuoshwa kwanza kwa maji ya farakano.

160 Sasa, fungueni pamoja nami upesi sana kwenye Waefeso 5, shikilieni tu mahali penu kisha mrejee nyuma, kurasa chache tu nyuma, kwenye Waefeso mlango wa 5 na kifungu cha 26:

Ili maksudi alitakase na kulisafisha... (Kanisa, analolizungumzia.)

161 Mnaona, sasa, hebu nirudi nyuma kidogo zaidi ya hapo. Turudi yapata kifungu cha 21, wakati mkiangalia:

Mnyenyekeane katika kicho cha Mungu.

162 “Nyenyeekeaneni.” Kusanyiko, jinyenyekezeni kwa mchungaji wenu. Mchungaji, jinyenyekeze kwa kusanyiko lako. Kikundi kidogo kikiinuka, usiwe upande wowote, jinyenyekeze kwa kusanyiko lote. Kusanyiko, kama mkianza katika kikundi, jinyenyekezeni kwa mchungaji wenu katika kumcha Mungu. Mnaona? Loo, ndugu! Hmm!

Enyi wake, watiini waume zenu, kama kumtii Bwana, (Maana ni bwana wako.)

163 Ni wangapi wanaojua hilo, ninyi wanawake? Hiyo ni kweli kabisa. Biblia ilisema hivyo hapo mwanzo. Ingali ni vivyo hivyo.

Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana.

Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa: naye ni mwokozi wa mwili.

164 Vivyo hivyo na mume. Nyote mnajua hilo, ninyi watu waliofunga ndoa na watu wazima, ama watoto walio na umri mkubwa kutosha kujua njia ya maisha. Vema.

...kama kumtii Bwana.

Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa: naye ni mwokozi wa mwili.

Kwa hiyo kama vile Kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo.

Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; (Kamwe usimkanyage! Ukifanya hivyo, hustahili kuwa mume. Hiyo ni kweli!)

Ili makusudi...

Sikilizeni sasa, hili hapa! Lipateni sasa:

Ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika... [Kusanyiko linasema “Neno!”—Mh.] Hmm!

165 Basi, kila mwabuduo anayepata njia ya kuingia katika *Hili* hana budi kuja kupitia Neno. Kuna wengi sana wanaokuja vinginevyo. Ninaamini katika hadithi ndogo na kadhalika, ambazo zinahusu “mama alikufa muda wa miaka mingi iliyopita naye anakungojea Mbinguni,” hilo linafanya kazi vema Neno *likiisha* kutumika. Watu wengi huja madhabahuni maana wanataka kukutana na mama yao Mbinguni. Hilo ni sawa,

unapaswa kufanya hivyo, bali hiyo siyo sababu inayokuleta madhabahuni. Unakuja madhabahuni ukizikiri dhambi zako kwa sababu Kristo alikufa badala yako, kwa Neno!

¹⁶⁶ Basi, dhabihu zozote zisizokuja kulingana na Neno hazikubaliki basi. Hiyo ni kweli? (Loo, ndugu, ninachukia kusema hivi. Loo, nachukia kulisema. Samahani kwa kulisema.) Hiyo ndiyo sababu Matendo 19 inasimama katika Biblia, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Wakasema, “Sisi . . . si kama kuna . . .”

Kasema, “Basi, mlibatizwa namna gani? Mbona hamjaingia Humu?”

¹⁶⁷ Walipitia njia nyingine mbali na Neno! Kasema, “Loo, tulipitia kwenye ile fomyula, tulibatizwa . . . Yohana.”

Akasema, “Huo hautafanya kazi. Yohana alibatiza tu kwa toba, sio kwa ondoleo la dhambi.”

¹⁶⁸ Ndipo waliposikia Haya, wakabatizwa tena. Kwa nini? Kwa Neno! “Wakaoshwa kwa maji ya Neno.” Neno lilisema, “Jina la Yesu Kristo!” Chochote kinachobandika kitu kingine chochote juu ya Hilo ni cha uongo!

¹⁶⁹ Sasa, ndugu yangu wa thamani, ninajua hii ni kanda pia. Sasa, msisimkwe. Hebu niseme hili kwa upendo wa kiungu, saa imekaribia ambapo siwezi kujizuia juu ya mambo haya tena, tumekaribia sana kwenye kule Kuja. Mnaona? “Utatu ni wa ibilisi!” Ninasema hilo BWANA ASEMA HIVI! Angalieni mahali unakotoka. Unatoka kwenye Baraza la Nikea wakati kanisa Katoliki lilipochukua mamlaka. Neno “utatu” hata halijatajwa katika Kitabu kizima cha Biblia. Na kuhusu Miungu *watatu*, hilo linatoka kuzimuni. Kuna Mungu mmoja. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁷⁰ Sasa, unasema basi, “Unaamini ya kwamba watu hawa wote ambao—ambao ni wa utatu ni wa kuzimu?” La, bwana. Ninaamini wao ni Wakristo. Lakini saa inakaribia, ndugu, ambapo wamekosea huku ni waaminifu.

¹⁷¹ Mtu yeyote, mahali popote, wakati wowote, anayetaka kulizungumzia suala hilo, aje kwangu; mhudumu yeyote, askofu, askofu mkuu, hata uwe ni nani. Na huu unarekodiwa, utaenda kote ulimwenguni. Ninaomba katika upendo wa kindugu, kwa ajili ya mtu yeyote anayenisikia kwenye kanda hii kote ulimwenguni, ambaye atanijia na kunionyesha fungu moja la maneno ya Maandiko ama aya moja katika historia yoyote (ambayo ni historia ya kweli) ambapo mtu yeyote alipata kubatizwa katika jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” mpaka walipounda dhehebu pamoja na kanisa Katoliki, nitabadilisha fundisho langu. Kila mtu alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo! Basi ndugu zangu wa thamani, macho yenu yamepofushwa msiyaone mambo hayo. Ombeni Mungu awape Nuru!

¹⁷² Sasa, kama unayo Maandiko ya kuliunga mkono, nitakuwa nikikutazamia ama kungojea simu yako. Wewe ni...wewe... Kupita kanda hii, unatembea katika ujinga wa kiroho makusudi endapo hutanipa changamoto juu ya hilo. Endapo unataka kujua Nuru ni nini na giza ni nini, hebu na tumuulize Mungu. Kumbukeni, ninasema BWANA ASEMA HIVI! Endapo unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake...Na iwapo hilo halikuwa ni kulingana na Neno, lingekuwa ni kosa. Basi iwapo si kulingana na Neno, ni jukumu lako kuja kwangu ukaninyoshe, a-ha, uone litakalotukia. A-ha. Ni kosa!

¹⁷³ Ninaamini ya kwamba maelfu mengi ya watu wa utatu wanaoamini katika Miungu watatu wameokoka, kwa sababu hawajui tofauti yoyote. Tatalifikia hilo tunapoendelea katika ujumbe.

¹⁷⁴ Sasa, ninyi nyote msizizime kanda zenu na kutoka nje ya nyumba, enyi ndugu wa utatu; sikilizeni Hili. Lakini ketini tu kimya kwa dakika chache. Unaliwajibikia kwa nafsi yako. Unaliwajibikia kwa kusanyiko lako. Unaona? Usiache kuzichukua kanda, kaa tu Nayo. Ichunguze kwa Neno uone kama ni kweli. Biblia ilisema "Hakikisha mambo yote."

¹⁷⁵ Ninajua halipendwi sana, ndivyo na Yesu alivyokuwa, ndivyo na Ujumbe ulivyokuwa, sikuzote. Mlinipenda nilipokuja na kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka miongoni mwenu, mlidhani ulikuwa ni umati mkuu, mkuu sana, na kujenga kanisa. Sasa, Yesu alifanya jambo lile lile hata siku moja ikambidi kuingia kwenye ile Kweli. Basi alipofanya hivyo, hata wale sabini walimwacha. Ndipo akawageukia wale wengine, wale kumi na wawili, na kusema, "Ninyi mtaenda pia?"

Ndipo Petro akasema maneno hayo muhimu, "Bwana, twende kwa nani, kwa kuwa Maneno Yako pekee ni ya Milele?"

¹⁷⁶ Nalo Neno la Mungu pekee ni la Milele! Basi nitafutie popote ambapo Mungu kamwe alikuwa na mtu yeyote aliyebatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu."

¹⁷⁷ Ukienda kwenye Mathayo 28:19, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," ambapo Mathayo ilisema, "Enendeni basi, mkayafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu"? Ndipo mtu yeyote anayewazia ya kwamba "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni jina, inaonyesha ya kwamba elimu yao ina kasoro. (Sasa, kwa mwanafunzi wa darasa la saba kuwaambia hilo maaskofu wanaousikiliza *Huu*.) *Baba* si jina, *Mwana* si jina, na *Roho Mtakatifu* si jina. Hivyo ni *vyeo* vinavyoenda kwa lile *Jina* (la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu), ambalo ni Yesu Kristo.

¹⁷⁸ Kumbukeni, hilo si katika hasira, hilo linasemwa katika upendo na heshima ya kiungu, pamoja na upendo na kuuhurumia Mwili wote wa Kristo ambamo ninaalikwa na

ndugu zangu wa utatu (na kote ulimwenguni) kuja kuhubiri katika kusanyiko lao. Lakini silitaji ninapokuwa miongoni mweni. Ninataka kuwa . . . Isipokuwa mniulize ninyi wenyewe, nami nitaenda kwenye parokia pamoja nanyi na kulizungumzia pamoja nawe. Lakini mbele ya kusanyiko leni, lingewavuruga. Ni jukumu lako kuupata ule Ufunuo na kwenda ukalifundishe kusanyiko lako, wewe ndiwe mchungaji wa hilo kundi. Ninazungumza na wahudumu. Iwapo hamwelewi, njoni, hebu tuketi tukashauriane. Biblia ilisema, “Thibitisheni mambo yote, lishikeni lililo jema.”

¹⁷⁹ “Bahari ya kioo,” ambapo dhabihu ilioshewa . . . Nasi tunaoshwa . . . Loo, msisahau hilo, tatalirudia baada ya kitambo kidogo, “Kuoshwa kwa maji ya Neno.” Basi inakubidi kulisikia Neno kabla hujaweza kuingia mle, kwa maana ni njia moja tu unayoweza kumwendea Mungu, hiyo ni kwa imani. Hiyo ni kweli? “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno,” tukiosha dhamira zetu. Sio kukutana na mwanadamu, sio kukutana na baba, sio kukutana na mama, sio kukutana na mtoto mchanga (hao wote ni wa kweli, tutafanya hilo), lakini kitu cha kwanza tunachopaswa kupitia ni njia ya Mungu ya kumwendea; tutaoshwa tutakapolisikia Neno la Mungu.

¹⁸⁰ Kwa imani tunatembea. *Neema*, “yale Mungu aliyokufanyia.” Hiyo ni kweli. Unamwamini Mungu, unamwamini Mungu; na mara unapoomba msamaha, tayari umesamehewa.

¹⁸¹ Kama vile nilivyokuwa nikizungumza na ndugu fulani jana, kidogo akachanganyikiwa juu yake, nami nikasema, “Angalia, ndugu, kama ulisema jambo fulani la kuudhi hisia za mke wako, papo hapo ungemwonea huruma, unasikitika ulifanya hivyo, tayari umelitubia moyoni mwako. Hiyo ni kweli. Lakini huna budi kwenda kumwambia kulihusu. Huna budi kwenda na kusema, ‘Mpenzi, na—nasikitika nilisema hivyo.’ Ndipo basi umetubu kwelikeli.” Sasa, hivyo ndivyo ilivyo na Mungu.

¹⁸² Mtu ambaye angeenda na kusema, “Niliiumiza hisia zake, haileti tofauti yoyote, nitamwambia kwamba ninasikitika, bali kweli sisikitiki,” wewe ni mnafiki. Unaona? Hiyo ni kweli. Hilo kamwe halitapokelewa na Mungu.

¹⁸³ Unapaswa kuzisikitikia dhambi zako kabisa. Ndipo ukiisha kujua umezisikitikia dhambi zako, halafu basi “Toba, na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zako, nawe utapokea msamaha, utampokea Roho Mtakatifu.” Unaona, rahisi tu, Mungu amelifanya rahisi sana.

¹⁸⁴ Hapa ninii . . . tunaona hapa katika “bahari ya kioo,” ililinganishwa na bilauri. Sasa, bahari ya kioo ni mfano, inafananishwa na bahari ya shaba. Hii ni bahari ya kioo, Mbinguni. Musa aliona kama bahari ya kioo na kufanya kile

kilichoitwa “bahari ya shaba,” madhabahu ya shaba, dhabihu ya shaba . . . madhabahu ya shaba, hasa.

185 Unajua kile shaba inachonena katika Biblia? Hukumu. Yeye alitengeneza nyoka wa shaba. *Nyoka* anamaanisha nini? Mfano wa *nyoka* ulimaanisha “dhambi iliyohukumiwa tayari,” katika bustani ya Edeni, ambapo, “Kisigino chako kitakiponda kichwa chake; kichwa chake kitakiponda kisigino.”

186 Nayo *shaba* inawakilisha “Hukumu ya Kiungu,” madhabahu ya shaba, ambapo dhabihu iliteketezwa; birika la shaba, ambapo ilioshwa kwa maji ya Neno. Mnaona? Mu- . . . Eliya, katika siku zake, alitoka na kuangalia juu, akasema, “Mbingu zinaonekana kama shaba.” (Hukumu ya Kiungu juu ya taifa lililokataliwa.) Loo, jamani! Shaba, ya shaba!

187 Sasa tuko kwenye “birika.” Nanyi mliona ya kwamba birika hili lilikuwa tupu na lilikuwa liking’aa kama bilauri. Kwa nini? Kanisa lilikuwa tayari limekombolewa!

188 Sasa, sasa, tunaona baadaye kidogo, hata hivyo, wakati wale watakatifu wa ile Dhiki wanapotokea, tunaiona tena imejaa moto. Hivi mlijua . . . Mngetaka kulisoma hilo? Hebu tufungue Ufunuo sasa, mlango wa 15, kifungu cha pili, na kusoma ambapo tunaona moto huu wa shaba tena. Vema:

Kisha nikaona malaika mwingine . . . nikaona ishara nyingine katika mbingu, (Kweli.) iliyo kubwa, na ya ajabu, malaika saba wenye . . . mapigo saba ya mwisho; maana katika hayo ghadhabu ya Mungu imetimia.

Sasa “ghadhabu” ya Mungu. Angalieni:

Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto: (Sasa, angalieni.) na wale waliokuwa wamepata ushindi juu ya yule mnyama, na sanamu yake, na juu ya alama, na kwa hesabu ya jina lake, wakasimama kando-kando ya hiyo bahari ya kioo, wenye . . . vinubi vya Mungu.

Nao wakaimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, . . .

189 Loo, mnaliona? “Wakati wa dhiki.” Loo! Mna haraka? [Kusanyiko linajibu, “La!”—Mh.] Vema, sikilizeni, hebu tuone jambo fulani hapa.

190 Tunakujaje? Hatuna budi kuja (Kanisa hili la Kimataifa) kwenye Neno hili, bahari ya kioo, maji, maji ya Neno (Hiyo ni kweli?), tulitambue Neno jinsi lilivyoandikwa. Ndipo dhabihu itapokelewa na kujazwa na Roho Mtakatifu kutoka ndani, tukimulika kwa Nuru ya wakati huo. Kutoka kwenye hili . . . Hii hapa ikitoka mahali patakatifu inaingia *hapa*, kutoka kwenye nyota kuingia *hapa*. Mnalipata?

¹⁹¹ Angalieni, sasa, mwishoni mwa wakati huu, Yohana, wakati alipoiona bahari ya shaba pale, ilikuwa “safi kama bilauri.” Ilikuwa ni kitu gani? Neno lilikuwa limeondolewa duniani, limenyakuliwa katika Kanisa, nayo ilikuwa “safi kama bilauri,” hakuna Damu tena, wakati wa Kanisa ulikuwa umekwisha.

¹⁹² Sasa, katika Ufunuo 15, masalio ya Uzao wa mwanamke, ambao walikuwa ni wale watakatifu wa ile Dhiki waliopitia kwenye ile Dhiki, walipatikana (Angalieni!) wamesimama juu ya bahari hii. Nayo ilikuwa imechangamana na moto, damu, miali myekundu ikiramba, moto wa Mungu. Walikuwa wamepata ushindi dhidi ya yule mnyama (Rumi), juu ya namba zake, juu ya hesabu ya jina lake, na juu ya sanamu yake (ule Muungano wa Makanisa), nao walikuwa wametoka. Na kupitia kwa mahubiri ya Musa na Eliya, manabii hao wawili watakaotokea kwa Israeli kuvuta ninii...kundi hili la watu, hao watakatifu wa Wakati wa ile Dhiki, huko nyuma katika wakati huo watakapoingizwa ndani, ilikuwa...

¹⁹³ Mnaona, Kanisa tayari limenyakuliwa sasa, lakini kumbukeni Mke yuko kwenye Kiti cha Enzi. Ule Wakati wa Dhiki...Waliishi katika falme, wakatoka, na kuwaleta wafalme wao wote na heshima zao na utukufu katika huu Mji. Tunapofikia kwenye Ufunuo 22, mtaona. Kama unaliandika hili na kulishikilia, tutakapolifikia utaona yale tunayomaanisha. Hatuna wakati kamwe wa kushika kila jambo dogo na kulifuatilia huku na huku, bali kugusia sehemu zake muhimu. Ndipo siku moja, labda, Bwana akipenda, tutakuwa na wakati mwingi wa kulizungumzia.

¹⁹⁴ Sasa, watakatifu hawa wa ule Wakati wa Dhiki waliotokea, walikuwa wamepitia kwenye ile dhiki kuu. (Kanisa halitapitia katika ile Dhiki kuu! Hivi mnaona wao walikuwa Utukufuni tayari?) Nao hawa hapa watakatifu wa ile Dhiki, waliotakaswa waliokuwa na...kwa kuwa ni kosa langu na lako kamwe hawakuwa wamelisikia Neno. Kama walilisikia na kulikataa, walienda moja kwa moja katika kuzimu; walitupwa nje katika giza la nje kwa sababu walilikataa Neno. Bali ikiwa hawakupata kulisikia, Mungu ni mwenye haki, Wakati wa Dhiki unawajilia.

¹⁹⁵ Sasa, angalieni kwa dakika moja tu. Watakatifu waliooshwa kwa Neno lile lile, maana ni madhahabu yale yale, ni bahari ile ile ya kioo na Neno lile lile. Ufunuo 2:5, Ufunuo 15: (ama hasa) :2 hadi :5. Angalieni, hebu kidogo tu. Sasa, sisi hatukuwapelekea Neno, hiyo ndiyo sababu walikuwa—walikuwa namna hiyo. Kamwe hatukuwapelekea Neno, tutawajibika. Kwa hiyo hatutaweza kuwapata watu wote; Kanisa halitaweza (katika wakati huu) lililo na ile Kweli. Kwa kuwa watapitia kwenye ile Dhiki, hao si Watakatifu waliokufa huko nyuma katika hizo nyakati za kanisa, kwa sababu Yeye alisema, “Walitoka katika ile Dhiki kuu,” na ile Dhiki kuu ingali ni ya usoni, Kanisa likiisha kwenda Nyumbani.

196 Loo, haya basi! Loo, ninalipenda! Sikilizeni! Hebu twende mbele kidogo, ninataka kuona walisikia Neno la namna gani. Sasa, hebu tuanze tena kwenye kifungu cha pili cha mlango wa 15.

Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto: na wale waliokuwa wamepata ushindi juu ya yule mnyama, . . . juu ya sanamu yake, . . . kwa alama yake, . . . kwa hesabu ya jina lake, wamesimama kando-kando ya hiyo hahari ya kioo, wenye . . . vinubi vya Mungu.

197 Sasa, mnaona, kamwe hawakuwa wameingia, bali walikuwa wamelisikia Neno. Walikuwa wamelisikia Neno. Sasa, sikilizeni, angalia aina ya Fundisho walilosikia, mwone kama linalingana na Kanisa sasa.

Nao waliimba wimbo wa Musa, mtumishi wa Mungu, (Hiyo ni kusema, Musa akiisha kuvuka.) na wimbo wa Mwana-kondoo, wakisema, Ni makuu na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; (Huyo Mwana-Kondoo ni nani?) Bwana Mungu Mwenyezi; ni haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa watakatifu.

198 Mnaona kile walichomtambua Yeye kuwa? Sio mtu wa tatu katika utatu, bali “Bwana Mungu Mwenyezi, Mfalme wa Watakatifu!” Sikilizeni! Mko tayari? Kifungu cha 4:

Ni nani asiye kucha, Ee Bwana, (herufi kubwa B-w-a-n-a, Elohimu) na kulitukuza . . . Ni nani aliyesalia asiye kucha, . . . na kulitukuza jina lako? . . .

199 Walioshwa kwa maji yale yale ambayo mnaoshwa kwayo sasa, kulisikia Neno, na imani na nguvu za Yesu Kristo akiwa ni Mwenyezi. Ndio Ufunuo mkamilifu hapo mwanzo. Jambo lote limefunganishwa katika Ufunuo ya kwamba Yesu Kristo ni Nani, “Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwetu!”

. . . Ni makuu na ya ajabu Jina lako, . . .

Ni nani asiye kucha . . . na kuliheshimu jina lako? wewe . . . ni . . . kwa kuwa wewe peke yako u mtakatifu: kwa maana mataifa yote watakuja na kusujudu mbele zako; kwa kuwa hukumu zako zimekwisha kufunuliwa.

200 Kwa maneno mengine: Tunaona kile inamaanisha kutolipokea, hukumu Zako zinadhihirishwa. Kwa hiyo sisi hapa tumesimama, tumeoshwa sasa, tunaoshwa kwa maji tukiisha kupitia kwenye ule Wakati wa Dhiki. Tumechukua msimamo wetu kwa ajili Yako nasi tulikuamini Wewe, na sasa tumesimama kwenye bahari ya kioo, nasi tunakuheshimu na kukutukuza Wewe kama uakisi wa Roho Wako Mtakatifu. Nazo taa Zako ni za kweli na hukumu Zako ni za haki.

201 Loo, jamani! Tungeweza kudumu juma zima juu ya hilo. “Ubatizo wa Roho Mtakatifu,” hebu tuchore kitu papa hapa

sasa, kwa dakika moja tu, nina kitu fulani ninachotaka kuchora. Sasa, hebu . . . kwa nini tusiipeleke ile pale pale tulipo.

²⁰² Sasa, kama tutaangalia, hii hapa picha kuu. Sasa, *hapa* ni Patakatifu pa patakatifu. Vema. *Hapa* ni mahali patakatifu. Na *hapa* ni pa kwanza, kabla ya kuja pale, ni—ni ile bahari.

²⁰³ Vema, sasa angalia. Tunamwendeaje Mungu? “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu,” linaloakisiwa kutoka kwenye Patakatifu pa patakatifu kuingia ndani ya mjumbe wa wakati.

²⁰⁴ Huko nyuma, na kule . . . Katika hekalu la Sulemani, lilitoa uakisi, taa hizo ziliakisi nuru yake ikaingia kwenye hilo birika la shaba. Kwa hiyo, *hapa*, malaika wa wakati wa kanisa anaakisi kuingia kwenye maji hayo kwamba Jamaa huyu ni nani *hapa*, akiakisi rehema Zake, Maneno Yake, hukumu Yake, Jina Lake. Yote yanaakisiwa humu ndani ambako unatenganishwa kwa kuliadini. Unalipata?

²⁰⁵ Angalieni jinsi hili lilivyo zuri hapa, tulikuwa tukizungumza juu yake hivi majuzi. Angalieni hapa, *hapa*, “Kwa hiyo tukiisha kuhesabiwa haki, kuhesabiwa haki kwa imani.” Vema, *mahali pa pili*, tukiisha kuoshwa, “kutakaswa.” Na, *halafu*, “kujazwa na Roho Mtakatifu.” Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu! Mnaliona? Ujumbe Wake ulikuwaje? Kuhesabiwa haki kwa kusikia; utakaso ni yale ufanyayo; na kuhusu yale uliyofanya katika kutoa shukrani kwa jambo hilo, Mungu akakutia muhuri kwa Roho Mtakatifu.

²⁰⁶ Sasa, wewe, ndugu yangu Mbaptisti, ninataka kukuuliza jambo fulani. Unasema, “Ibrahimi angalifanya nini zaidi ila kumwamini Mungu? Naye Mungu akamhesabia kwamba ana haki.”

²⁰⁷ Hivyo tu ndivyo angaliweza kufanya, papa *hapa*, alimwamini Mungu. Lakini Mungu, ili kuikubali imani yake, alimpa muhuri wa tohara na kumtia muhuri, ikionyesha ya kwamba ilimbidi Mungu ku- . . . aliikubali imani yake. Basi kama ukikiri unamwamini Mungu, wala kamwe hujatiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu . . . Waefeso 4:30, ukitaka kuliandika, Waefeso 4:30, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa Yeye mliitiwa muhuri!” Wala hujatiwa muhuri mpaka umempokea Roho Mtakatifu.

²⁰⁸ Inadumu muda gani? Hata uamsho unaofuata? “Hata ukombozi wetu, ile Siku yenyewe ya ukombozi.” Hakuna njia ya kumwacha Huyu. Huwezi kumwacha, kwa kuwa Yeye hatakuacha. Unaona? “Kwa kuwa umetiwa muhuri hata Siku ya ukombozi wako.” “Hakuna cha usoni, hakuna cha wakati uliopo, hatari, njaa, kiu, mauti, wala chochote kile, kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio ndani ya Kristo.”

Paulo alisema, “Nimeshawishika kabisa na hilo!” Haya basi! Haya basi, umetiwa muhuri hata Siku ya ukombozi wako.

209 Angalieni, hilo litafikisha kwenye Jumapili iliyopita—iliyopita tena. Hivi nina wakati? Ninaninii tu... Angalieni, angalieni hili, roho... roho, nafsi, na mwili. Vema, mnaona: mwili, nafsi, roho.

210 Sasa, hebu nifute hayo na kuweka kitu fulani hapa kwa ajili yenu. Sasa, nitachora kitu fulani hapa, sikupata nafasi ya kukichora Jumapili iliyopita kwa hiyo nimekichora hapa mimi mwenyewe kwenye kipande hiki cha karatasi ya manjano. Ninakitaka kusudi muweze kukiandika nanyi mnaweza kuona yale ninayomaanisha, sasa, ninyi mlio na penseli zenu. Sasa, *huu* ni mwili; na *hii* ni nafsi; na *huyu* ni (herufi kubwa R-o-h-o) Roho, Roho Mtakatifu. Vema. Sasa, hivyo ndivyo tumeumbwa.

211 Kama mkiangalia *hapa*, mahali patakatifu, Patakatifu pa patakatifu; *hapa* madhabahu, mahali patakatifu; na *hapa* ile bahari—ile bahari, hapo ndipo unapolisikia Neno, “Imani chanzo chake ni kusikia, kulisikia Neno,” utengano, bahari ya utengano, bahari itenganishayo. Sasa, angalieni hili. Sasa, kuna mlango mmoja tu wa kuingia *hapa*, na hiyo ni kusema inakupasa kuja *hapa* kwanza. Hiyo ni kweli?

212 Sasa, laiti ningalikuwa na nafasi, ningeweka *hapa*, “wale—wale wanawali.” Wakati ninii... Ile “Karamu ya Arusi,” nyingine. Mnaona jinsi mtu huyu alivyoingia *hapa* kwenye Karamu ya Arusi, naye aliingilia njia nyingine? Huu *hapa* ulikuwa Mlango. Yesu alisema, “Mimi ndimi Mlango.” Nayo meza hii ya arusi ilikuwa imewekwa *hapa* nao watu wameketi kuizunguka, na huyu hapa mtu mmoja hapa juu ambaye hakuwa amevaa Vazi la Arusi. Basi Mfalme alipoingia, Yeye alisema, “Uliingiaje hapa, rafiki yangu? Ulipataje kuingia hapa?” Ilionyesha ya kwamba hakuingia kwa Mlango huu. Alipitia dirishani ama akaingilia mlango wa nyuma, ama kupitia baadhi ya kanuni za imani ama dhehebu. Hakupitia kwenye Mlango!

213 Maana katika mashariki ya kale wangali wana jambo lile lile, bwana-arusi anayeenda kuoa, yeye hutoa mialiko na anampa vazi kila mtu aliyemwalika.

214 Loo, jinsi moyo wangu unavyozunguka-zunguka ninapoliwazia! “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipopewa mwaliko na Baba Yangu kwanza, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Tuliitwaje? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu majina yetu yaliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kuiona Nuru, kumpokea Roho Mtakatifu, kutembea ndani Yake. Majina yetu (wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa) yaliwekwa kwenye Kitabu wakati ule ule Jina la Mwana-Kondoo lilipowekwa mle. Biblia, tutaifikia baada ya kitambo kidogo, ilisema, “yeye aliwadanganya wote juu ya nchi

ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

²¹⁵ Angalieni, basi kama yeye...bwana arusi mwenyewe, aliposimama mlangoni. Naye huyo jamaa akaleta mwaliko, kasema, “Huu hapa.”

²¹⁶ “Asante.” Akauchukua mwaliko, akauweka hapa chini, kisha akamvalisha vazi kusudi wote wafanane. Ninapenda hilo! Mnaona? Katika nguvu za Mungu, katika Kanisa la Mungu aliye hai, matajiri, maskini, wafungwa, walio huru, weusi, wazungu, wa hudhurungi, wa manjano, wote wanafanana kwa kuwa wamevikwa vazi kwa Uweza ule ule wa Roho Mtakatifu. Mnaona?

Sasa, ilionyesha hakupita kwenye Mlango.

²¹⁷ Sasa, angalieni hapa. Loo, kama mtu alijaribu kuingia katika Patakatifu pa patakatifu (mtu fulani, mwalimu fulani wa Biblia ananiambia), kama mtu fulani alianza kuingia katika Patakatifu pa patakatifu hapa pasipo kupitia *hapa*, alikufa. Mwana wa Haruni alichukua moto wa kigeni siku moja, moto fulani wa kimadhehebu (wakati Huo haukuwa ni moto wa kimadhehebu), nao wakafia mlangoni. Hiyo ni kweli? Ama ilikuwa ni wana wa Eli, naamini. Wana wa Eli waliwaingiza ndani, wakati iliwakilisha wana wa Haruni ambaye alikuwa ni kuhani.

²¹⁸ Sasa, sasa, kunayo njia moja ya kuingia katika huo mwili. Mwili huu unaongozwaje? Sasa, angalieni kwa makini sana sasa na mziweke penseli zenu tayari. Hili *hapa* lango upande huu linaloingia mwilini: moja, mbili, tatu, nne, tano. Sasa, mmeuchora huo? Sasa, lango la kwanza *hapa* ni: kuona, kunusa, kusikia, na kuonja, na kugusa ama kuhisi (lolote linalotaka kuwa, haijalishi). Sasa, hizo ndizo hisia mwilini. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua hilo? Hisia sita zinauongoza mwili. Sasa, tunayo nafsi ukiisha kupitia *hapa*. Hisia ziko nje, huo ni mfumo wa nje.

²¹⁹ Sasa, *humu* ndani kuna moja, mbili, tatu, nne, tano, sifa tano katika nafsi. Sasa, mnataka kuziandika? Ya kwanza ni wazo, wazo. Ya pili ni dhamiri. Na ya tatu ni kumbukumbu. Na ya nne ni hoja. Na ya tano ni upendo.

²²⁰ Sasa, mlizipata zote? Endapo hamzipati, basi hebu nijue sasa. Mmeziandika zote? Kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia; mwili, hicho ndicho kiingilio cha mwili.

²²¹ Nafsi ni wazo, dhamiri, kumbukumbu, hoja, na upendo, hizo ndizo hisi ama sifa, kama vile hisi za nafsi. Nayo nafsi ni asili ya roho ambayo iko ndani, maana nafsi hutoa tu mazingira ya kile kilichoko ndani yako. Inachukua mahali pa utakaso, nafsi hupachukua, inakaa katika mazingira yale yale pale. Vema, sasa, kila...kila mtu ameandika hayo yote? Vema.

²²² Sasa, kwa lango *hili* kuna moja tu, lango moja, linaloitwa “hiari.” Wewe ndiye bosi wa yale yanayoingia huko ndani. Nayohufanya nini? Hii ni nini? *Mwili* hauna budi kusafishwa, lile birika; kutakaswa, mahali *hapa*; kujazwa na Roho Mtakatifu, *hapa*, napo hapa panakuwa ni kiti cha hukumu cha Mungu tena, ambapo Mungu anaketi moyoni mwako, nawe ukifanya kosa fulani, useme, “Loo, jamani, nimefanya kosa.”

²²³ Watu wengine husema, “Hainihukumu ku—kuwa na nywele fupi,” wanawake. “Hainihukumu kujipodoa kwa rangi za makucha ama vipodozi, ama chochote kile. Hainihukumu kwenda kwenye dansi. Hainihukumu kusema uongo mdogo usiodhuru. Hainihukumu kucheza karata katika karamu yangu ya karata.” Unajua ni kwa nini? Huna chochote cha kukuhukumu. “Hilo halidhuru dhamiri yangu.” Huna dhamiri yoyote kadiri nyoka asivyo na nyonga. Kwa hiyo unaninii tu. . . Huna dhamiri yoyote, hakuna kitu mle cha kukudhuru. Wewe ni wa ulimwengu!

²²⁴ Ila nakupa changamoto kumruhusu Yesu Kristo aingie *humu* ndani na ujaribu kufanya hivyo wakati mmoja! Ndugu, utahukumika sana utarudi nyuma na kutikisa kichwa chako kutokana na kitu hicho hakika tu kadiri ninavyosimama hapa, maana Yeye ni mtakatifu. Sikilizeni, ninayanukuu Maandiko, “Kama ukiyapenda hayo mambo yaliyo ulimwengu, mambo ya ulimwengu, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.”

²²⁵ Ilifanyikaje? Hiari. Kwa nini utaita hiyo ‘hiari,’ Ndugu Branham?” Kwa sababu inamrejesha mwanamume na mwanamke nyuma tena kama tu Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni. Juu ya nini? Ile miti miwili! Hiari, *huu* ni mauti. *Huu* ni Uzima, hiari. Utovu wa uadilifu. . . Uhuru wa kujichagulia! Mungu alimweka mwanadamu wa kwanza, Adamu na Hawa, papa hapa kwenye uhuru wa kujichagulia. Yeye anakuweka mahali papo hapo. Na njia pekee unayoweza kukiweka kitu hiki *hapa* ndani ni kwa hiari yako mwenyewe. Haleluya! Hiari yako! Inakupasa kupenda kufanya Mapenzi ya Mungu. Inakubidi kuondolea mbali mapenzi yako mwenyewe upate kuruhusu Mapenzi ya Mungu yaingie, kwa kuwa hii ndiyo njia ya pekee inayoelekeza moyoni.

²²⁶ Loo, unaweza kujiunga na kanisa, ninyi Wabaptisti na Wapresbiteri. Nanyi Wamethodisti na Pilgrim Holiness mnaweza kuja kwenye utakaso. Lakini inawabidi kupenda kufanya Mapenzi ya Mungu, hiari, kumwacha Roho Mtakatifu aingie *hapa* ndani, apate kutoa. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo. Watasema kwa lugha mpya. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa ama kula vitu vya kufisha, na kadhalika. Ishara hizi zitafuatana na hao ambao wameruhusu mapenzi yao yawe ni Mapenzi

Yangu, na kazi nifanyazo hao nao watazifanya.” Ninatumaini hamtalikosa. Kuna hiari ya kufanya Mapenzi ya Mungu. Mnaona ninalomaanisha?

²²⁷ Angalieni hapa, tukinena juu ya mahali patakatifu, lile birika. Hizi *hapa* taa, vinara vya taa (moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba), kila moja ina mwangaza. Zinapata wapi mwangaza wao? Mwangaza wao unaakisiwa wapi, inaakisi wapi? Haiakisi hapa pembeni kwenye dhehebu fulani. Inaakisi hapa nyuma kwenye Neno! Ni maji ya farakano. Whiu!

²²⁸ “Kwa kuwa habari ya toba na ondoleo la dhambi” (Luka 24:49) “zitahubiriwa katika Jina Lake kwa mataifa yote, kuanzia Yerusalemu.” Habari ya toba na ondoleo la dhambi zilifunzwaje Yerusalemu? Umbali gani? Zitaenda ulimwenguni kote. “Tubuni,” kasema Petro, katika Matendo 2:38, “mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi yenu.” Ujumbe huo utaenda kote ulimwenguni, ndipo mwisho utakuja. Ndipo mwisho utatimia, baada ya Ujumbe *huu* kwenda kote ulimwenguni.

²²⁹ Vipi, ati vinara hivi vya taa hapa vinaakisi mwangaza hapa juu ya baadhi ya Methodisti, Presbiteri, ama dhehebu la Kipentekoste? Vema, la hasha!

²³⁰ Vinaakisi *hapa* ndani kama “MIMI NIKO,” sio “Nilikuwa.” Sio watu watatu ama wanne mbalimbali, bali Mungu akiketi pale ndani akijiakisi Mwenyewe nje kwa kila moja ya makanisa hayo. Angalieni huko nyuma mwone yale waliyofanya (ndio kwanza tupitie kwenye historia), walimwakisi jinsi alivyokuwa, kama alivyo, na kama atakavyokuwa sikuzote.

²³¹ “Yeye aliyekuwako...” Mara Yohana alipopata mtazamo Wake wa kwanza, yeye alisema, “Yeye aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja, Mwenyezi Mungu, kuumba kwa Mungu, Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho.” Hiyo ndiyo Nuru ya kweli ya kuakisiwa. Mnaiona? Amina! Whiu!

²³² Baada ya saa sita, nami ni—nina...Sikilizeni, hebu tuharakishe tu kusudi muweze kuyanakili. Ninachukia tu kuwaweka muda mrefu kupita kiasi, bali sijui ni wakati gani nitakapowaona tena. Mnaona? Nami ninawatakeni mlipate hili, enyi marafiki, huu ni Uzima. Sasa, angalieni, simaanishi kwa sababu ninalisema. Iwapo mimi—iwapo ninaakisi kitu kama hicho...basi mimi...m—mnauelewa moyo wangu vibaya. Sijaribu kuakisi, “Loo, hii ni ninii tu...Si kitu nyie.” Sijaribu kufanya hivyo. Endapo hujaipokea ile Nuru, ninajaribu kuwaelekeza kwa Moja hapa. Si hii hapa mimbarani, Ile pale kwenye Kiti kile cha Enzi. Nacho hicho Kiti cha Enzi hakina budi kuingia moyoni mwako, ndipo utaona jambo lile lile hasa linaloakisiwa hapa.

²³³ *Hiki* hapa juu ni nini? Kinaakisi *Hili*. Na *hiki* ni Hili, Neno. Kuoshwa kwa maji ya Neno, kwa Neno; kuoshwa (kupitia

kwa maji ya farakano) kutoka kwa mambo ya ulimwengu—ulimwengu, kwa Neno. Neno linasema Yeye ni yule yule jana na hata milele. Halisemi, “Ni yeye yule katika wakati wa Kipentekoste, huko nyuma katika wale wanafunzi, halafu wakati mwingine Yeye akabadilika.” La, Yeye ni yule yule! Mnaona? Huwezi kulifanya liseme kitu kingine. Tungeweza kukaa tu juu ya moja ya mambo hayo kwa saa kadhaa, lakini natumaini ya kwamba mnalipata sasa. Mungu amewaita, mtalipata. Hivyo ndivyo ninavyoamini. Vema, bwana.

²³⁴ Sasa, ni kitu gani? Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; nafsi, mwili, roho; yote ni sawa. Sasa, taa inaliki Neno. Neno la kweli linaakisi nini? Taa hii ingeakisi nini, kama ilikuwa ikipata uakisi wake kutoka kwenye Utukufu huu wa Shekina? Ingeuakisi Utukufu wa Shekina. Hiyo ni kweli?

²³⁵ Kama ulipata katika seminari, nuru yako, utaakisi seminari. Ukiipata katika seminari ya Methodisti, utaakisi Umethodisti. Unaakisi! Kama uliipata katika seminari ya Kipentekoste, unaakisi Upentekoste. Lakini kama uliipata katika Utukufu wa Mungu, kwenye kichaka kilichowaka moto . . .

²³⁶ Mbona, wakati Musa alipotoka katika Uwepo Wake, ilibidi aweke kitu fulani juu ya uso wake, kwa hiyo, watu wasingeweza hata kumwanguka. Hiyo ni kweli? Alikuwa amejaa nguvu za Mungu.

²³⁷ Stefano, mtu aliyejaa Roho Mtakatifu. Kujaribu kumkomesha, mbona, ilikuwa ni kama kujaribu kuizima nyumba katika siku yenye upepo, inayowaka moto; kuuzima moto kutoka kwake . . . na nyumba inayoteketea katika siku yenye upepo. Loo, kadiri walivyo—kadiri walivyoipulizia, ndivyo ilivyo zidi kuwa mbaya. Mbona, usingeweza kumkomesha. Mara moja, walipomweka mbele ya Mahakama ya Wazee, Biblia ilisema, “Yeye alisimama pale, alionekana kama malaika.”

²³⁸ Sasa, sidhani “malaika” lilimaanisha tu yeye alikuwa ni Kiumbe fulani aliyesimama pale; lakini, malaika anajua kile hasa anachozungumzia. Vivyo hivyo na malaika yeyote, mjumbe wa wakati wa Kanisa, haimbidi kurudi nyuma na kuona yale seminari inayowazia. Yeye anajua yale Mungu aliyosema katika Biblia Yake, na nguvu zinazoakisi kuthibitisha ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Haogopi, yeye anasimulia yale hasa anayojua kwamba ni Kweli. Naye Mungu amesimama moja kwa moja pale akiliunga mkono kwa ishara zile zile na maaajabu, na kwa Neno lile lile. Huyu ni malaika!

²³⁹ Stefano alisimama pale, akasema, “Ninajua ninachozungumzia.” Kasema, “Enyi wenye shingo ngumu msiotahiriwa mioyo wala masikio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu. Kama vile baba zenu walivyofanya, nanyi ni vivyo hivyo!” Kasema, “Ni yupi kati ya baba zenu hajawaua manabii kisha kuwajengea makaburi yao?”

²⁴⁰ Ninyi madhehebu, ni nani kati yenu hajafanya jambo lile lile? Mnaona? Kujenga makasri makubwa makubwa yenye kuta nyeupe na nyumba za maiti na kadhalika huku, na kisha kuzungumza juu ya Mungu! Ninyi ndio hasa mliomweka Yeye katika nyumba ya maiti, ninyi ndio wale hasa mliomtia kaburini. Hicho ndicho kitu chenyewe kilichomlaza kaburini huko nyuma, kilikuwa ni kanisa kubwa la kasri, dhehebu, Mafarisayo na Masadukayo waliomweka mle ndani halafu wanajaribu kumjengea kumbukumbu.

²⁴¹ Hebu niwaambie ya kwamba Kristo ni Kiumbe aliye hai. Yeye si kitu kilichokufa, Yeye ni Kitu ambacho “kilifufuka kutoka kwa wafu na ni hai milele.” Loo, ndugu! Hakika! Linafanya nini? Linaakisi nini? Linaakisi kutoka *hapa*, lingekuwa ni nini? Lingeaki-... Uakisi Wake wa kweli ni nini? Basi kitu cha kwanza lingekisi, kingekuwa ni Jina Lake. Hiyo ni kweli? Lingeliakisi Jina Lake. Kitu cha pili lingekisi, kingekuwa ni nguvu Zake. Mnaona ninalomaanisha? Lingeakisi kila kitu alichu Yeye.

²⁴² Kwa hiyo kama *hii* inaakisi kwenye wakati huu *hapa*, kila kitu Yeye alichokuwa, basi Yeye ni yule yule! Whiu, utukufu! Utukufu! Ni kitu gani? Inamwakisi kama Yeye alivyokuwa, kama alivyo, kama vile atakavyokuwa sikuzote, maana inatoka moja kwa moja kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu; Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele; Mungu yeye yule, Nguvu zile zile, Utukufu ule ule, kila kitu kile kile. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Loo, ndugu!

²⁴³ Hebu twende tu mbele kidogo. Sasa, hebu tuchukue sehemu iliyosalia ya kifungu hiki cha 6 hapa, cha mlango wa 4. Ninayo maoni machache yaliyoandikwa hapa juu ya hilo, nami ninataka kuharakisha niyafikie nikiweza. Sasa, ha—hayo mengine, ukiisha kuondoka kwenye huu mla-... tukiisha kuondoka kwenye kifungu hiki, kwa urahisi linazunguka tu, likisema yale waliyofanya. Hebu tuone kama tunaweza kufikia pale.

... *kioo... bahari ya kioo...* (Sasa, tunajua hiyo ilikuwa ni nini.) *katikati ya kile kiti cha enzi,...* Wenye uhai *wanne*, wale *wanyama...*

²⁴⁴ Sasa, sasa, ni wangapi walio na toleo la marudio la Biblia? Katika toleo lenu la marudio, inasema “Wenye uhai.” Vema, nilishangaa jinsi ambavyo hii King James hapa ilisema wenye... walikuwa “*wanyama*” wanne? Vema, nikajitwalia kamusi ya Kiyunani—Kiyunani, na kurudi kwenye kamusi ya Biblia na kuona hilo lilimaanisha nini. Sasa, hii hapa maana yake. Sasa, angalieni kwa makini. Neno lililofasiriwa hapa, sasa litieni alama kusudi mweze kulichunguza, pia, mweze kuwa na uhakika. Mnaona, ninawatakeni mwandike nsemayo, na...

mkiweza na mkitaka. Vema, toleo la marudio linasema, “Wenye uhai,” ndani yake. Sasa, angalieni:

Na . . . walikuwako . . . walikuwako wenye uhai wanne wamejaa macho mbele na nyuma.

²⁴⁵ Nayo inaendelea na kutoa sifa za “wenye uhai,” ambazo tutazifikia katika dakika moja. Sasa, *mnyama* hapa amewakilishwa. Hivi una maandishi ya pambizoni katika Biblia yako, juu—juu ya *wanyama*? Kama unayo, nenda kwenye maandishi ya pambizoni. Ninaona Daktari Scofield hapa ametia yake alama. *Wanyama* linamaanisha, yeye ameandika hapa, anasema, “Viumbe hai.” Loo, jamani! Sasa, angalieni. Neno la Kiyunani hapo ni, “Z, o maradufu, m” . . . ama, “Z, o maradufu, n” ni, “Z, o maradufu, n.” Sasa, katika—katika Kiyunani, anaitwa Zoon ambalo linamaanisha “Kiumbe.”

²⁴⁶ Sasa, sivyo . . . kama ukitaka kulisoma sasa. Hatuna wakati. Nilitaka kulisoma, bali sina. Andikeni Ufunuo 11, 13, na 17. Sasa, hapo ambapo *mnyama* alipo, hiyo milango katika Ufunuo 11, 13, na 17, wanaitwa *wanyama* vivyo hivyo; bali hao *wanyama* pale, tafsiri yake ni “t-h-e-r-i-o-n,” *therion*. Hilo neno, neno la Kiyunani *therion*, ambalo linamaanisha “mnyama mwitu, asiyefugwa.” *Therion*, linamaanisha “mnyama mwitu, asiyefugwa.”

²⁴⁷ Lakini Zoon linamaanisha “Kiumbe,” mnaona, “Viumbe hai (Zoon) wanne.” Sio *wanyama* “mwitu,” *therion*; bali, “Zoon, Viumbe hai.”

²⁴⁸ Basi *therion* ni “mnyama mwitu mkali, asiyefugwa.” Kwa maneno mengine, kama utaangalia mlango wa 11, “mnyama wa Rumi.” Mlango wa 13, “Marekani.” Mlango wa 17, “Marekani na Rumi pia,” makanisa ya kimadhehebu yakiungana na Ukatoliki yanawafanya wasioongoka, wasiofugwa kwa Injili. Whiu! Wasiofugwa!

²⁴⁹ “Mungu abarikiwe, tumetoka kwenye kanisa kuu la Methodisti, dhehebu la Baptisti, Presbiteri, Pentekoste. Tunajua tunachozungumzia! Hakuna anayeongoza . . . atakayetwambia sisi!” Haya basi. Wasiofugwa! Wasioongoka! Wasiowapenda wa kwao! Wasiotaka kufanya suluhu! Wasingiziaji! Wasiotosheka! Na wenye kuwachukia walio wema! Wenye mfano wa . . .

²⁵⁰ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kupitia hilo sasa. Nami ningependa tu kukirarua kitu hicho vipande-vipande sasa hivi, bali mimi . . . kusudi lingie kwenye kanda hii, kwa vyovyote vile. Lakini hatuna wakati wa kufanya hilo. Sasa, mnaelewa. Ni wangapi wanaoelewa? Semeni “Amina!” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Mnaona, haya ni . . .

²⁵¹ *Zoon* ni nini, Z-o maradufu-n? Viumbe hai. Huenda likatamkwa, *Zoon*, Z, o maradufu, n. Ungetamkaje hilo, “Zoon”? “Zoon,” ningesema.

252 Nalo *therion* ni t-h-e-r-i-o-n, “therion,” mnaona. Kwa hiyo hilo linamaanisha “wanyama mwitu, wakali, wasiofugwa.” Hivyo ndivyo hao wanyama... Hebu chukua ninii yako... chukua kamusi yako ya Kiyunani na kurejea nyuma kabisa uone kama hilo si neno lile lile. Hebu angalia mle ulione. Chukua ninii yako—chukua kitabu chako cha kiada cha Kiyunani, chukua Emphatic Diaglott yako. Sasa, ona kama hiyo si kweli, kwamba hiyo ni kweli, kwamba linamaanisha “mnyama asiyeugwa,” katika Ufunuo 11, 13, na—na 17.

253 Na hapa katika Ufunuo 4, linamaanisha “Mwenye uhai,” sio *mnyama*; bali anaitwa “mnyama” bali siye. Jambo lile lile katika Ezekiel 1:8, 1 hadi :28, ndipo. Labda tutaliendea katika dakika moja.

Vema, “Mnyama wa mwitu, asiyeugwa, asiyeongoka.” Asiyeugwa!

254 Lakini *hawa* ni “Wenye uhai.” Hao ni nini? Hao si Malaika. Hebu niwaambie kitu, hebu tusome katika Ufunuo 5, papa hapa upande mwingine wa ukurasa. Ufunuo 5, na kifungu cha 11:

Nikaona, kisha... nikasikia sauti ya malaika wengi
 (“malaika wengi,” wengi) pande zote za kile kiti cha enzi
 (“Na” ni kiunganishi.) na za wale wenye uhai na...
 wazee:...

255 Mnaona, “na,” kiunganishi. Mnaona? Hawakuwa ni Malaika, wala hawakuwa ni wazee, walikuwa ni “Wenye uhai” kwenye Kiti cha Enzi. Loo, hivi hamlipendi hili? Wenye uhai! Wao si Malaika, maana hii inalithibitisha papa hapa, mnaona:

...nikaona, na... nikasikia sauti ya malaika wengi
 pande zote za kile kiti cha enzi na wale wenye uhai na
 wazee:...

256 Sasa kuna aina tatu mbalimbali hapa. Natumaini ninyi nyote mna mfumo huu hapa chini sasa. Sasa, ninataka kuwaonyesha. Kuna aina tatu mbalimbali zake, spishi tatu mbalimbali (Sasa, angalieni.) pande zote za kile Kiti cha Enzi.

257 Hiki *hapa* Kiti cha Enzi. Sasa, wa kwanza kwenye Kiti hiki cha Enzi ni wale Wenye uhai wanne. Nje ya hao ni wazee ishirini na wanne (namna *hiyo* tu) wanaoketi juu ya kiti cha enzi, juu ya viti vya—vyao vya enzi, viti vidogo vya enzi chini. Na pande zote za hiki, mna majeshi mengi ya Malaika wakikizunguka Kiti cha Enzi. Mnaona ninalomaanisha? Kila mmoja wao ni tofauti, mmoja kwa mwingine. Hao *hapa* Malaika; hawa *hapa* wazee; na hawa *hapa* Wenye uhai.

258 Hebu tusiondoke hapo kwa dakika moja. Hebu tushikilie hapo tu kwa dakika moja, “Wenye uhai.” Hao ni akina nani kama wao si Malaika, si wanadamu waliokombolewa? Hao ni nini? Mngetaka kujua? Hii hapa tafsiri yangu. Ninatumaini kwamba ni ya kweli; ninaamini ni kweli. Ni walinzi wa Mungu wa Kiti

Chake cha Enzi. Sasa, tutaifuta hii katika muda kidogo tu. Sasa, mnaona, wao—wao si Malaika wala wanadamu. Si wanyama mwitu. Wao ni Viumbe, “Wenye uhai.”

²⁵⁹ Sasa, hiki *hapa* Kiti cha Enzi cha Mungu. Nao *hawa* ni walinzi Wake. Hebu tusome kidogo tu cha hayo tupate kujua katika dakika chache. Mnaona, hao ni Malaika wa Mungu au walinzi wa Mungu wa Kiti Chake cha Enzi, nao... Hebu tupate... hebu ki—kidogo tu tena, hebu turejee kwenye Ezekieli. Ni—ninayo mambo haya yameandikwa hapa, nami ninachukia tu kuyapita, ninajua ya kwamba hii ni... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hebu turejee kwenye Ezekieli mlango wa kwanza, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 12 hadi cha 17, kidogo tu.

Nao walikwenda kuelekea mbele, kila mmoja wao:...

²⁶⁰ Sasa, tutaangalia katika dakika chache... Nanyi mnakumbuka hiki kifungu cha 7 hapa, sasa, angalieni jinsi walivyoonekana hapa katika kifungu cha 7 cha mlango ule ule wa Ufunuo, “wale wanne.”

Na huyu mwenye uhai wa kwanza alikuwa mfano wa simba... mwenye uhai wa pili alikuwa mfano wa ndama... mwenye uhai wa tatu alikuwa ni uso... alikuwa na... wa wanadamu, nao wenye uhai wanne walikuwa mfano... tai warukao... mwenye uhai wa nne... mfano wa tai arukaye.

²⁶¹ Sasa, wakati Ezekieli alipouona Utukufu wa Mungu, yeye aliona kitu kile kile ambacho Yohana alikiona. Mnakumbuka Jumapili iliyopita jinsi tulivyoupata “Utukufu wa Mungu,” na tukachukua picha ambapo Yeye alipigwa pamoja nasi? Mnakumbuka hilo? “Utukufu wa Mungu,” kitu kile kle ambacho Ezekieli alikiona, kitu kile kile Yohana alichooona, Hiki hapa leo hii. Kinamfanya Yesu Kristo yeye yule katika wakati wa Ezekieli, kitu kile kile kilichokuwa hapa duniani, Mungu yeye yule aliye hapa pamoja nasi leo hii; yeye yule jana, leo, na hata milele; Yeye Aliyekuwapo, Yeye Aliyepo, na Atakayekuja; kile kiingilio cha nafsi, mwili, na roho; bahari ya shaba (lile Neno), Mtakasaji nafsi yetu, na Mwenye Kujaza na Roho Mtakatifu. Kitu kile kile, mnaona, kile kile tu!

²⁶² Sasa, angalieni hili. Vema:

... naye roho... kokote walikokwenda;... sasa... kwenda, ndiko walikokwenda; nao hawakugeuka walipokwenda.

²⁶³ Wasingeweza kugeuka. Kama walikuwa wakienda *hivi*, walikuwa wakienda kama mwanadamu; kwenda *hivi*, walikuwa wakienda kama tai; kwenda *hivi*, walikuwa wakienda kama ndama; wakienda *hivi*, walikuwa wakienda kama simba. Wasingeweza kwenda nyuma! Ilibidi waende mbele kila mahali walipokwenda, kila mmoja wa hao wanyama. Sasa, *mnyama*

anamaanisha nini katika Biblia? Nguvu. Vema, linamaanisha “nguvu.”

264 Sasa:

Kwa habari za kuonekana kwao vile viumbe hai, na kuonekana kwao kulikuwa kama makaa ya moto yawakayo, kama...kwa...kuonekana kwa vinga vya moto: moto ule ulikuwa ukienda juu na kushuka chini, katikati ya vile viumbe hai; na ule moto ulikuwa mwangaza mwingi, na katika ule moto ukatoka mwangaza.

Huyo ni Mungu. Kutoka kwenye moto ulitoka Mwangaza; sio nurulimwengu, sasa, Mwangaza wa Milele.

Na vile viumbe hai walipiga mbio, na kurudi (Hebu tuone)...viumbe hai walipiga mbio, kwenda na kurudi kama kuonekana kwa kumulika kwa umeme.

Basi, nilipokuwa nikivitazama vile viumbe hai, tazama, gurudumu moja juu ya nchi, karibu na kila kimoja cha vile viumbe hai, pande zake zote nne.

Kuonekana kwake magurudumu hayo...kazi yake kulikuwa kama...rangi ya...zabarajadi: nayo yote manne yalikuwa na mfano mmoja: na kuonekana kwake na kazi yake kulikuwa...kulikuwa kwamba ni gurudumu ndani ya gurudumu lingine.

265 “Mfano ni upi hapa, Ndugu Branham? Ni kitu gani?” Inamaanisha ya kwamba walinzi hawa—walinzi hawa walikuwa ni sanduku la Mungu...Walikuwa safarini, wakiyabingirisha magurudumu wakati Ezeieli alipowaona; bali wakati Yohana alipowaona, walikuwa tayari wameingia mahali pao halisi Mbinguni. Lile sanduku la Mungu lilikuwa duniani, likibingirika kwa magurudumu, wakati wakilihamisha mahali mahali, ilimaanisha lilikuwa safarini, walilipeleka kotekote kupitia nyikani na kotekote hata hekaluni na kadhalika; bali sasa limepokelewa huko juu maana wakati wa Kanisa umekwisha, nalo limepokelewa juu Utukufuni. Mnaona? Limesimama sasa, Mbinguni, huku Malaika wote na kadhalika wamelizunguka. Tunawaona baada ya kitambo kidogo wakitoa taji zao na kuanguka kifudufudi na kumpa Yeye utukufu. Mnaona? Walikuwa ni walinzi wa Mungu wa hekalu, wa lile sanduku.

266 Sasa, kumbukeni walinzi wa Mungu wa lile sanduku, ama kiti cha rehema. Sasa, kumbukeni. Kwamba ni wangapi, Yohana aliwaona, ni wangapi? Wanne. Ni wangapi yeye a—aliwaona? Aliona wanne, pia, Viumbe hai wanne. Sasa, angalieni, wote wawili waliona ono lile lile.

267 Nayo nne ni namba ya duniani. Mlijua hilo? Ni wangapi wanaojua sasa kabla haijatubidi kulingilia, nne ni namba ya

duniani? Hakika! Kama wale Waebrania wanne... Ni duni-... Ni namba ya duniani, ya “ukombozi, ukombozi.” Sasa, wekeni hilo niani mwenu, “ukombozi,” maana nitaligusia, katika dakika moja tu, kwa nguvu sana. Mnaona, “Ukombozi!” Sasa, kulikuwako na wana watatu wa Kiebrania katika ile tanuru ya moto, bali Yule wa nne akaja, ilikuwa ni ukombozi. Lazaro alikuwa kaburini siku tatu, bali ya nne ilipofika alikombolewa. *Nne* ni namba ya Mungu ya “ukombozi,” kwa hiyo ilionyesha ya kwamba hawa Wenye uhai hapana shaka walikuwa na uhusiano fulani na dunia.

268 Ninatumaini hamna njaa kupita kiasi sasa. Ninatumaini shauku yenu ya chakula cha kiroho iko juu ki—kidogo ya ile yenu ya kawaida sasa. Mnaona? Vema.

269 Sasa, angalieni, “Wana macho” (katika Ezeieli hapa ndani) “mbele na nyuma na ndani.” Hebu tusome tu hilo. Angalieni hapa, mnaona. Mnaona humu ndani, ninaamini walinena kupitia hapa, “wenye uhai,” nyuso nne, kama tai, na mabawa, wamejaa macho nje, ndani. Angalieni hapa:

Na hawa wenye uhai wanne, na kila mmoja alikuwa na mabawa sita;...

270 “Nao waliruka,” na kadhalika, “nao walikuwa na macho nje, ndani, na nyuma.” Ilinena juu ya akili zao. Walijua yaliyokuwapo, yaliyopo, na yatakayokuja; kwa kuwa walikuwa papo hapo kwenye kile Kiti, karibu sana hata wao hawakuwa wanadamu. Walinzi wa hekalu, ama, sio walinzi wa hekalu, (Walinzi wa hekalu, wale mia moja na arobaini na nne elfu.), bali huyu hapa ni mlinzi wa kiti cha rehema, walinzi wa Kiti cha Enzi, Kiti cha Enzi, papo hapo karibu na Mungu, “Wenye uhai,” kitu cha pili kutoka kwa Mungu, wamesimama pale. Akili zao, wanajua yaliyokuwapo, yaliyopo, yatakayokuja. Walikuwa na macho “kwa nje,” ikionyesha yale wangeweza kuona, yatakayokuja; “macho kwa ndani,” wanajua kila kitu sasa; na “macho kwa nyuma,” ambayo yaliujua yaliyokuwapo. Yaliyokuwapo, yaliyopo, yatakayokuja, wakiakisi kupitia kwenye nyakati za kanisa “Yeye Aliyekuwapo, Yeye Aliyepo, na Atakayekuja; Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

271 Washikilieni sasa. Tutakifuatilia kitu hicho moja kwa moja kwenye ubao katika dakika chache. Angalieni. Sasa, hebu kidogo.

272 Inaonyesha akili zao, na ilionyesha walijua, kujua. Walijua mambo yote ya usoni na yaliyopo na yaliyopita, na yote kuyahusu!

273 Na ninii zao... Walikuwa hawachoki. Hawakuchoka kamwe. Wasingeweza kuwa chochote kinachohusiana na mwanadamu, yeye huchoka. Lakini wao walikuwa hawachoki,

waliimba “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu!” siku nzima na usiku kucha kupitia kila wakati. “Mtakatifu!”

²⁷⁴ Hebu na turudi nyuma kwa dakika moja tu. Hebu turudi nyuma, ninayo Maandiko niani mwangu, Isaya 6, upesi sana. Angalieni! Isaya aliona kitu kile kile hasa.

²⁷⁵ Kila ono la Bwana... Hivyo ndivyo ninavyosema. Ikiwa maono tuliyo nayo siku hizi si maono halisi ya Biblia, basi yamekosea. Kama yakiakisi, ama, ufunuo wowote unaomwonyesha Mungu chochote ila kile Yeye amekuwa daima, ni ufunuo wa uongo. Kanisa lote limejengwa juu yake, Mathayo 17.

²⁷⁶ Hebu tuone, Isaya, mlango wa 6. Nabii huyu kijana alikuwa akiegemea mikononi mwa huyu mfalme mzuri, naye alikuwa amemnunulia kila namna ya nguo nzuri. Naye alikuwa ni nabii, naye alikuwa ameendelea kote ambapo... Lakini siku moja huyo mfalme akafa, kwa hiyo ilimbidi—ilimbidi kujitegemea. Kwa hiyo akashuka kwenda hekaluni kuomba. Kwa sababu alianza kuondoka miongoni mwa mahali makazi ya mfalme yalipokuwa, basi, kupata ninii... Maskini mfalme mwema alikuwa ni mtu mzuri mtakatifu. Bali alitoka nje na kuona jinsi hao watu walivyokuwa wakiishi, kwa hiyo akashuka hekaluni. Sasa, sikilizeni.

Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.

²⁷⁷ Utukufu! “Upindo Wake” ni nini? Huo hapo, “Malaika, Wenye uhai,” upindo Wake uliomfuata. Upindo ndio unafuata nyuma, mnaona?

... pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.

Na juu yake walisimama maserafi: na kila mmoja wao alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, ... kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.

Wakaitana kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni BWANA wa majeshi: dunia yote imejaa. ... utukufu.

Na hapo misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.

²⁷⁸ Jamani! Loo, jamani! Hiyo inaonyesha hayo maono yanafanana kabisa kwa kila mmoja wa hao watu. “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu!” Hawachoki, usiku na mchana, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana!”

279 Hebu turudi nyuma kwa dakika moja sasa, kuwa na hakika tumewapata jamaa hawa vizuri. Mara ya kwanza ambapo walinzi hawa walitajwa, ni katika Mwanzo. Sasa, kumbukeni, kila kitu tunachohubiri hakina budi kutoka katika Mwanzo hadi Ufunuo. Wakati wowote unapotaka kuuliza swali, njoo uniulize. Unaona? Haina budi kuwa ni Biblia nzima, sio tu sehemu yake, maana Mungu habadiliki! Kile Yeye alichokuwa katika Mwanzo, ndicho alicholeo, na alichokuwa katika wakati wa katikati. Sikuzote ni yeye yule! Mnaona? Sasa, katika Mwanzo, wakati Makerubi hawa... Hivyo ndivyo nilivyokuja kuwapata, ilibidi nirudi nyuma nipate kujua kile walichokuwa hapo mwanzo.

280 Hebu tufungue Mwanzo 3:24, kwa muda kidogo tu sasa. Mwanzo, mlango wa 3 na kifungu cha 24. Mnalipenda? [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Vema. Sasa, hebu tuanzie kwenye kifungu cha 22. Na—napenda tu Hili! Hili ni jambo ninalotaka kuingiza tu humu ndani, dogo tu la ziada, bali huenda likafaa sana siku moja.

BWANA...*akasema, Tazama, huyu mtu amekuwa... mmoja wetu...*

281 Sasa, dada zangu wapendwa na wa thamani na vipenzi (hebu niliweke namna hiyo), msifikiri ninarusha sifa mbaya juu ya u—uaminifu na ile tunu adhimu, na ya thamani ya wanawake. Ninajaribu kuonyesha hapa yale mwanamke... Tafadhalini! Na kwenu nyinyi mlio kwenye kanda, ninyi wanawake mtakaokuwa mkisikiliza kanda hii, sijaribu kuwadharau, mimi ni mtumishi tu wa Bwana kuileta Nuru. Kitu duni sana na kitovu cha uadilifu kuliko vyote na kichafu kuliko vyote duniani ni mwanamke anapokuwa ni mbaya. Na kito cha thamani kuliko vyote kilichopo kwa mwanamume, mbali na wokovu wake, ni mwanamke mzuri. Nami ninamzungumzia yule aliye duni, mtovu wa uadilifu, asiye heshimika. Nami nitawaonyesha papa hapa wakati tukiwa kwenye hilo, afadhali tu niwaonyeshe ni kwa nini mimi... hata Biblia inafundisha kwamba wanawake wasiwe wahubiri, wachungaji, walimu, ama chochote kingine kanisani. Sasa, sikilizeni tu hili:

BWANA...*akasema, Basi, huyu mtu amekuwa... mmoja wetu, (Sasa, Yeye hakusema mwanamke amekuwa mmoja, "mwanamume huyu amekuwa mmoja wetu.")... na anajua mema na mabaya:... (Mwanamke hakujua; yeye alidanganywa. Mnaliona?)*

282 Sasa, Paulo alisema, "Simruhusu mwanamke kufundisha wala kuchukua mamlaka yoyote, bali...kwa kuwa Adamu aliumbwa kwanza na halafu Hawa. Naye Adamu hakudanganyika, bali mwanamke alidanganyika." Kwa hiyo hakufanyika mmoja wa Mungu. Yeye hakujua tofauti yoyote, alidanganywa. Mnalipata? Kama mnalipata, semeni, "Amina," ili mimi... [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.]

BWANA... akasema, Basi, huyu mtu amekuwa... mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; naye anajua... na sasa asiye akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele;

Kwa hiyo BWANA... akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa.

Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto urukao... upanga wa moto unaogeuka huko na huko, (Mnaona wale wenye uhai wanne? Kuna njia nne tu unazoweza kupitia, mnaona: mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini. Makerubi hawa walikuwa na upanga wa moto langoni mwa ile bustani...) kulinda njia ya mti wa uzima.

²⁸³ Maana kama mtu alipata kuushika ule Mti wa Uzima, basi angaliishi milele.

²⁸⁴ Nao hawa Makerubi, waliotajwa kwa mara ya kwanza, waliwekwa kwenye lango la mashariki la ile bustani, wakielekea pande nne. Nilipaswa kufanya hilo tofauti kidogo na hilo; siwezi kuutendea haki utaratibu wa Mungu na mambo kama hayo, lakini ni—ninaninii tu... ili kwamba mjue ninalomaanisha. Hiyo hapa bustani ya Edeni. Nalo hili ndilo lango papa hapa, linafungukia hapa juu, linafunguka kwa nje, na penye lango hili walikuwapo Makerubi. Makerubi! Basi, kumbukeni, haisemi “Kerubi,” ilisema “Makerubi.” Makerubi waliwekwa pale kulinda Nini? Mti wa Uzima. Hiyo Ndiyo waliyopaswa kulinda, Njia ya Mti wa Uzima. Njia, Njia ni Nani? [Ndugu mmoja anasema, “Yesu.”—Mh.] Inakisiwa kutoka wapi? Hapa ni mahali patakatifu, hawa hapa Makerubi.

²⁸⁵ Sasa, angalieni, andikeni haya yote. Hapa ni Patakatifu—Patakatifu... hapa ni Patakatifu pa patakatifu, Patakatifu pa patakatifu, hapa ni mahali patakatifu, na hapa ni ile bahari, na hii hapa taa za nuru, zile saba zinazoiakisi ile Nuru kutoka hapa, hapa ndani, hapa ndani, hapa ndani, hapa ndani, hapa ndani, hapa ndani. Mnaona? Zinaakisi nini? Zinalinda na kuakisi kwa Moto wa Mungu Njia ya Mti wa Uzima. Mnaona, haiwezi kutokea hapa, seminari ya Presbiteri ama seminari ya Pentekoste, haina budi kutokea Hapa, ikiakisi ile Nuru. Vema.

²⁸⁶ Mnaona, Makerubi hawa—hawa ambao Yohana aliwaona hapa hapana budi walikuwa wanavutiwa na kuulinda Mti wa Uzima, kwa hiyo hawana budi kuvutiwa na binadamu. Ama someni Mwanzo, kurejea kwenye Mwanzo tena, “Waliulinda Mti wa Uzima, wakailinda, Njia ya Uzima.” Njia ya Uzima! Njia ikoje? Yesu alisema, “Mimi ndimi hiyo Njia. Mimi ndimi Chakula kile kitokacho kwa Mungu Mbinguni. Mtu akila Chakula hiki,

ataishi milele.” Sasa ipo Njia ya kurudi kwenye Mti huo wa Uzima. Mnalipata?

²⁸⁷ Sasa, kwenye hili, ninataka kuonyesha sasa na kulihakikisha hili: ni madhabahu. Sasa, hii hapana shaka ilikuwa ni madhabahu kwenye bustani ya Edeni. Nitawaambia ni kwa nini. Mnakumbuka ya kwamba Kaini na Habili wote wawili walipanda wakaja kuabudu? Kwa hiyo hiyo inaonyesha ya kwamba madhabahu ya Mungu iliamishwa na kuwekwa kwenye bustani ya Edeni, na njia pekee ya kurudi Edeni ni kwa hiyo madhabahu. Wewe hapa tena, unaona, umerudi Edeni kupitia kwenye madhabahu. Na iliwabidi kuilinda njia hiyo pale, kuilinda, wasiweze kurudi kule mpaka madhabahu haya yatakapofunikwa kwa damu.

²⁸⁸ Ee Mungu, kwani watu hawawezi kuliona? Mnaona, hakuna kingine ila Damu! Hapana budi pawe na upatanisho, kiti cha rehema pale, madhabahu haya ya hukumu hayana budi kuwa kiti cha rehema; na wakati madhabahu haya, kama Damu ikiondolewa, patasimama kwenye Siku ile ya hukumu moto wa ghadhabu ya Mungu kuulinda Mti ule tena. Ni kitu kimoja tu kitakachoingia kwenye lango hili kuingia Edeni tena, itakuwa ni kupitia Damu ya Yesu Kristo. Mnaliona?

²⁸⁹ Sasa, angalieni. Naam, sasa Kaini . . . Loo, huyu *hapa* Kaini; na huyu *hapa* Habili, Habili. Vema. Sasa, wavulana hao wote wawili walikuja kwenye lango hili wapate kuabudu. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo hapana shaka ilikuwa ni madhabahu ya Mungu. Hiyo ni kweli? Na mbele ya madhabahu haya walijenga kibadala, madhabahu mengine. Hii *hapa* madhabahu ya kweli ya Mungu, yamo ndani ya moyo wa mwanadamu. Halafu pana madhabahu mengine *hapa* chini, ambayo yalikuwa yakiwakilisha Patakatifu pa patakatifu katika mahali patakatifu.

²⁹⁰ Loo! Loo! Ninajisikia kunena kwa lugha. Loo, jamani, Utukufu wa . . . Hivi hamwezi kuona ni kamilifu? Tazameni tu! Loo, sababu ya mimi kusema hivyo, ni kwa kuwa siwezi kupata maneno ya kutosha katika lahaja yangu ya Kiingereza kuelezea hisia zangu. Mnaona, kitu fulani hakina budi kuelezea.

²⁹¹ Kama vile Ndugu Rowe, mwanadiplomasia kwa Rais . . . karibu Marais wanne ama watano mbalimbali, yeye alisema, “Loo, Ndugu Branham, usiku mmoja nilikuja mkutanoni.” Akasema, “Sikujua la kufanya,” akasema, “Nilisimama huko nje.” Kisha akasema, “Loo,” kasema, “Nimempenda Bwana maisha yangu yote.” Akasema, “Nimekuwa ninii” (nafikiri) “Mwepiskopolia.” Akasema, “Nami nilidhani nilimjua Bwana.” Akasema, “Basi usiku mmoja niliangalia kote, sikujua la kufanya.” Kasema, “Ni—nisingeingia ndani kwa chochote kile, lakini” kasema, “Nilisikia Neno likitolewa. Loo, likaanza kuja.” Akasema, “Nikaanza kutembea huku na huku nje ya hilo hema, nikienda huku na huku,” kisha kasema “moja kwa

moja sikuweza kusubiri kuingia mlangoni, nilitambaa chini yake wakati wito wa madhabahuni ulipotolewa, nikakimbia madhabahuni na kuanguka chini, kasema, ‘Bwana, mimi ni mwenye dhambi!’” Kisha kasema, “Ndipo akanijaza kwa Roho Wake Mtakatifu.”

²⁹² Kisha kasema, “Ninaweza kuzungumza lugha nane mbalimbali,” maana ni mwanadiplomasia. Mnaona? Yeye ni... yeye yuko katika... yeye—yeye ni mwa—mwanadiplomasia wa Rais, na... kote kote kutoka kwa Woodrow Wilson kuendelea. Yeye ni mwanadiplomasia kwa kila mmoja wa Rais wetu, mwanadiplomasia wa nchi za nje, anaweza kuzungumza lugha yoyote ya kigeni. Yeye alisema, “Kwa jumla ninajua kila lugha iliyoandikwa inayojulikana ulimwenguni.” Bali kasema, “Nilikuwa nimejaa utukufu sana nisingeweza kutumia yoyote ya hizo kumsifu Yeye, kwa hiyo Bwana akanipa moja mpya kabisa kutoka Mbinguni kumsifu kwayo.” Loo! Loo! Haya basi.

²⁹³ “Kulinda lango hili.” Kaini na Habili walikuja hapa wapate kuabudu. Kwa hiyo hapana shaka walikuwa wakilinda madhabahu. Hiyo ni kweli, hawa Makerubi?

²⁹⁴ Jambo lingine, tazameni hapa ushahidi mwingine. Kaini... Iangalieni Biblia sasa! Ningewatakeni mwifungue, lakini inaninii... msijali, mnalipata kwenye Mwanzo. Vema, angalieni. Kaini alitoka, Kaini alitoka Mbele za Bwana kutoka langoni mle bustanini. Kwa hiyo hapana shaka Uwepo wa Bwana ulikuwa madhabahuni, nayo madhabahu yalikuwa penye lango. Utukufu! Loo! Vema. Ndipo makao ya Mungu, madhabahuni Pake. Sasa, Kaini alitoka Mbele za Bwana, kutoka mahali hapa. Mnataka kuliandika? Mwanzo 4:16, mkitaka kuliandika. Sasa, sasa, mmeyapata hayo yote, sivyo, mmeyaandika?

²⁹⁵ Sasa, nina kitu kingine ninachotaka kuchora hapa kwa dakika moja. Ninatumaini hakuna maharagwe yenu yoyote yatakayoungua, ama chochote kwenye ninii yenu... Sasa, angalieni... Acheni yaungue, hilo ni sawa, yataangamia kwa vyovyote vile. Hebu—hebu tuwazie hapa, hili ndilo—hili ndilo jambo lililo—lililo halisi.

²⁹⁶ Musa alitwaliwa Mbinguni, Musa, alitwaliwa kutoka duniani hata Mbinguni na akaona madhabahu ya Mungu. Hiyo ni kweli? Ninajaribu kuthibitisha hoja yangu hapa. Mnajua kile ninachotaribu kufanya, sivyo? Vema. Yeye alipaa juu Mbele za Mungu. Ndipo aliposhuka kutoka Mbele za Mungu, yeye alisema, Mu... Mungu akamwambia Musa, “Fanya kila kitu duniani mfano wa vya Mbinguni.” Hiyo ni kweli? Vema.

²⁹⁷ Sasa, basi wakati alipofanya hivyo, wakati alipolifanya lile Sanduku la Agano, aliweka Makerubi wawili kulilinda hilo sanduku. Mnaona ni kitu gani? Ilikuwa ni hekalu... ilikuwa ni madhabahu, wale walinzi wa Kiti cha Enzi. Hao Makerubi wawili, Yeye alisema “Wafinyange kwa shaba na uweke mabawa

yao yameshikana namna *hii*,” kwa sababu hivyo ndivyo hasa alivyoona Mbinguni.

²⁹⁸ Hivyo ndivyo hasa Yohana alivyoona Mbinguni, Makerubi hawa wanne pande zote nne za sanduku la Kiti cha Enzi Mbinguni. Walikuwa ni walinzi wa lile sanduku. Makerubi, walinzi wa kiti cha rehema.

²⁹⁹ Mkitaka kulisoma Andiko hilo (hatuna wakati wa kuliendea), andikeni Kutoka 25:10 hadi 22.

³⁰⁰ Sasa, hao wanakilinda kiti cha rehema wakati Mungu yuko katika Utukufu Wake wa Shekina. Utukufu wa Shekina ulikuwa wapi? Kwenye kiti cha rehema. Hiyo ni kweli? Wao wanaulinda Utukufu huo wa Shekina. Hmm! Whiu! Sikilizeni, enyi marafiki! Basi inaonyesha ya kwamba kila mhuni hawezi kuja pale na kuchukua kutoka kwa Hicho. Huna budi kujiandaa kabla hujaingia Mbele Zake.

³⁰¹ Hebu mwangalieni Haruni, katika mfano. Kabla...Sasa, kumbukeni, kusanyiko siku hizo hata lisingaliweza kupakaribia kwa njia yoyote. Bali Haruni alipoingia...Ni mara ngapi yeye alipata kuingia ndani Yake? Mara moja kwa mwaka. Yeye alikuwaje...? Ilibidi avae nguo fulani, zilizotengenezwa kwa mikono fulani, nguo za aina ya kipekee. Ilibidi avae kwa njia fulani. Alikuwa na komamanga na kengele, kwamba kila wakati alipotembea ililia “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana.” Alikuwa akikikaribia kiti cha rehema, pamoja na damu.

³⁰² Naye ilibidi atiwe mafuta kwa mafuta fulani, atiwe manukato kwa marashi fulani yaliyotengenezwa kwa ua la Uwandani. Naye Yesu alikuwa ndiye hilo Ua la Uwandani. Basi, angalieni, ua ni kitu cha kupendeza, lina manukato ndani yake. Ila kabla hayo manukato hayajatolewa, hilo ua halina budi kupondwapondwa, ndipo marashi yanakamuliwa kutoka kwenye hilo ua. Yesu, maishani mwake, yalikuwa ndiyo maisha mazuri kuliko yote yaliyopata kuishiwa; bali asingeweza kubaki hivyo, maana ilibidi alitie mafuta Kanisa Lake (lipate kuukaribia Utakatifu Wake), kwa hiyo maisha yake yalikamuliwa. Ndipo Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa juu Yake anawekwa juu ya Kanisa, Naye anamfanya yeye yule jana, leo, na hata milele, Ua la Uwandani, manukato yaliyomo. Mtu anayekaribia hapa Patakatifu pa patakatifu hana budi kutiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu yeye yule. Ndipo anapotembea, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa...” (Si akiwa na biri mdomoni mwake.) “Mtakatifu!” (Si akiwa na ukosi uliopinduliwa.) “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu,” huku amevikwa utakatifu wa Yesu Kristo. Hmm! Jinsi Wewe ulivyo wa ajabu! Loo!

³⁰³ Sasa, “kiti cha rehema.” Sasa, kiti cha rehema kiko moyoni, kiti ambamo kuangaza kwa Utukufu Wake—Wake katika watoto

Wake wote, ule Utukufu wa Shekina katika moyo wa binadamu. Huu *hapa* moyo wa binadamu. Hiyo ni kweli? Hicho ndicho kiti cha rehema? Unapitiaje kwake ukaingia Humo kupitia mifumo hii mbalimbali? Kupitia kwa hiari, hiari. Unaingia *hapa*, na kupita *pale*, kunatokea *nini*? Utukufu wa Shekina. Ni—ni nini Utukufu wa Shekina? Ni Uwepo wa Mungu. Na wakati mwanamume anapotembea, ama mwanamke, yeye anauakisi Utukufu wa Shekina. Yeye haingii kwenye vyumba vya kamari na—na kufanya mabaya, na kutoka *hapa* nje na kulikana Neno. Haidhuru watu wanasema nini, ameuelekeza moyo wake kwenye jambo moja: Mungu. Na kama yeye kweli ameitwa na Mungu basi Yesu Kristo anajiakisi Mwenyewe kupitia kwake kwa Utukufu wa Shekina, akifanya mambo yale yale Yeye aliyofanya huko nyuma; kuidhihirisha Injili ile ile, akilihubiri Neno lile lile, Neno lile lile likidhihirishwa katika kipimo kile kile lilichokuwa wakati huo, kama tu kweli lilivyokuwa kule Pententekoste linapimwa tena. Loo, jamani!

³⁰⁴ “Kiti cha rehema.” Ezekieli na Yohana wote wawili waliona mambo yale yale. Sasa, angalieni, sasa tuko karibu kufika mwisho, katika muda mfupi tu. Sasa, *hapa* ndipo ninapowataka mpate jambo fulani. Loo, tafadhali msilikose! Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba Makerubi hao walikuwa *Viumbe hai* wala sio wanyama? Walikuwa ninii . . . daraja la juu zaidi.

³⁰⁵ Sasa, hivi Malaika ni wa daraja la juu zaidi kuliko mwanadamu ama daraja la chini? Vema, bwana. Ni nani aliye mkuu zaidi, mwana wa Mungu ama Malaika? Mwana wa Mungu! Ni nani Mungu angemsikia vizuri zaidi, Malaika anayesimama pale mbele Yake akisihi apate kitu fulani, ama mmoja wenu ninyi nyote akisihi? Mmoja wenu nyote! Mnaona, kwa kuwa ninyi ni wana na binti. Hao ni—hao ni watumishi. Mnaona? Wao ni watumishi, nanyi ni wana na binti. Kwa hiyo tazameni mamlaka mliyo nayo, tunahofia tu kuyatumia.

³⁰⁶ Sasa, ninawatakeni muone *hapa*, hili ni zuri. Loo, jamani! Hebu nifikie *hapa* na kuruka baadhi ya haya nipate kuyafikia haya. Chukueni penseli zenu sasa, haya ndiyo niliyotaka sana muyachore. [Ndugu Branham anachora ubaoni—Mh.] Labda afadhali niipunguze hii kidogo. Sasa, Israeli katika safari yao, walipopiga kambi, sasa angalieni hili kwa makini, walipiga kambi: moja, mbili, tatu, nne. (La, ninaamini nimekosea.) Moja, mbili, tatu; moja, mbili, tatu; moja, mbili, tatu; moja, mbili, tatu; hivyo ndivyo walivyopiga kambi kukizunguka kiti cha rehema. Sasa, ninajua, ninyi nyote mnajua hilo, mmetazama na kusoma katika Agano la Kale.

³⁰⁷ Sasa, upande wa mashariki, upande wa mashariki, papa *hapa*, nitialiandika mpate kuwa na hakika kulipata. Mashariki, upande wa mashariki sikuzote ulikuwa ni Yuda. Hili ndilo lango, Y-u-d-a, Yuda. Na pamoja na Yuda . . . alikuwa kiongozi

wa makabila matatu pamoja na bendera yao; makabila matatu pamoja na bendera yao, bendera ya Yuda. Mnakumbuka... Ni wangapi waliopata kuona *Amri Kumi*, *Amri Kumi* ya Cecil DeMille? Vema. Ama, mlilisoma mumu humu katika Maandiko, katika Maandiko pale, hasa, huyo hapo Yuda upande wa mashariki. Vema.

³⁰⁸ Upande wa magharibi, *hapa* chini, (Sasa ninyi yaandikeni, muyasome vizuri... ni katika Kutoka, na kadhalika, wakati wakitoka.) alikuwa ni Efraimu, E-f-r. Naye alikuwa na makabila matatu pamoja na bendera yao. Vema, Efraimu.

³⁰⁹ Sasa, na upande wa kusini ilikuwa ni Rubeni, R-u-b, pamoja na makabila matatu, na bendera yao.

³¹⁰ Kisha upande wa kaskazini ulikuwa ni Dani, Dani pamoja na makabila matatu, na makabila matatu na bendera yao. Vema.

³¹¹ Sasa, hivyo ndivyo walivyopiga kambi. Sasa, kumbukeni, hebu tusome sasa katika Maandiko sasa kusudi tupate hili vizuri kabisa. Nitaanzia kwenye kifungu cha 7:

Na... mwenye uhai alifanana na simba, na wa pili... alifanana na ndama, (ama maksai mdogo) na mwenye uhai wa tatu alikuwa na uso kama wa mwanadamu, na mwenye uhai nne alikuwa... na... mwenye uhai wa nne alikuwa mfano wa tai arukaye.

Na hawa wenye uhai wanne, kila mmoja alikuwa na mabawa sita; na kwa pande zote na ndani wamejaa macho: wala hawapumziki mchana wala usiku, wakisema, Mtakatifu, mtakatifu... Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja.

Na hawa wenye uhai wakampa yeye aketiye juu ya kiti cha enzi utukufu, na heshima, na shukrani, yeye aliye hai hata milele na milele.

Ndipo hao wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele zake yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi, hao walimsujudia yeye aliye hai hata milele na milele, na kuzitupa taji zao—kuzitupa taji zao mbele ya kile kiti cha enzi, wakisema,

Wewe wastahili, Ee Bwana, kupokea utukufu... heshima... uweza: kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako hivyo... viliumbwa.

³¹² Sasa, sasa, hebu angalieni. Upande wa mashariki—upande wa mashariki, aliona uso wa namna gani? Kama ukiangalia, ilikuwa ni simba, s-i-m-b-a, hiyo ilikuwa ndiyo bendera. Hiyo ilikuwa ndiyo—hiyo ilikuwa ndiyo bendera halisi ya Yuda. Kwa sababu Yeye ni... Yesu alitokana na... Kweli! Naye ndiye Simba wa kabila la Yuda.

313 Sasa, ni wangapi waliopata kuona Zodiaki? Wengi wenu mnaajua kwamba ni nini: ile nyota. Mnaona? Hiyo ilikuwa ndiyo Biblia ya kwanza ya Mungu. Sasa, inanzia kwenye kitu gani, tarakimu ya kwanza katika zodiaki, alama ya kwanza? Ni bikira! Hiyo ni kweli? Na ya mwisho ni ipi? Leo, yule simba. Kule Kuja mara ya Kwanza na Kuja mara ya Pili kwa Kristo, yote kupitia pale. Wanapata kaa aliyekingamana . . . ama wakati uliokingamana kufikia tu ambapo ni samaki waliokingamana, ambao ndio wakati wa kaa, nasi tunaishi moja kwa moja kuupitia huo.

314 Basi angalieni katika piramidi wakati alipoijenga, katika wakati wa Henoko, kila jiwe lilikuwa mle ndani. Wangeweza kuvipima vitu hivyo kwa usahihi sana na kutabiri vita na kadhalika. Kila kitu kimekamilika ila Jiwe la Kichwa. Kwa nini? Mnaona kwenye noti yenu ya dola? Itoeni mkaitazame, kifuniko hakipo juu yake. Kwa nini? Kamwe haikufunikwa. Kristo ndiye Jiwe la Kichwa lililokataliwa, Yeye alikuwa ndiye Jiwe la Kichwa lililokataliwa. Yeye yuaja karibuni sana. Tazameni jinsi Kanisa hilo, huko nyuma kabisa katika Wakati wa Kilutheri, sehemu ya chini ni pana sana; kisha inakuwa uchache, inazidi kuwa uchache kidogo, kidogo zaidi mpaka inashuka moja kwa moja chini kabisa; ikiisha kuuacha wakati wa Kipentekoste, ndipo inashuka moja kwa moja kusudi kila jiwe lipate kuenea moja kwa moja ndani yapate kuweka kile kifuniko mle ndani, Kanisa litakalomleta Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele. Kamilifu tu iwezavyo kuwa!

Sasa, Yeye alikuwa ndiye Simba wa kabila la Yuda.

315 Sasa, mtu yeyote aliyewahi kuisoma Biblia anajua tarakimu ya Dani ilikuwa ni nini, ama kile—kile Dani . . . Loo, ninaamisha kile, naam, Dani alikuwa nini? Yake, yeye alikuwa ni tai. Hiyo ni kweli. Alikuwa ni tai. Mtu fulani amekuwa akiisoma Biblia. Yeye alikuwa ni tai.

316 Sasa, ya Rubeni ilikuwa ni mwanadamu. Alikuwa ndiye wa kwanza, aliye mnyonge kuliko kundi lote. Hivi Yakobo hakusema hivyo katika—katika Mwanzo 49? “Rubeni wewe ni malimbuko ya uwezo wangu; lakini kama maji, ulikipanda kitanda changu na kukitia najisi kitanda changu,” naye aliishi na suria wa baba yake. Mnaona, huo ni utovu wa uadilifu wa mwanadamu. Mnaona? Wanyama hawana utovu huo wa uadilifu, simba, hakuna moja ya vitu hivi vilivyo na huo; bali mwanadamu anao, anakimbia na mke wa jirani yake na kadhalika. Kama tu . . . Jambo lile lile tu, kila kitu kimekamilika.

317 Sasa, hili hapa chini, *hii*, Dani alikuwa ni tai. Na, *hii*, Rubeni alikuwa ni uso wa mwanadamu. Naye Efraimu ni ndama. Sasa, mnaipata ile picha pale? Efraimu . . . Hivyo ndivyo walivyopiga kambi, katika Biblia.

318 Sasa, kama mtaangalia, Dani ni kiongozi wa makabila matatu, Yuda ni kiongozi wa makabila matatu, Rubeni ni kiongozi wa makabila matatu, na Efraimu ni kiongozi wa makabila matatu. Tatu nne ni kumi na mbili, makabila kumi na mawili ya Israeli. Mnaona, kila moja likiwa na bendera yao; nayo bendera ya Yuda ilikuwa ni simba; bendera ya Rubeni, mtu; bendera ya Efraimu, ndama; bendera ya—ya—ya Dani ilikuwa ni tai.

319 Sasa, angalieni hapa nyuma yale Yohana aliyosema, “Na mmoja alikuwa na uso...” Hebu tusome hapa sasa, tuone tu kama si kitu kile kile kama kilichokuwa Mbinguni:

...mwenye uhai wa kwanza alikuwa mfano wa simba, (Yuda)...mwenye uhai wa pili alikuwa mfano wa ndama, (huyo ni maksai mdogo) ...mwenye uhai wa tatu alikuwa uso wa mwanadamu; na mwenye uhai wa nne alikuwa...tai arukaye.

320 Jinsi hasa makabila ya Israeli yalivyopiga kambi kote, wakilinda, wao ni walinzi wa duniani wa haki ya kulikaribia lile sanduku. Loo, Haleluya! Hivi hamlioni?

321 Hapa! Rehema, k-i-t-i c-h-a r-e-h-e-m-a, “kiti cha rehema.” Hakuna kitu kingaliweza kuja popote karibu nacho pasipo kuyapitia makabila hayo. Kupitia nini? Simba; kumpitia mtu, akili ya mwanadamu; na kumpita farasi mtenda-kazi, kama maksai; ama kumpita tai, wepesi wake. Mnaona? Mbingu, nchi, katikati, na kote kote huku; mnaona, walikuwa ni walinzi. Na juu yake ilikuwa ile Nguzo ya Moto. Ndugu, hakuna kitu kilichogusa kiti hicho cha rehema pasipo kukaribia...

322 Na kitu pekee kingaliweza kukikaribia kilikuwa ni kupitia kwa damu. Haruni aliingia mle mara moja kwa mwaka pamoja na damu. Sasa mnalionga? Sasa, angalieni. Kila kiongozi wa makabila matatu akikilinda kiti cha rehema, kile kiti cha rehema cha Agano la Kale. Sasa, mmeliandika hilo, kila mtu? Sasa, hili hapa lililo jipya kabisa, ndugu. Sikilizeni hili, ndipo tutaondoka. Sasa, kumbukeni, hao walikuwa ndio walinzi wa Agano la Kale. Ni wangapi waliopata kulisoma katika Biblia, mnaojua hiyo ni kweli? Mnaona, hao ndio walinzi wa Agano la Kale.

323 Sasa tunaishi katika wakati mwingine. Utukufu! Loo, ninaupenda wakati huu! Nanyi je? Sasa, Mungu anacho kiti cha rehema leo hii cha kulindwa. Mnaamini hilo? Kiti cha rehema kinapatikana wapi? Moyoni mwa mwanadamu. Ni wapi kilipokuja moyoni mwa mwanadamu? Kwenye siku ya Pentekoste wakati Roho Mtakatifu (ambaye ni Mungu) alipoingia katika moyo wa mwanadamu. Hiyo ni kweli? Sasa, hebu tutie alama hii hapa chini, nanyi mwe tayari kuichora mkitaka. Pentekoste, P-e-n-t, nitaweka Pentekoste. Hiki ni kiti cha rehema, Roho Mtakatifu. Tukiweke hapa...Hebu niwaambieni, tulifanye la kufaa zaidi, hebu tuweke hapa

ndani “Hua” ambaye anamaanisha... ndege, mnaona. Vema, kukilinda kiti cha rehema, sasa Mungu anao walinzi wa kiti cha rehema siku hizi? Sasa kwa kuwa... Sasa, tazameni jinsi ilivyochorwa vizuri.

³²⁴ Nilikuwa nimeketi hivi majuzi na kuona hili, nami nikaruka tu juu na kukimbia nikizunguka na kuzunguka na kuzunguka kiti, nikisema, “Utukufu! Utukufu! Utukufu! Utukufu! Utukufu,” kuzunguka, kuzunguka. Charlie, nitatenda vibaya kuliko ninavyotenda huko nwituni mara nyingine. Dada Nellie, kama ningetenda jinsi hiyo, utanifukuza nyumbani mwako upesi sana. Huh? Loo, nilikuwa tu na wakati mzuri sana. Sasa, angalieni jinsi ilivyokuwa, yale Bwana aliyofanya.

³²⁵ Sasa, Pentekoste, baada ya Pentekoste, kiliandikwa Kitabu cha (Nini?) Matendo ya Roho Mtakatifu, M-a-t-e-n-d-o. Hiyo ni kweli? Matendo kinaanza na nini, jambo la kwanza la kuingia katika wokovu? Matendo 2:38. Hili hapa la mwisho, huku. Hiyo ni kweli? “Wote walijazwa na Roho Mtakatifu na wakaanza kunena kwa lugha zingine. Naye Petro akasimama na kuwahubiria somo. Wao wakasema, ‘Tufanye nini? Tutaingiaje katika hilo?’ Akasema, Matendo 2:38, ‘Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu, Jina la Yesu Kristo.’”

³²⁶ Sasa, kumbukeni, Mungu anao walinzi kwa ajili ya hicho—kwa ajili ya hicho kiti cha rehema. Ni nini hicho kiti cha rehema wanachokilinda? Vema. M-a-t-h, Mathayo, upande wa mashariki; Luka, Luka; Marko; na Yohana. Injili zao zote nne zinakithibitisha Kitabu cha Matendo kijacho, wanakilinda mahali popote unapotaka kukiangalia.

³²⁷ Hebu tukichukue kimoja tu, kimoja tu, hatuna wakati. Ninavyo ishirini ama zaidi vilivyoandikwa hapa chini, lakini hebu tuchukue tu kimoja kwenye somo hili kwa ajili ya wokovu. Tutakuwa na wakati wa kuomba? La, ni saa saba, kwa hiyo nadhani hatutakuwa nao isipokuwa ninyi nyote mwe mnataka kuwaombea wagonjwa. Sasa, nina... ninao tu wakati mwingi sana. Mnaona? Vema.

³²⁸ Sasa, angalieni hili! Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, ni kitu gani? Namba ya duniani, ya Injili, nne. Vema, angalieni.

³²⁹ Sasa, Mathayo 28:19. 28, sasa, hapo ndipo ninyi ndugu wa utatu mnapoelekea, 28:19. Vema. Mathayo, sehemu ya mwisho ya huo mlango, ilisema, “Enendeni basi, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu”; lakini hii hapa Pentekoste inakuja, naye Petro akasema, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu.”

³³⁰ Kuna kasoro fulani hapo. “Mathayo, hivi wewe ndiwe mlinzi wa lango hilo la mashariki?”

³³¹ Likoje hilo lango? Lango ni kitu gani? Yesu. Yesu alisema, “Mlango ni mwembamba.” Hiyo ni kweli? Linaendelezwa...

Linaendelezwaje, s-t-r-a-i-t [m-l-a-n-g-o-b-a-h-a-r-i—Mf.] ama s-t-r-a-i-g-h-t [n-y-o-f-u.] *S-t-r-a-i-t* [m-l-a-n-g-o-b-a-h-a-r-i] linamaanisha “maji,” “maji ndiyo lango.” Unaingiaje? “Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo,” yanafungua hayo malango. Salaala! Whiu!

³³² “Loo, lakini, Ndugu Branham, una Mathayo 28:19 hapo chini.” Hiyo ni kweli kabisa. “Lakini, Mathayo, wewe ni mlinzi wake?”

“Hakika, mimi ni mlinzi kamili.”

³³³ Sasa fungueni Mathayo 1:18 muone inavyosema, angalieni kama inalinda—inalinda hili. Mwone kama Mathayo 1:18 inalinda Mathayo 1...28 na Matendo 2:38. Mwone kama inalilinda!

Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: . . .

“Huyu hapa Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu,” wanajaribu kusema.

. . .kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Mariamu mama yake . . .alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

Yupi? Hilo linawafanya wote wawili Mmoja!

Na hayo . . .yote . . .yamekuwa, ili . . .Na tazama, . . .

Sasa Yusufu mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, . . .asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa jinsi hii.

. . .tazama, malaika wa Bwana, akishuka, akamjia (Mwajua.) na kusema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo; maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. (Mnaona?)

Naye atazaa mwana . . .watamwita jina lake YESU: . . .

Ilikuwa . . .yote . . .yametendeka, ili litimie . . .kwa nabii . . .

Ambalo, bikira atachukua mimba . . .(Isaya 9:6) . . . bikira atachukua mimba, naye . . .atazaa mwana, nao watamwita jina lake . . .[Kusanyiko linasema, “Imanueli.”—Mh.]

³³⁴ Yeye analilinda? “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ni hizi tu: ni sifa za Jina hilo moja. Kwa hiyo huyo mlinzi husimama pale pale kulilinda. Mnalipata? Loo, jamani! Sasa, ni wangapi wanaojua hilo? Hili hapa! Yeye ni mlinzi.

³³⁵ Sasa, hebu tuninii tu . . .Ninalo lundo zima la mengine kwa ajili ya wokovu, kuyachukua haya mengine. Lakini sasa

kama tutakuwa na mstari wa maombi katika dakika moja tu, kwa yapata tu dakika kumi hebu tujaribu kitu kingine hapa kwa dakika moja. Hebu tuchukue Maandiko fulani sasa. Niliyaandika wapi haya? Haya hapa. Vema.

³³⁶ Sasa hebu tuchukue na tuone kama Mathayo hapa juu atakilinda kwa ajili ya uponyaji wa Kiroho. Chukueni penseli zenu na kadhalika sasa, kwamba mnaandika haya? Vema. Tuone kama Mathayo anagawanya... atakilinda. Hebu tuchukue Mathayo 10:1.

³³⁷ Hebu tuchukue tuone kama Yohana... moja tu ama mbili, hebu tuchukue mawili, ama moja ama mawili ya jinsi haya yalivyo, Yohana 14:12, na 15:7.

³³⁸ Tuone kama yanaulinda uponyaji wa Kiungu kukizunguka Kiti cha Enzi cha Mungu! Marko 16, Marko 11:21 na 22.

Luka 10:1 hadi 12, na Luka 11:29 hadi 31. Hebu tufuatilie wachache wake, tuone kama wanalinda, tuone kama wanalinda haki ya uponyaji wa Kiungu kama vile wanavyolilinda lango la ubatizo wa Jina la Yesu. Tunaweza kuuchukua kupitia kila mmoja wao. Hiyo ni kweli.

³³⁹ Sasa, hebu turudi nyuma tu tuone Mathayo 10:1. Ifungueni tu sasa ili sisi... kisha tutafunga tu katika dakika zingine tano, kumi, si zaidi ya hizo, Bwana akipenda. Vema, hebu tufungue Mathayo 10, tuone kama Mathayo analinda Matendo ya mitume.

³⁴⁰ Hivi mlidhani kwamba—kwamba Mungu haweki mlinzi kwenye Neno Lake? Angalia kama hao ndama, simba, mwanadamu, tai wangali hawaketi kwenye malango hayo papa hapa ardhini sasa hivi? Hizi hapa Injili, Injili nne. Mnaona? Pia, ninyi angalieni, kila walikokwenda walienda moja kwa moja mbele. Hawapingani, wanakaa pamoja. Mnaona? Mmoja huenda kwa werevu wa mwanadamu; huyo mwingine anaenda kwa wepesi wa tai; huyo mwingine ni mchungaji... Mmoja ni mwinjilisti, kuruka kama mwinjilisti, mnaona; huyo mwingine ni mchungaji; huyo mwingine ni shupavu; huyo mwingine ni mwerevu. Mnaona, kulindwa kila upande, Mungu akiilinda Injili hii ya Roho Mtakatifu! Iamini, ndugu! Vema.

³⁴¹ Sasa hebu tuchukue Mathayo 10:1.

Alipokuwa amewaita wanafunzi wake kumi na wawili, akawapa uwezo... (Hmm!)

Walikusanyika katika chumba cha juu,
Wote wakiomba katika jina Lake,
Wakabatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Ndipo nguvu za utumishi zikaja;
Aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia yayo hayo,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao.

³⁴² Loo, mtulize tu huyo mtoto mdogo kwa dakika moja tu sasa. Sikilizeni tu, sikilizeni kwa makini:

. . . naye akawapa amri juu ya pepo wachafu, . . .

³⁴³ Wachungaji wengi huwaacha roho wachafu wakae moja kwa moja kanisani mwake; mavazi ya wanawake, matendo, karamu za kadi, karamu za karata, madansi, milo ya jioni, kila . . . Loo, rehema!

. . . juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na maradhi ya kila aina.

³⁴⁴ Mnamwona mlinzi huyo ameketi pale langoni? Mlinzi wa Injili kukiunga mkono kitabu hicho cha Matendo kilichoandikwa!

³⁴⁵ Sasa, nilimsikia mwalimu mkuu sio muda mrefu uliopita, akisema, ninii . . . mmoja . . . mtu mashuhuri, mtu mzuri, nilikutana naye, nikampa mkono, ndugu mzuri. Yeye akasema, “Lakini Matendo ya mitume yalikuwa tu ni mjengo kwa ajili ya Kanisa.” Huh! Kwa maneno mengine, alikuwa na mjengo *hapa* nje, mnaona. Wakati, Matendo ya mitume kilikuwa ndani, na Injili hizi ndizo mjengo wa kukishikilia pamoja na kukilinda. Angalieni jinsi ni—ni—nia ya mwanadamu inavyoweza kufanya lolote. Ningaliwazia jambo lile lile kama haikuwa ni Yeye. Mnaona?

³⁴⁶ Mjengo, Pentekoste haikuwa ni mjengo wa Injili. Zile Injili nne ndizo mjengo wa kuiunga mkono Pentekoste! Wakiisha kuusimamisha mjengo huu, Pentekoste ikaibuka. Hiyo ni kweli? Ni kipi kilichoandikwa kwanza, Kitabu cha Matendo ama—ama mitume? Mitume. Yesu alitembea kote akitenda kazi na kubashiri yale yatakayokuja, nao Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, hao walinzi wanne wakaja nao walikuwa wakiandika kila kitu walichoona kikitimia, wakiyaelezea jinsi tu yalivyo, jinsi yalivyokuwa yanaenda kutukia, kile kilichokuwa kinaenda kutukia. Ndipo mara wakayajengea mjengo, nao Huu hapa ukaja! Amina! Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, ndio mjengo, ama kazi ya ulinzi inayolinda lile hekalu kuu, kile Kiti cha Enzi, ile Baraka ya Kipentekoste.

³⁴⁷ Sio dhehebu la Kipentekoste, ndugu, dada, yamerudi moja kwa moja nje ya kitu hicho chote, uh-hum, huko nyuma kuliko kanisa lingine lolote. Wako mbali sana kuliko Walutheri walivyokuwa. Lutheri ilishikilia vizuri kidogo kuliko wao walivyofanya, na hiyo ni kweli, na ni zaidi sana hivyo. Kweli tu kabisa, Gene, maana, sasa, sikumwona Yesu nje ya kanisa la Kilutheri, akijaribu kuingia, bali akijaribu . . . maana nafikiri Yeye kamwe hakuwako kwa kuanzia. Bali Yeye—Yeye alikuwa katika kanisa la Kipentekoste kisha akatolewa nje. Hiyo ni kweli.

Sasa, Mathayo 10:1.

348 Sasa hebu twendeni hapa kwenye Yohana 14:12 tuone kama—kama—kama Yohana ataunga mkono na kuyalinda mambo ya thamani ya Pentekoste. Katika Yohana, mlango wa 14 na kifungu cha 12, Yesu akinena:

Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; na kubwa kuliko hizi atafanya; maana Mimi naenda kwa Baba.

349 Loo, ndugu, lango hilo pale, ambapo tai alikuwa ameketi papo hapo maana hiyo ndiyo huduma ya kiinjalisti, mwajua, kuruka kama tai. Wepesi, kwenda kasi hata kwenye nchi ya kinabii huko juu, mnaona, anaweza kuona mbele na kujua mambo yaliyokuwapo, yaliyopo, na yajayo. Mnaona? Ameketi pale pale akikilinda, kasema, “Kazi nizifanyazo Mimi!” Mwangalieni huyo tai, mnaona.

350 *Huyu* hapa yule simba, mtumishi. Yesu aliwapa uweza. Naye analinda, Yeye analinda Matendo 2:38. Yeye analiunga mkono papo hapo juu, yule simba.

351 Huu hapa unakuja wepesi wa Injili, pamoja na huyu tai, akisema, “Hizi kazi nifanyazo ninyi nanyi mtazifanya. Nyingi kuliko hizi mtafanya,” kuruka kote ulimwenguni pamoja Nayo! Kama yule hua aliyekuwa na kichwa cha mwenziwe kilichong’olewa, na kumwagiliwa, kuinyunyizia damu ardhini, akilia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana,” kumtakasa mwenye ukoma. Naam.

352 Sasa, nina lingine pale, Yohana 15:7. Hebu tufungue moja kwa moja kwenye mlango wa 15, kifungu cha 7:

Ninyi mkikaa ndani yangu, sasa, na maneno yangu. . . (sio neno la seminari). . . maneno yangu yakae ndani yenu, mtaomba mtakalo nanyi mtatendewa.

353 Hiyo ni kweli? Basi Injili hiyo imelindwa papa hapa. Baraka hii ya Kipentekoste imelindwa na Yohana na Injili yake; imelindwa na Mathayo, Injili yake.

354 Sasa, hebu tushuke twende kwenye Injili inayofuata, Marko, mlango wa 16, tuone kama Marko aliilinda Baraka hii ya Kipentekoste. Marko, mlango wa 16. Sasa, hebu tuanzie hapa yapata ninii. . . baada. . . inapozungumzia juu ya ufufuo. Sasa, hebu tuendeleo kushuka mpaka tufikie takribani ki—kifungu cha 14 cha Marko 16:

Baadaye akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.

355 Hawakuwasadiki wale waliokuwa wakijaribu kuwaambia ujumbe. Mnaona, hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Watu walio na ushuhuda wa Roho Mtakatifu; watu walisema, “Upuuzi, hao

ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha.” Basi akawakemea kwa ugumu wa mioyo yao, mnaona, na kutokuamini kwao; waliokuwa wamemjua katika kufufuka Kwake.

Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

³⁵⁶ Kitu gani? Kuihubiri ile...hii...kuna Injili moja tu; walinzi wanne. “Mkaihubiri Injili hii kwa kila kiumbe!” Sasa, kumbukeni, Yeye anawachukua wote wawili, walinzi wote wanne (Mathayo, Marko, Luka, na Yohana), mnaona, “Mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe!”

Aminiye na kubatizwa ataokoka; na asiyeamini, atahukumiwa. (Mnaona, inakubidi kuingia ubatizo huu hapa.)

Aminiye na kubatizwa ataokoka;...asiyeamini, atahukumiwa. (Loo, ndugu, amini, tafadhali!)

Na...(Kiunganishi, kuziunganisha sentensi hizo zingine pamoja)...Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio;...

³⁵⁷ Vema, sasa, hebu tuone, Methodisti inasema nini? “Kama unaweza kupaza sauti, uishi maisha mema.” Wabaptisti wanasema, “Iweni tu na imani na mkabatizwe.” Mwepiskopolia anasema, “Simama kama Mwepiskopolia, namna hiyo, kisha uiname wakati kukariri kunapoendelea.” Mkatoliki anasema, “Sema ‘Salamu Maria.’” Mpentekoste anasema, “Jiunge na dhehebu letu. Batizwa katika Jina la ‘Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.’” Huyu unaenda. Unaona?

...ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Katika jina langu...(Hmm. Hakuna “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu” kuhusu hilo)...katika Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;

Watahika nyoka;...wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. (Amina! Loo, ndugu!)

³⁵⁸ Sasa turudi moja kwa moja kwenye wa 11, na basi karibu tuko tayari kufunga. Mathayo 11, nami nina 20 na 21, Yesu akizungumza. Haya yote ni Yesu akizungumza, sasa, sio mmoja wao bali ni yale Yesu anayozungumza, kila moja.

Hata kesho yake walipofika...karibu na Bethania, aliona njaa:

Akaona kwa mbali mtini...

³⁵⁹ Hapo ndipo alipoulaani huo mti (hiyo ni Mathayo 21). Nina...:12, kunradhi tafadhali. Marko 11:21 na 22:

Petro akakumbuka habari yake, akamwambia, Mwalimu, tazama, mtini ulioulalani njiani...

Yesu akamjibu, akamwambia, *Mwaminini Mungu.*
(Mnaona?)

*Kwa kuwa amin, nawaambia, (basi, iko ndani)...
nawaambia, Yeyote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka,
ukatupwe baharini; wala asione shaka moyoni mwake,
ila... amini kwamba hayo asemayo yatatukia,
anaweza kupata... yatakuwa yake yoyote asemayo.*

³⁶⁰ Jamani, lango la kusini limelindwa na ndama. Lango la kaskazini limelindwa na simba, lango la kaskazini... Namaanisha lango la mashariki. Nalo lango la kaskazini limelindwa na tai arukaye, Yohana, yule mwinjilisti. Halafu tabibu upande *huu*, Luka, mwanadamu.

³⁶¹ Sasa, hebu tuone yale Luka asemayo. Hebu chukueni Luka, mlango wa kwanza... Ninaamini tuna Luka 10:1 hadi 12, ni lile—ni lile agizo. Nyote mnajua hilo ni nini, lakini... Luka, mlango wa 10, na 1 hadi 12. Vema, tungeendelea moja kwa moja na kuyasoma yote, bali hatutakuwa na muda wa kufanya hivyo. “Enendeni...” Nitaanzia kwenye kifungu cha 3:

Enendeni: angalieni, nawatuma kama wana kondoo kati ya mbwa-mwitu.

Msichukue mfuko, wala mkoba,...

³⁶² Mnaona, “Msiende kwa jina fulani la kimadhehebu. Nendeni jinsi ninavyowatuma. Mnaona? Msiende na hakikisho kwamba mtapata dola mia moja elfu kwa ajili ya uamsho huu; msipozipata, msinde. Mnaona. Pageni miamsho yenu.” Yeye alisema, “Nendeni ninakowatuma.” Mnaona.

*Msichukue mfuko, wala mkoba, wala viatu:...
msimwamkie mtu njiani.*

³⁶³ “Usisimame na kusema, ‘Nitaenda kule nione jinsi ninii... hawa wanavyoendelea... jinsi hawa...’ Nendeni moja kwa moja ninakowatuma. Msimsikilize mtu mwingine yeyote.”

Na nyumba yoyote mtakayoingia,... semeni, Amani iwemo nyumbani humu.

*... akiwemo mwana wa amani, amani yenu itarudi...
itamkalia: la, hayupo, amani yenu itarudi kweni.*

Basi kwenye saa hiyo hiyo kaeni katika nyumba iyo hiyo (hasa), mkila na kunywa vya kwao: (Sasa, upuuzi huu wote juu ya “kutokula nyama, na kadhalika.” Jamani, salaala! Mnaona?) maana, mtenda kazi anastahili kupewa ujira wake. Msihame-hame kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii.

³⁶⁴ Uende na akina Jones leo, kwenye chakula cha jioni, na kwenda pamoja na—na wengine wawili kesho yake, na wengine wawili wakati huo mwingine. “Ninyi kaeni papo hapo!”

Hapo ni wakati ninapoenda kwenye mkutano, mwajua, ndio sababu nakaa moja kwa moja kwenye hoteli, na kukaa pale pale, hapo ndipo hasa ninapopata amani. Mnaona? Msiende kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii!

Na mji wo wote mtakaouingia, huko wakiwakaribisha, vileni vyakula viwekwavyo mbele yenu:

Waponyeni wagonjwa—waponyeni wagonjwa waliomo, waambieni, Ufalme ni...Mungu umekuja karibu nanyi.

365 Lakini sasa, vema, hebu nisome kifungu kifuatacho:

Na mji wo wote mtakaoingia, nao hawawakaribishi, tokeni nje...ya mji katika...iyo hiyo...siku,...

Hata mavumbi ya mji wenu yaliyogandamana na—nasi, sisi...(Hebu tuone sasa.)...Hata... Na...Hata mavumbi ya mji wenu yaliyogandamana na miguu yetu tunayakung'ua juu yenu: Lakini jueni hili, ya kwamba ufalme wa Mungu umekaribia.

Nawaambia ya kwamba itakuwa rahisi zaidi Sodoma kuistahimili siku hiyo ya hukumu, kuliko mji huo.

366 Loo, ndugu, pamoja na hakikisho hilo lililobarikiwa! Wasipoona, wasipowapokea, endeleeni, semeni tu, “Vema, kama hamnitaki, nitapangusa tu mavumbi, na kutoka kwenye viatu vyangu, na niondoke mara moja.” Kwa maneno mengine, useme, “Kamwe sikuchukua chochote; kama nikila chochote, nitakilipia, na tuendele.” Akasema, “Amin...” Na kila mmoja wa miji hiyo waliyopitia wala hawakupokelewa, kila mmoja wao umezama wala haupo leo hii. Na kila mji—mji uliowapokea, unasimama hata wa leo. Haya basi.

367 Sasa, moja zaidi, kisha kufunga. Hebu tuone, tuna 10. 11:29 hadi 31, Luka 11:29 hadi 31, ndipo tutafunga. Loo, nalipenda Hili!

Na makutano walipokuwa wamekusanyika...

368 Hebu tuone, hivi nina ninii...Hiyo ni Luka, Luka 11:29? Naam, nadhani hii ingekuwa ndiyo. Naam:

Na makutano walipokuwa wakikusanyikia, alianza kusema, Kizazi hiki ni kizazi kibaya: kinachotafuta ishara; wala hakutakuwa...na... ishara...hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona.

Maana, kama vile Yona alivyokuwa ishara kwa Ninawi, ndiyo...ndiyo atakavyokuwa Mwana wa Adamu kwa kizazi hiki.

Malkia wa kusini atasimama...hukumuni pamoja na...kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa na hatia; wakati yeye alikuja kutoka ncha za dunia aisikie

hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na kizazi hiki, nao... watakihukumu kuwa na hatia: kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

369 Ninasema nini sasa? Nafunga, itanibidi kuyaachilia hayo mengine. Lakini, katika kufunga, ninataka kusema hili kwa sababu nimewaweka muda mrefu sana. Yeye anasema nini hapa? “Siku itakuja ambayo kizazi kiovu na, cha zinaa,” (Sasa kumbukeni!) “kitatafuta ishara. Na hiki ni kizazi kiovu na cha zinaa.” Naye alisema, “Kizazi hicho kitapokea ishara.” Angalieni jinsi inavyolingana na hayo mengine ya Biblia, ile ishara ya Yona. “Yona alikuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku; vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika tumbo la du—dunia siku tatu mchana na usiku.” Itakuwa nini? Ishara ya ufufuo. Mnaona? Ishara ya ufufuo itafanywa katika kizazi kiovu na cha zinaa, nayo ilifanywa katika Kitabu cha Matendo. Yesu alifufuka katika wafu, akaja ndani ya Petro, Yakobo, na Yohana, na wale mitume, nao wakakifanya Kitabu hiki cha Matendo (hayakuwa ni matendo ya mitume), yalikuwa ni matendo ya Roho Mtakatifu akitenda kazi *ndani ya* mitume.

370 Sio mtu siku hizi; ni Roho Mtakatifu akitenda kazi kupitia kwa mtu, ama watu, mnaona, ndiye anayetenda hizo kazi. Si huyo mtu; huyo mtu ni chombo tu, mnaona, bali Roho Mtakatifu ndiye Mafuta yaliyomo kwenye chombo hicho. Mnaona?

371 Basi angalieni waliyofanya, angalieni ishara walizofanya za Yesu. Ilibidi wawatambue maana... Wa—walikuwa hawana maarifa, hawana elimu, Petro na Yohana. Lakini iliwabidi kuwatambua, waliishakuwa pamoja na Yesu! Walifanya mambo aliyoyafanya Yeye. Kwa hiyo, mnaona, kila Kitabu katika Biblia, kila... vile Vitabu vinne, zile Injili nne zinalinda Baraka za Kipentekoste pamoja na kila Andiko kuunga mkono yale hasa waliyosema. Na sasa Matendo ya mitume yanathibitisha leo hii pamoja na zile Injili nne ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnampenda?

Walikusanyika katika chumba cha juu,
Wote wakiomba katika jina Lake,
Walibatizwa na Roho Mtakatifu,
Na nguvu za utumishi zikaja;
Aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia yayo hayo,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao.

372 Hebu niuimbe:

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha
juu,
Wote wakiomba katika jina Lake,
Walibatizwa na Roho Mtakatifu,
Na nguvu za utumishi zikaja; (Hizo ndizo
tunazohitaji siku hizi.)
Aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia yayo hayo,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Hawa watu huenda wasijifunze kuwa, (Sio . . .
Kama tu Petro, Yakobo, na Yohana.)
Wala kujivunia sifa za ulimwengu,
Wote wamepokea Pentekoste yao,
Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
Nao wanatangaza sasa, karibu na mbali pia,
Nguvu Zake zingali ni zile zile, (Kama tu
zilivyokuwa.)
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Loo, nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Loo, njoni, ndugu zangu, mwitafute baraka hii
Itakayousafisha moyo wako na dhambi,
Itakayoanzisha mlilo wa kengele za furaha
Na itaendelea kuiwasha moto nafsi yako;
Loo, inawaka sasa ndani ya moyo wangu
Loo, Jina Lake litukuzwe,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha kwamba ninaweza kusema mimi
ni mmoja wao; Haleluya!
Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao.

³⁷³ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Huwadanganya wengi sana wa watu hao. Hivi . . . Watu wengi hapa nje mtaani wanaohudhuria kanisa, walio wafuasi wa kanisa, wamedanganyika kama Hawa alivyokuwa hapo mwanzo. Hawajui tofauti yoyote.

³⁷⁴ Loo, njoo uuchukue ule Mti wa Uzima! Sasa, badala ya wale Makerubi . . . Sasa, ninataka kusema jambo fulani. Badala

ya Makerubi hao kukilinda Kiti hiki cha Enzi, wao wako hapa nje wakitafuta, wakijaribu kusukuma watu, wawalinde kwenye kile Kiti cha Enzi, wakijaribu kuwapitisha langoni, waurudie ule Mti wa Uzima tena wapate kuula Huu. Yesu alisema, “Mimi ndimi Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni. Yeye aulaye Mwili Wangu na kunywa Damu Yangu yuna Uzima wa Milele nami nitamfufua katika siku ya mwisho.” Hiyo ni kweli. Loo, nina furaha sana!

³⁷⁵ Ni wangapi wagonjwa walio chumbani? Hebu tuone mikono yenu, inueni mikono yenu. Vema. Ni wangapi walio... Hiyo ni... Hivi—hivi nilimwelewa Billy? Yuko wapi? Je, alisambaza kadi za maombi? Hivi wewe...? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Vema, ni nani aliye... [Sehemu tupu kwenye kanda.]

³⁷⁶ Sasa, angalieni huku, ninyi nyote. Sasa, hivyo ni kama tu ilivyo inapokuja chini ya Utukufu hapa, mnaona. Mnaona? Mnaona? Inakuja... Ni hii Nuru hapa. Unasogea hapa, unaona. Sasa, angalia, ni ninii tu—ni uakisi tu, uakisi tu, ndio huo, mnaona. Sio ile Nuru. Hii hapa Nuru ikining’inia papa hapa, mnaona, papa hapa kwenye mwanamke huyu. Ilitokea tu niliishika nami nikafikiri ilikuwa juu ya mtu fulani.

³⁷⁷ Sasa, mnamwona mmoja nami ninawaona wawili. Mmoja wao ni wa kawaida, na Huyo mwingine ni wa Kimbinguni. Yupo mtu anayeketi upande wa nje hapa, kwenye mstari huu akiangalia kwenye Nuru ile. Ilingusa. Yeye ametoka Seymour, Indiana, naye yuna... alikuwa na kiharusi. Iwapo utaamini, bwana, Mungu atakuponya kiharusi hicho. Amina! Amini sasa!

³⁷⁸ Unaamini kwa moyo wako wote? Basi ikiwa Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, atanijalilia kufanya jambo fulani kukuthibitishia ya kwamba ni Mungu, basi utaamini kwa moyo wako wote? Ugonjwa wa—wako ni ugonjwa wa wasiwasi uliosababishwa na ku—ku—kukoma hedhi. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Pia hutoki hapa.

³⁷⁹ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... shida yako ni nini? Na, kwa kufanya hivyo, kwamba Yeye angekupa afya? [Sehemu tupu kwenye kanda.]... angeweza kukupa afya, kwa sababu si wewe unayetaka kuwa mzima, ni mwanao. Mnaona? Yeye yuko Virginia. Unaamini kwamba ninaweza kukwambia shida aliyo nayo, kwa msaada wa Mungu? Yuna vidonda. Hiyo ni kweli. Pia ana tatizo lingine, yeye hajaokoka. Nawe unamwombea. Sasa, Bibi Baker, rudi Somerset na uamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atampa afya. [Sehemu tupu kwenye kanda.]...?... kukupa afya, unamkubali kama Mponya wako? Kama ungeweza... [Sehemu tupu kwenye kanda.]... mponyaji. Paulo alisema wakati mmoja... [Sehemu tupu kwenye kanda.]

³⁸⁰ Kusanyiko hili la watu ambao wamesikiliza kwa makini sana mpaka kwenye muda huu wote hapa wa siku, Bwana, sasa,

Bwana Mungu, ninaomba ya kwamba rehema na wema Wako utakaa juu yao.

³⁸¹ Shetani, ninakupa changamoto katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani ya watu hawa! Wamekaa kuisikiliza Injili. Huwezi kuwashikilia tena. Jalia nguvu za ibilisi zilizowafunga watu hawa, ziondoke!



UFUNUO, MLANGO WA NNE SEHEMU YA III SWA61-0108

(Revelation, Chapter Four Part III)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 8 Januari, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org